# Nipashe

Jumatano Oktoba 16, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580050

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

itter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Mafuriko yaua wanafunzi tisa wa shule za msingi tatu

UKURASA 3


18 siasa

TUJIKUMBUSHE

SHAKIL AFRIDI

• Ni Daktari aliyeisaidia CIA kumpata Bin Laden

Huku daktari huyo akionekana kuwa shujaa Marekani, nchini Pakistan anaonekana kama msaliti ambaye alilitetea aibu taifa hilo

UKURASA 18

MATOKEO DARASA LA 7

# Kanda ya Ziwa yaibuka kinara



• **Yatoa** shule zote bora, wavulana 10 bora, wasichana 8, wasimamizi, walimu matatani kwa udanganyifu...*Uk. 2*




UKURASA 2

## Lissu asisitiza kugombea urais

UKURASA 3

Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu uandikishaji kwenye daftari la wapigakura kwa ajili ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa. (Wa pili kushoto) ni Katibu Mkuu wa Chama hicho, Dk. Vincent Mashinji na Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, Salum Mwalimu. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mbowe aanika sababu kusuasua uandikishaji

**MICHEZO** SIMBA, YANGA HAKUNA KULALA UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Kanda ya Ziwa kinara darasa la saba

**Na Romana Mallya**

MIKOA ya Kanda ya Ziwa imeng'ara katika matokeo ya mitihani ya darasa la saba baada ya kutoa watahiniwa tisa bora kitaifa, akiwamo mshindi wa jumla wa mwaka huu.

Wakati mikoa hiyo ikifunika, matokeo hayo yaliyotangazwa jana jijini Dar es Salaam na Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani la Taifa (Necta), Dk. Charles Msonde, yanaonyesha ufaulu wa jumla umepanda kwa asilimia 3.78 kulinganisha na mwaka jana.

Hata hivyo, katika mpangilio wa mikoa, halmashauri, manispaa na majiji kiufaulu, Mkoa wa Dar es Salaam unaongoza kitaifa ukiwa na idadi ya watahiniwa 74,940 ambapo waliofaulu mtihani huo ni 69,907 sawa na asilimia 93.28.

Katibu Mtendaji huyo alisema watahiniwa 947,077 wa shule za msingi walisajiliwa kuufanya mitihani wakiwamo wasichana 495,937 (asilimia 52.37) na wavulana 451,140 sawa na asilimia 47.63, watahiniwa waliosajiliwa wenye mahitaji maalum walikuwa 2,679 sawa na asilimia 0.28.

Dk. Msonde alisema watahiniwa 933,369 sawa na asilimia 98.55, wakiwamo wasichana 489,966 sawa na asilimia 98.80 na wavulana ni 443,403 sawa na asilimia 98.29 ya waliosajiliwa, walifanya mitihani.

Watahiniwa 13,708 sawa na asilimia 1.45 hawakuufanya mtihani huo, kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo utoro na ugonjwa. Kati yao wasichana ni 5,971 na wavulana 7,737.

Alisema ufaulu wa jumla unaonyesha watahiniwa 759,737 kati ya 933,369

INAENDELEA UK.8



Madereva wa Bajaj wakiziosha kwa kutumia maji yaliyotuama katika eneo la Jangwani jana, kutokana na mvua zilizonyesha, jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mbowe aanika sababu kusuasua uandikishaji

**Na Waandishi Wetu**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kimedai mdororo wa uandikishaji wapigakura unaofanyika sasa nchini kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa, umetokana na serikali kuzuia vyama vya siasa kufanya mikutano ya hadhara.

Mwenyekiti wa wa Taifa wa Chadema na Kiongozi wa Kambo Rasmi ya Upinzani Bungeni, Freeman Mbowe, alisema hayo jana jijinui Dar es Salaam, alipozungumza na waandishi wa habari.

Alisema vyama vya siasa vina nafasi kubwa kuhamasisha wananchi kujitokeza kushiriki kujiandikisha na kupiga kura na kwamba kwa kuvizuia kufanya mikutano ni kupunguza hamasa kwa wananchi kushiriki uchaguzi.

"Nataka kuwakumbusha viongozi kuwa mdororo unaoendelea nchini ni matokeo ya kauli, matendo na tabia zao za mara kwa mara. Wamewalazimisha Watanzania waamini kwamba chama pekee kinachostahili kuchaguliwa ni Chama cha Mapinduzi," alisema Mbowe ambaye pia ni Mbunge wa Hai.

Alisema hali hiyo inaweza kuendelea hata katika uchaguzi mkuu wa mwakani iwapo hatua ya kuzuia vyama kufanya mikutano itaendelea, hali ambayo inawafanya wananchi kushindwa kulinganisha utofauti wa kiongozi kati ya chama kimoja na chama kingine na kusababisha kushindwa pia kufanya uchaguzi.

Kuhusu ushiriki wa chama hicho katika uchaguzi wa serikali za mitaa, alisema hakina mpango wa kususia kama kilivyofanya uchaguzi kadhaa ikiwamo mdogo wa wabunge na madiwani kwa kuwa una umuhimu wa kipekee kwa wananchi. Aliwataka wananchi kujitokeza kwa wingi kujiandikisha.

**WAHAHA KUHAMASISHA**

ZIKIWA zimebaki siku mbili kumalizika kwa muda wa kujiandikisha kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa uliopangwa kufanyika Novemba 24, mwaka huu, viongozi wameendelea kuhaha kukamasisha wananchi kujitokeza na kujiandikisha.

Wakati viongozi hao wakihaha, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) yenye jukumu la kuratibu uchaguzi huo, imesema hadi juzi asilimia 68 ya wananchi walikuwa wamejiandikisha.

Katika kuhakikisha lengo linatimia, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, jana alikimbilia katika magulio na maeneo yenye watu wengi, huku akiagiza maofisa waandikishaji kuhamisha vituo kwa dharura na kuwafuata wafanyabiashara ili kujiandikisha.

Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Dar es Salaam inatajwa kuwa ndiyo iliyo chini kwa uandikishaji ikilinganishwa na mikoa mingine.

Kiwango cha chini cha uandikishaji katika mkoa huo kinawaumiza vichwa viongozi na sasa kila wilaya na hata ngazi ya mkoa, wamekuwa wakipita huku na huko hasa maeneo yenye shughuli nyingi za kiuchumi na mwingiliano wa watu kuwahamasisha kujiandikisha.

Alipokwenda katika Soko la Kimataifa la Kumbukumbu ya King

INAENDELEA UK.8

# Matatani udanganyifu mitihani darasa la saba

**Na Romana Mallya**

WATU 42 wakiwamo walimu wakuu, wasimamizi wa mitihani na walinzi, wameingia matatani kwa kuhusika katika udanganyifu wa mtihani wa darasa la saba uliofanyika mwezi uliopita.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Mitihani (Necta), Dk. Charles Msonde, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akitangaza matokeo ya mtihani huo ambao watahiniwa 947,077 wa shule za msingi waliosajiliwa, kati yao 933,369 walifanya mtihani huo, sawa na asilimia 98.55.

Alisema kutokana na udanganyifu huo tayari mamlaka za ajira na zinazohusika na sheria zimearifiwa na hatua zimeshaanza kuchukuliwa.

"Septemba 12, wakati mtihani wa Kiswahili ulipokuwa ukifanyika, msimamizi wa Shule ya Msingi Nambarapi, Adam Komba kutoka Halmashauri ya Tunduma mkoani Ruvuma, alitayarisha majibu akiwa ndani ya chumba cha mtihani na kuwaonyesha watahiniwa.

"Baada ya kuwaonyesha, aliyatuma majibu hayo kwa simu kwenda kwa Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Michiga, iliyoko Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu mkoani Mtwara, Edson Thabiti, ili ampatie mtahiniwa ambaye ni ndugu yake,' alisema.

Kwa mujibu wa katibu huyo,Thabiti na msimamizi ambaye ni Mwalimu Mohamed Ding'ombe, walikiri kupokea majibu hayo na kuwapatia watahiniwa.

Alisema katika mkoa wa Singida na Halmashauri ya Iramba, ilibainika wanafunzi wa shule ya Ntwike kuwa walipewa majibu kwa msaada wa Mwalimu Mkuu, Agapito Mlwilo na Mwalimu Pascal Balohho na Celina Kime wakishirikiana na wasimamizi wanne.

Dk. Msonde aliwataja wasimamizi hao kuwa ni Lucyrace Temu, Anna Mpamila, Joyce Kitundu na Neema Ng'adi.

"Mwalimu Mkuu wa Ntwike alimtumia pia majibu Mwalimu Mkuu, Ibrahim Mulula wa Shule ya Msingi Sekenke wa Halmashauri ya Iramba. Mulula alipoyapokea, alimpa mlinzi ambaye ni ndugu wa Lazaro Msengi na kwa kushirikiana na msimamizi wa shule, Brendan Kimu, Fatma Mohamed, Zuhura Mfinanga na Selima Rahimu wakawapa watahiniwa," alisema.

Katika Mkoa wa Tabora na Halmashauri ya Nzega, alisema walibaini mwalimu Christopher Mboga alishirikiana na wasimamizi Gasper Mushina na Amri Tawakal kuandaa majibu na kuwapa watahiniwa wa shule ya Mboga (Nzega).

Alisema majibu hayo yalitumwa

INAENDELEA UK.8



Mtuhumiwa Taqabal Mwasha akiwa chini ya ulinzi wa askari Polisi kabla ya kusomewa shtaka la kukutwa na mirungi kilo 214, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Lissu asisitiza kugombea urais, aahidi kurejesha Katiba Mpya

**Na Enock Charles**

MWANASHERIA wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Tundu Lissu, amesisitiza nia yake ya kugombea urais, iwapo atapata wito kutoka kwa wananchi na chama chake kugombea nafasi hiyo.

Akizungumza na VoA nchini Marekani, alisema; "Nimeshatangaza utayari wangu wa kugombea nafasi hiyo nikiteuliwa na chama changu na ninarudia tena nikipata wito wa kugombea urais nitapokea wito huo."

Lissu ambaye yupo nje ya nchi tangu Septemba 7, mwaka juzi kwa ajili ya matibabu baada ya kushambuliwa kwa risasi, alisema hayo licha ya hivi karibuni kunukuliwa na vyombo mbalimbali vya habari nchini akieleza kuwa hatarejea nchini hadi hapo chama chake kitakapo mhakikishia usalama wake.

Akieleza kuhusu malengo yake iwapo atafanikiwa kuteuliwa na chama chake kugombea urais, Lissu alisema atarejea upya mchakato wa kutengeneza Katiba Mpya ya wananchi ili kuwapatia wananchi Katiba bora.

Kauli hiyo ya Lissu kuhusu kugombea nafasi ya urais amekuwa akiirudia mara kwa mara, licha ya kuugua kwake na hivi karibuni kudai kuwa hatarejea nchini.

Lissu ambaye amekuwa mbunge kwa vipindi viwili, alivuliwa ubunge wake kutokana na sababu iliyotolewa na Spika wa Bunge, Job Ndugai za utoro bungeni na pia kutokujaza fomu za maadili ya watumishi wa umma, ambazo hutakiwa kujazwa pia na wabunge wote.

Lissu alifungua kesi katika Mahakama Kuu ya Tanzania kudai ubunge wake kwa kile alichodai Spika kukiuka taratibu za uamuzi wa kumvua ubunge, hata hivyo, alishindwa katika kesi hiyo.

# Mafuriko yaua wanafunzi tisa wa shule msingi tatu

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

WANAFUNZI tisa wa shule tatu, ni miongoni mwa watu 13 waliokufa kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Morogoro.

Jeshi la Polisi limeeleza kwamba wanafunzi waliokufa ni wa umri wa kati ya miaka tisa hadi 15.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Wilibrod Mutafungwa, alisema miongoni mwa waliofariki dunia ni wanafunzi watano wa Shule ya Msingi Nyachiro, waliokufa maji baada ya kuzama katika mto Mvuha Kata Kibogwa Tarafa ya Matombo katika Wilaya ya Morogoro.

Alisema tukio hilo lilitokea Jumamosi saa 10.30 jioni katika Kijiji cha Nyachiro, na kuwataja waliokufa ni Neema Rajabu (10), Latifa Khalid (9) ambao ni wanafunzi wa darasa la pili, Munila Khalid (11) wa darasa tatu na Omary Khalid (14) ambao miili yao imepatikana.

Mwingine aliyekufa ni Zanisha Adam (9) wa darasa la pili ambaye mwili wake haujapatikana, kazi ya kuusaka mwili huo inaendelea kwa kushirikisha Polisi na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

Mutafungwa alibainisha kuwa Said Rajabu (11) mwanafunzi wa darasa la tatu aliyekuwa na wenzie waliokufa alinusurika na kujeruhiwa baada ya kuona maji yakizidi, alikimbia na baadaye alianguka na anaendelea na matibabu katika zahanati ya Kibogwa.

Wengine waliokufa ni wanafunzi wawili wa Shule ya Msingi Kibwaya Tarafa ya Mkuyuni, Rajabu Issa (11) na Shabani Msimbe (15), baada ya kutumbukia kwenye dimbwi la maji walipokuwa wakiogelea.

Wanafunzi hao walifariki dunia Ijumaa saa 8.00 mchana katika Kitongoji cha Kisemo, Kijiji cha Kibwaya Tarafa ya Mkuyuni, na kwamba maji hayo yalitokana na mvua zinazoendelea.

Wanafunzi wengine wawili waliokufa maji ni Karim Athuman (13) na Hussein Hassan (14) wa Shule ya Msingi Ulundo waliozidiwa na maji wakiwa wanaogelea mto Ngerengere.

Alisema alisema tukio hilo lilitokea Oktoba 5 mwaka huu saa 6.00 mchana Kitongoji cha Ulundo, Kijiji cha Mtego wa Simba Kata ya Mikese Wilaya ya Morogoro.

Tukio jingine lilitokea Jumamosi saa 12 asubuhi atika bwawa la Mindu Manispaa ya Morogoro, ambapo mvuvi, Jabiru Chris (40) mkazi wa Manzese alifariki dunia baada ya kutumbukia kwenye bwawa hilo akiwa katika shughuli za uvuvi.

Inadaiwa chanzo cha kifo hicho ni mtumbwi aliokuwa akitumia kupoteza mwelekeo na kuzama.

Kamanda Mutafungwa akasema tukio jingine lililotokea Oktoba 6 majira ya asubuhi huko Kipera, Kata ya Tungi Manispaa ya Morogoro ambapo Yasin Ally (50), alifariki dunia baada ya kutumbukia kwenye dimbwi la maji alilokuwa akiogelea.

Katika hatua nyingine, Mutafungwa alisema watu wawili Ramadhani Mkuku na Frank Daud walifariki dunia katika kiwanda cha sukari cha Kilombero K2, baada ya kutumbukia katika bwawa la kuhifadhia uchafu wa utokanao na miwa. Tukio hilo lilitokea Jumapili.


OFISI YA RAIS,
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
MKOA WA MTWARA

KONGAMANO LA UWEKEZAJI NA
MAONESHO YA BIASHARA MTWARA 2019



MGENI RASMI: WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAREHE: 31 OKTOBA – 3 NOVEMBA 2019 | MAHALI: UWANJA WA CHUO CHA UALIMU MTWARA

Kongamano la Uwekezaji na Maonesho ya Biashara Mtwara 2019 litahusisha uzinduzi wa Mwongozo wa Uwekezaji Mtwara na kuwa jukwaa la kuonesha fursa za uwekezaji; ambazo bado hazijatumika kwenye Mkoa kwa watu binafsi, makampuni na taasisi mbalimbali ndani na nje ya nchi. Kongamano hili litabebwa na kaulimbiu:

"Wekeza Mtwara kwa Matokeo Makubwa: Kinara wa Uchumi wa Gesi na Korosho Tanzania"
Pamoja na mambo mengine, Kongamano hilo litatoa fursa za:

- *Kufanya mawasilisho, mada na hotuba;*
- *Kupata ushuhuda kutoka kwa wawekezaji;*
- *Majadiliano ya uwili, Kampuni na Kampuni; na Serikali na Kampuni;*
- *Kuona fursa mbalimbali za uwekezaji;*
- *Kushiriki katika Usiku wa Mtwara; na*
- *Kuona fursa kubwa ya kuwekeza kwenye ufukwe wa Msangamkuu.*

Karibuni wote mshiriki na kushuhudia fursa nyingi za uwekezaji kwenye Mkoa wa Uchumi wa Gesi na Korosho Tanzania.

*Wahi Nafasi yako sasa*

MTWARA Investments Forum & Expro

Kwa taarifa zaidi tafadhali wasiliana nasi kupitia:
Simu: HOTLINE: 0677 300 500 /0754 088 461 / 0783 955 555
Barua Pepe: info@mtwarainvestmentforum.or.tz
investmentforum@mtwara.go.tz
Tovuti: www.mtwarainvestmentforum.or.tz
@mtwarainvestors @mtwarainvestors

215461002




Mkurugenzi wa Shirikisho la Wenye Viwanda Nchini (CTI), Leodgar Tenga (kulia), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu hafla ya utoaji tuzo ya Rais ya mzalishaji bora 2019, itakayofanyika kesho. Kushoto ni Ofisa wa CTI, Neema Mhondo na Ofisa Masoko wa Kampuni ya ALAF, Theresia Mmassy. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Magufuli amwombea msamaha Nape jimboni

**Na Elizabeth Zaya**

RAIS John Magufuli amemwombea msamaha kwa wananchi wake, Mbunge wa Mtama, Nape Nnauye, huku akieleza ameshamsamehe, hivyo wanapaswa kumpa ushirikiano.

Rais Magufuli alimwombea msamaha huo aliposimama katikia kijiji cha Mtama, kusalimia wananchi akiwa njiani kuelekea wilayani Ruangwa mkoani Lindi katika ziara ya kikazi.

Alisema Nape ni kijana mzuri na mchapa kazi licha ya kwamba alifanya makosa kidogo na kwamba alishamsamehe kabisa.

"Nashukuru kwa kumchagua kijana wangu Nape, ni kijana mzuri na amechangamka. Ni mchapakazi alifanya vimakosa vidogo vidogo, lakini mimi nimeshamsamehe moja kwa moja," alisema Rais Magufuli na kuongeza:

"Nataka niseme kwa dhati ya moyo wangu, naomba mtoe ushirikiano kwake, ni kijana mzuri na mimi nampenda, yaliyopita si ndwele, tugange yajayo, Nape hoyeeee."

Baada ya kumaliza kumwombea msamaha Nape na kueleza hayo, Rais Magufuli aliwaambia wananchi kwamba anaamini yapo mengi yaliyofanyika katika Jimbo la Mtama na kumpatia nafasi mbunge huyo kuyaelezea.

Akizungumzia ambayo yamefanyika katika jimbo lake, Nape alisema kati ya majimbo ambayo yamepewa kipaumbele na serikali ya awamu ya tano ni pamoja na jimboni kwake.

Nape alitaja baadhi ya maeneo ambayo yamepewa kipaumbele katika jimbo hilo tangu kuingia kwa serikali hiyo kuingia madarakani ni pamoja na sekta ya afya, umeme na miundombinu.

"Nakushukuru sana Rais kwa yale yote ambayo serikali yako imetufanyika katika Jimbo la Mtama, tumehemewa na upendeleo ambao unatupatia," alisema na kuongeza:

Wakati unaomba kura katika jimbo hili tulikuwa na asilimia 11 tu ya umeme, lakini mpaka sasa ninavyoongea tumefikia asilimia 86, huu ni upendeleo mkubwa sana, tunakushukuru sana," alisema Nape.

Aliongeza: "Katika sekta ya afya umetupatia zaidi ya Sh. bilioni 2.8 kwa ajili ya hospitali ya wilaya na vituo vingine vya afya katika jimbo hili. Lakini pia tangu waletwe hawa watu wa Tarura, barabara zetu nyingi kwenda vijijini zimetengenezwa."

Mbali na hilo, Rais Magufuli aliagiza Ofisi-Tamisemi, kupeleka makao makuu ya Halmashauri ya Lindi vijijini kupelekwa Mtama na kuitwa Halmashauri ya Mtama.

Wakati huo hio, Rais Magufuli ameiagiza Wizara ya Fedha na Mipango kutoa Sh. milioni 620 leo kwa ajili ya kutumika kumalizia ujenzi wa ghala la kuhifadhia mazao mbalimbali wiyalani Ruangwa mkoani Lindi.

Rais Magufuli alitoa agizo hilo jana alipotembelea ghala hilo kujionea maendeleo ya ujenzi wake.

Alipotembea katika ghala hilo hakuridhishwa na namna ujenzi huo unavyokwenda na hivyo kuhoji sababu za kusuasua kwake.

Hata hivyo, baada ya kujibiwa kwamba kinachokwamishwa ni ukosefu wa fedha ambazo wameomba Wizara ya Fedha, alitumia simu yake ya mkononi kupiga katika wizara hiyo na kuagiza fedha hizo kufikia leo ziwe zimepelekwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi huo.

Rais Magufuli pia alizindua barabara ya Naganga hadi Ruangwa yenye urefu wa kilomita tano kwa kiwango cha lami.




# Hakimu atoa neno kesi vigogo Chadema

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imetoa siku moja kwa mawakili wa pande zote mbili katika kesi inayowakabili vigogo wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kujadiliana kisheria na kuwasilisha hoja zao ili waanza kujitetea.

Vigogo hao tisa wanaokabiliwa na kesi ya uchochezi, akiwamo Mwenyekiti Taifa, Freeman Mbowe, wanashtakiwa kwa mashtaka 13 ya uchochezi.

Jana, wakili wa utetezi alidai mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, anayesikiliza kesi hiyo kwamba kesi imepangwa kusikikiza ushahidi wa utetezi na walikuwa na shahidi mmoja.

Hata hivyo, Wakili wa Serikali Mkuu Faraja Nchimbi, alipinga shahidi wa nje kusikilizwa ushahidi wake kabla washtakiwa hawajajitetea kwa sababu utaratibu huo unakinzana kisheria.

"Mheshimiwa Hakimu kuna changamoto kubwa mahakama yako kuanza kuwasikiliza mashahidi wa nje kabla washtakiwa hawajajitetea. Utaratibu huo unakinzana na sheria upande wa Jamhuri unaupinga," alidai Nchimbi.

Hakimu Simba aliamuru pande zote mbili zikapitie na kusoma sheria ili wawasilishe hoja za pingamizi hilo la awali na majibu.

Alisema kesi hiyo itaendelea kesho mahakamani hapo kusikiliza hoja za kisheria za mawakili.

Mbali ya Mbowe, washtakiwa wengine ni Katibu Mkuu Dk. Vicent Mashinji; Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko; Mbunge wa Bunda Mjini, Ester Bulaya, Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, Salum Mwalimu; Mbunge wa Kibamba, John Mnyika; Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche; Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa; na Mbunge wa Kawe, Halima Mdee.

Washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka 13 likiwamo la kula njama wakiwadaiwa kuwa Februari 1 na 16, mwaka jana, jijini Dar es Salaam, waliku a njama ya kutenda kosa la kufanya mkusanyiko usio halali na kukiuka tamko la kutawanyika.

# Kesi vigogo NSSF yapigwa tena kalenda

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imepiga kalenda kesi inayowakabili vigogo tisa wa Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF), akiwamo Kaimu Mkurugenzi wa Fedha, Jamila Vulu, na wenzake wa Idara ya Fedha mpaka Oktoba 28, mwaka huu itakapotajwa tena.

Kesi hiyo ya uhujumu uchumi ikiwamo kughushi, wizi na kutakatisha zaidi ya Sh. bilioni mbili, ilipangwa jana kwa ajili ya kutajwa lakini upande wa Jamhuri ulidai kuwa upelelezi haujakamilika.

Jana, mahakama hiyo chini ya Hakimu Mkazi Vick Mwaikambo, ilikubali ombi la Jamhuri la kupanga tarehe nyingine ya kutajwa kutokana na madai ya kutokamilika kwa upelelezi. Awali, kesi hiyo ilipangwa mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Kelvin Mhina, lakini kwa kuwa amepata udhuru wa kikazi, ilitajwa mbele ya Hakimu Mwaikambo.

Wakili wa Serikali Gloria Mwenda, alidai kuwa kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa lakini upelelezi haujakamilika, hivyo kuomba tarehe nyingine ya kutajwa. Hakimu Mwaikambo alisema kesi hiyo itatajwa tena Oktoba 28, mwaka huu na washtakiwa wataendelea kukaa mahabusu. Mapema mahakamani hapo, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, aliwataja washtakiwa kwamba mbali na Vullu kuwa ni Mwandishi wa Hundi Abdul Njozi, Meneja Uhakiki Amir Kapera, Mhasibu James Oigo, Mhasibu Mkuu Hellen Peter na Mhasibu Mwandamizi anayeshughulikia matumizi, Ivonne Kimaro.

Wengine ni Kaimu Meneja Rasilimali Watu, Tikyeba Alphonce na Mhasibu Dominic Mbwete.

Wankyo alidai katika shtaka la kwanza kwamba washtakiwa wote wanadaiwa kati ya Julai Mosi, 2016 na Septemba 4, 2017 walikula njama ya kutenda makosa ya kughushi na kutakatisha fedha.

Shtaka la pili, mshtakiwa Njozi na Akiri wanadaiwa katika kipindi hicho, wakiwa watumishi wa umma, kwenye ofisi za makao makuu ya NSSF, walighushi hundi 47 za Benki ya CRDB kwa akaunti namba 01J1028249500 yenye jina la NSSF zenye jumla ya Sh. 2,130,211,437.35.



Meneja wa Tigo Kanda ya Kaskazini, Lilian Mwalongo, akijaribu kuwasha gari wakati wa uzinduzi wa promosheni ya Tigo Fiesta 2019 Chemsha Bongo, katika viwanja vya Nyerere Square, jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Nyerere aenziwa elimu ya uzalendo

**Na Mwandishi Wetu**

MAKUMBUSHO ya Taifa imetoa elimu ya uzalendo kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari kama sehemu ya kumuenzi Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika kumbukizi ya miaka 20 ya kifo chake.

Katika programu hiyo iliyofanyika Makumbusho ya Taifa jijini Dar es Salaam jana, wanafunzi, walimu, wananchi na wasanii waliojumuika pamoja walipewa elimu ya uzalendo na misingi muhimu aliyoisimamia Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika uhai wake.

Pamoja na mambo mengine wanafunzi walifundishwa misingi ambayo Mwalimu Nyerere alisimamia ikiwa ni pamoja na utu, haki, amani, usawa, na uzalendo.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Makumbusho ya Taifa, Dk. Gwakisa Kamatula, aliwataka wanafunzi na wananchi waliojitokeza kushiriki katika programu hiyo ya kumuenzi Mwalimu kufuata misingi aliyosimamia kwa matendo.

Alisema programu hiyo maalumu kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari ina lenga kuwafundisha watoto matendo ya kizalendo kwa nchi yao ya Tanzania kama namna pekee ya kumuenzi Nyerere ambaye kwa maneno na matendo yake alionyesha uzalendo kwa nchi yake na Afrika kwa ujumla. Mratibu wa programu hiyo, Anamery Bagenyi, alisema kuwa programu hiyo ijulikanayo kama Wajuu wa Mwalimu zinaendelea kutolewa na Makumbusho na Nyumba ya Utamaduni kupitia Kitengo cha Elimu.

Bagenyi ambaye ni Ofisa Elimu Mwandamizi wa Makumbusho ya Taifa na Nyumba ya Utamaduni, alisema programu hiyo imekutanisha wanafunzi na walimu kutoka shule za msingi za Olympio, Bunge, Mzinga B, Mwenge na Shule ya Mwalimu Nyerere iliyoko Mbezi Beach.

Vilevile programu iliwaleta pamoja wanafunzi na walimu kutoka shule za sekondari za Baobao iliyoko Wilaya ya Bagamoyo na Mikwambe Wilaya ya Temeke na wasanii kutoka kikundi cha Mjomba. Msanii Mrisho Mpoto aliwaeleza wanafunzi kuwa Mwalimu Nyerere alisimamia misingi ya haki, amani, usawa na uzalendo ambao nao wanatakiwa kufuata na kutenda.

Wanafunzi wamefundishwa kuipenda nchi yao na kuwaandaa kuwa wananchi wa kutegemewa katika kuijenga nchi yao na Afrika.

Jumla ya wanafunzi 500 pamoja na walimu wao walihudhuria programu hiyo.

# Shule 30 kikaangoni matumizi mabaya ya fedha za umma

**Na Happy Severine,** BARIADI

TAASISI ya Kupambana na Kuzuia Rushwa (Takukuru) mkoani Simiyu katika kipindi cha Julai hadi Septemba, mwaka huu, imefanya ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za umma katika shule 30 mkoani hapa. Lengo la ufuatiliaji huo ni kuona kama kuna ufujaji, ukiukwaji wa sheria, taratibu na miongozo ya fedha hizo inayotolewa na serikali.

Mkuu wa Takukuru mkoani hapa, Joshua Msuya, alisema uchunguzi huo pia ulikuwa na lengo la kuona kuna uvujaji, ushirikishwaji wa jamii na kuona thamani ya fedha iliyotekelezwa kama inalingana na miradi husika.

Alisema katika ufutaliaji huo, wamebaini kuwa baadhi ya uongozi wa shule umeundwa kusimamia mipango ya matumizi ya fedha hizo na kusababisha ucheleweshaji wa upatikanaji wa huduma iliyokusudiwa. "Tulibaini kuwapo kwa ukiukwaji wa miongozo ya matumizi ya fedha za umma iliyotolewa na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) kwa shule zote za msingi tulizozifikia. Baada ya kubaini hivyo, tulishauri miongozo ifuatwe pamoja na sheria ya ununuzi wa umma," alisema Msuya.

Shule zilizofikiwa na uchunguzi huo 10 za Wilaya ya Meatu, 10 Maswa na zingine ni za Wilaya ya Bariadi. Katika hatua nyingine, Takukuru mkoani hapa inawachunguza watumishi wanne wa wilaya ya Busega waliohusika na upotevu au ubadhirifu wa Sh. milioni 55 ambazo zilipaswa kutumika kwenye shughuli ya urasmishaji makazi kwenye kata za Lamadi, Mkula, Kiloleli, Mwamanyili na Kabita. Pia taasisi hiyo imeokoa Sh. 8,686,000 ambazo kati ya hizo, Sh. 7,321,000 zimeokolewa kupitia udhibiti wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri ya Wilaya ya Meatu na Sh. 1,365,000 kupitia uchunguzi wa malipo ya safari hewa kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi.

Msuya aliongeza kuwa katika kipindi hicho, kesi mpya mbili zimefunguliwa katika Mahakama ya Wilaya ya Maswa Mubarak Ally ambaye ni Mhandisi wa Maji wilaya hiyo na Octavian Mishana ambaye ni ofisa ardhi wilaya hiyo.


DRC DANISH REFUGEE COUNCIL

**TANGAZO LA ZABUNI**

SHIRIKA LA KUHUDUMIA WAKIMBIZI LA DANISHI LINATARAJIA KUNUNUA T-SHIRTS.

KWAHIYO SHIRIKA LA DANISHI LILILOPO KIBONDO LINAWAARIKA WAZABUNI KULETA BEI ZAO.

NYARAKA ZA KUJAZIA BEI ZINAPATIKANA KATIKA OFISI ZA DANISHI KIBONDO KUANZIA TAREHE 15.10.2019 HADI TAREHE 28.10.2019 SIKU ZA KAZI SAA 2:00 ASUBUHI MPAKA SAA 10:30 JIONI. TUNAPATIKANA BARABARA YA IRC KIBONDO.

KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA +255627423991
au barua pepe jean.kabore@drc.ngo

ZABUNI ZITAFUNGULIWA HADHARANI TAREHE 30.10.2019 SAA 4:00 ASUBUHI OFISI ZA DANISHI KIBONDO NA KAMATI YA KUFUNGUA ZABUNI LA DANISHI.

UNAWEZA KURUDISHA ZABUNI KUPITIA rfq.tza@drc.ngo AU KULETA MOJAKWA MOJA OFISINI VINGINEVYO NI BATILI.

215457702

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Siku zilizoongezwa zitumieni kujisajili

**SERIKALI** imeongeza siku tatu zaidi kwa ajili ya wananchi kujiandikisha ili waweze kupiga kura kuchagua viongozi wa vijiji, vitongoji, mitaa pamoja na wajumbe wengine.

Hii inamaanisha kuwa kesho ni mwisho wa kujisajili.

Tunaipongeza serikali kwa kuona hitaji na umuhimu wa kuwaongezea muda ili kila mmoja ajiandikishe na kutumia haki yake kikatiba ya kuchagua viongozi wa serikali za mitaa, vitongoji na vijiji wanaofaa. Tunaungana na viongozi kuwahamasisha wananchi kujiandikisha kwa sababu ili waweze kupiga kura na kumchagua mwenyekiti wa kijiji, kitongoji, mtaa na wajumbe wa serikali wanapaswa kujiandikisha kwanza kwani ndivyo matakwa na maelekezo ya kisheria.

Na sasa kwa wale ambao hawajajiandikisha ndiyo wakati wa kufanya hivyo ili kuweka madarakani viongozi watakaotuhudumia bila kutaka rushwa, kutunyanyasa na pia ni wakati wa kuwaondoa kwenye uongozi wale ambao ni wazembe na wababaishaji na wasiowajibika.

Tunaungana na serikali kuwahimiza wananchi kujiandikisha ili kuchagua viongozi bora ambao watazishughulikia na kuzitatua kero za Watanzania katika ngazi za mwanzo ikiwamo waliosababisha migogoro.

Tunawashauri wananchi wajitokeze na kujiandikisha kwa wingi ili kuwachagua viongozi wa serikali za mitaa ambao watawaongoza kwenye masuala mbalimbali kama kuwapa utambulisho wa awali wakati wanafuatilia taarifa za kufungua akaunti benki. Aidha, watakuwa wa kwanza kwenye kuwasaidia kwenye migogoro ya ardhi, kutatua matatizo ya kifamilia na usuluhishi kabla ya kwenda mahakamani.

Aidha, ni suala muhimu kushiriki wakifahamu kuwa hawa ndiyo watakaowaongoza kwa miaka mitano.

Tunaona kuwa kuna haja ya kuwachagua viongozi hawa kwani ndiyo wanaowajibika kufuatilia utekelezaji na uendelezaji wa mipango bora ya maisha ya wananchi katika jamii zetu. Hawa ndiyo wanaosimamia na kushirikiana na wananchi kuleta mabadiliko chanya kwenye uzalishaji iwe kilimo, ufugaji, uvuvi na shughuli nyingine za maendeleo kwenye hatua za mwanzo. Tukumbuke, kazi kubwa ya viongozi hawa ni kusimamia na kuendeleza ustawi wa jamii, kuhakikisha uwepo wa amani, utulivu, ulinzi, kuheshimiana na yote hayo ili kuwe na jamii zilizo bora. Kuchagua viongozi hawa ni muhimu kwani ndiyo wa kwanza kushughulikia matatizo ya wananchi katika hatua za mwanzo kwa ajili ya kutoa majawabu na ufumbuzi wa changamoto zao katika hatua za mwanzo.

Tukumbuke tunahitaji kuwa na viongozi hawa kwani ndiyo wa kwanza kujenga uhusiano wa uaminifu baina ya jamii na viongozi wao au wa serikali kuu.

Ikumbukwe kuwa iwapo watu hawatachagua viongozi bora, wakapuuza uchaguzi na wakawaachia wachache wakachagua wale wanaowapenda kwa maslahi yao, inaweza kusababisha wababaishaji hao kuingia madarakani, utakuwa mwanzo wa kusababisha kufarakana baina ya watu na serikali.

Hii ni kutokana na ukweli kuwa taswira ya serikali inaweza kuchafuliwa na viongozi wabovu na wasiowajibika wanaowachosha badala ya kuwahudumia wananchi.

Ndiyo maana tunaihamasisha jamii kufahamu kuwa kuchagua viongozi bora utakuwa ndiyo mwanzo wa kufahamu na kufuatilia masuala mbalimbali ya maendeleo yatakayoisaidia jamii katika kupata uelewa wa masuala muhimu ya maendeleo. Wananchi tujitokeze kuchagua viongozi kwani hawa ndiyo wanaotuhamasisha kufahamu na kushiriki masuala mbalimbali ya maendeleo kwa kutumia taratibu, sheria na mifumo mbalimbali tuliyojiwekea. Kwa msingi huo, tunawakumbusha wananchi kuwa kupiga kura lisiwe suala la hiari bali matakwa na maelekezo ya kikatiba.

Hivyo shime tutumie muda tuliongezewa kujiandikisha ili kupata viongozi bora na watakaotuhudumia kwenye ngazi za mitaa, vijiji na vitongoji. Tusipuuze wajibu wa kujichagulia viongozi tushiriki na tuhakikishe kuwa tunawachagua walio bora kwa ajili ya maendeleo yetu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Elimu sasa ijielekeze zaidi kujitegemea

Na Sabato Kasika

**JUZI** Oktoba 14 ilikuwa ni kumbukumbu ya miaka 20 ya kifo cha Baba wa Taifa, Hayati, Julius Kambarage Nyerere aliyefariki dunia Oktoba 14 mwaka 1999, katika Hospitali ya Mtakatifu Thomas, jijini London, Uingereza.

Katika maadhimisho ya kumbukumbu ya kifo chake, watu wa kada mbalimbali wamemzungumzia kwa mapana na marefu Rais huyu wa kwanza wa Tanzania, kuhusu yale aliyofanya kwa ajili ya maendeleo ya taifa hili.

Binafsi ninaweza kusema kuwa kila elimu ya Tanzania inapozungumzwa siyo rahisi kumuweka pembeni Baba wa Taifa, kutokana na ukweli kwamba siku zote alitamani kila Mtanzania apate elimu.

Kumbukumbu zinaonyesha kuwa Baba wa Taifa alianza hilo mara tu baada ya nchi hii kupata uhuru, pale alipotangaza vita dhidi ya maadui watatu, maradhi, ujinga na umaskini.

Aliamini kwamba maadui wawili kati ya hao watatu, ambao ni umaskini na maradhi hawawezi kuondoka iwapo Watanzania hawatapata elimu.

Hivyo alifanya kila njia ili kuhakikisha kila Mtanzania anapata elimu bila kujali kama ni tajiri au maskini ili mradi tu awe ni raia mwenye akili timamu.

Kulikuwa na Azimio la Musoma la mwaka 1974 kuhusu watoto wote wenye umri wa kwenda shule wapelekwe huko ili wakapate elimu. Hii pia inaonyesha ni jinsi gani alitaka Watanzania wapate huduma hiyo muhimu kwa maendeleo ya taifa na dunia kwa ujumla.

Hata watu wazima, ambao hawakubahatika kupata elimu rasmi, hawakuachwa nyuma, walikuwa na madarasa yao kila siku jioni baada ya kutoka kwenye shughuli za uzalishaji mali.

Jambo la kufurahisha ni kwamba elimu ilitolewa bure, hali ambayo kwa kweli wale ambao hawakuwa na matumaini ya kuipata kutokana na hali duni ya maisha, waliweza kuipata hadi ngazi ya chuo kikuu.

Baba wa Taifa alijikita zaidi kwenye elimu ya kujitegemea ili kuwajenga vijana kujifunza zaidi kazi za uzalishaji shuleni, na kuziwezesha shule zijitegemee kutokana na uzalishaji huo.

Muungwana anaamini kwamba juhudi za Baba wa Taifa za kutaka kila mtoto wa Kitanzania apate elimu zimerithiwa na serikali ya awamu ya tano, ambayo nayo imejikita katika hilo kwa kuruhusu watoto kusoma bure.

Serikali kuamua kubeba mzigo wa kulipa gharama zote kwa elimu ya msingi na sekondari kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne ni kuonyesha kwamba imedhamiria kuhakikisha kila mtoto wa Kitanzania anapata elimu.

Hatua hii ni wazi kwamba Baba wa Taifa anaenziwa kwa vitendo katika juhudi zake za kutaka Watanzania wote wanaelimika bila kuangalia uwezo wa mtu kifedha, bali wote kwake walikuwa sawa.

Muungwana anaipongeza serikali ya awamu ya tano kwa ubunifu na weledi katika utendaji wake, lakini jambo la msingi zaidi ni kwamba ungefanywa mkakati ili elimu ijikite zaidi kwenye kujitegemea.

Mbali na kujitegemea, kazi hizo ziliwawezesha wanafunzi kujengwa kwa namna ambayo iliwapevusha fikra zao, na hivyo kuleta mtizamo chanya na mabadiliko ya kweli katika jamii kufuatana na ujuzi walioupata.

Hivyo juhudi za sasa za kutoa elimu bure pia zizingatie kuwajenga vijana wa Tanzania katika misingi ambayo iliachwa na Baba wa Taifa ambayo ni elimu ya kujitegemea, watoto waelimishwe kuwa raia wa wema na wenye uzalendo.

Kwani nje ya wanafunzi kupewa elimu ya darasani, vilevile walipewa elimu ya stadi za maisha. Dhana hii ya Baba wa taifa aliyoiasisi juu ya elimu ya kujitegemea iliondoa mapungufu mengi yaliyokuwepo kwenye elimu ya mkoloni ambayo iliegemea zaidi katika jamii ya kibepari iliyooandaa watu kutawaliwa na si kujitawala.

Kimsingi unapozungumzia dhana ya elimu bure kuanzia elimu ya msingi mpaka kidato cha nne kwa sasa, hauwezi kuitenganisha na sera ya serikali juu ya elimu bure na pia Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM).

## BARUA MJADALA

### *Wakazi Kilimanjaro tabia hii haikubaliki*

**Mhariri,**

*NIMEJITOKEZA leo kwenye nafasi hii inayotupa fursa wananchi pamoja na mambo mengine ya kueleza kero na changamoto mbalimbali zinazotukabili kwenye maeneo yetu, katika dhima nzima ya kusukuma gurudumu la maendeleo mbele.*

*Kwa fursa hii, ninapenda kuzungumzia hatua isiyo ya kiungwana au kistaarabu inayofanywa na baadhi yetu sisi wazaliwa wa mkoa wa Kilimanjaro ambayo hata katika misahafu kwa wanaoamini haikubaliki.*

*Tayari watoto wetu, ambao ni wanafunzi waliokuwa wanasoma shule za misingi wamemaliza mitihani yao ya kitaifa katika ngazi hiyo ya elimu, na kwa hali hiyo kwa sasa wako majumbani wakisubiri matokeo yao kwa ajili ya kujiunga na masomo ya sekondari.*

*Sasa wakati wa kipindi hiki wanachosubiri majibu, kuna utamaduni wa wakazi wa mkoa wa Kilimanjaro na hasa sisi Wachaga ya kuchukua watoto hao ili waje watufanyie kazi zetu na hasa zile za kusimamia biashara mbalimbali kwa maana ya kuuza.*

*Kimbembe huwa kinatokea wakati majibu ya mtihani huo yanapokuwa yametoka na kijana akawa amefaulu na kwa hali hiyo akahitajika sasa arudi nyumbani kwao tayari kwa ajili ya maandalizi ya kujiunga na kidato cha kwanza kwa masomo ya sekondari.*

*Mara nyingi 'matajiri wao' ama wenye biashara ambao wanakuwa wamewachukua watoto hao huwa wakati mwingine hawako tayari kuwaachia, wakitaka waendelee kuwauzia biashara zao.*

*Ndipo visa vya kwamba kuna mapungufu ya fedha kutoka kwenye biashara zao ama kuna mapungufu ya mitaji yaliyojitokeza baada ya kijana huyo kuwa ameanza kuisimamia biashara husika kabla hajaja.*

*Ndipo unakuta kijana wa watu anafanyiwa visa vya hapa na pale kwa lengo la kumkwamisha asiende kuendelea na masomo yake au hata kama anaondoka basi asiweze kulipwa haki yake ya mshahara aliyokuwa akiidai.*

*Ninatoa wito kwetu sisi wakazi wa mkoa wa Kilimanjaro na hasa sisi Wachaga tumuogope Mungu, kwa maana tuachane na aina hii ya dhuluma ambayo baadhi ya wenzetu wamekuwa wakiifanya kwa muda mrefu sasa.*

*Ieleweke kuwa vijana hao huruhusiwa na wazazi ama walezi wao ili waje wajitafutie kipato cha kuwawezesha kujikimu katika kipindi wanachosubiri matokeo yao na tusitumie mwanya huo kuwadhulumu watoto hawa.*

**Deogratius Massawe-Rombo**

**WASILIANA NASI:**

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**



Baadhi ya viongozi wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki (EAC) katika picha ya pamoja hivi karibuni wakiongozwa na kiongozi wao, Rais John Magufuli (watano kutoka kushoto). **PICHA: MTANDAO**

# Bila ushirikiano sasa Afrika inajiua yenyewe

**Na Mwandishi Wetu**

BIASHARA miongoni mwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, (EAC), inatetereka na mambo si mazuri.

Ni masuala yanayoibuka kwenye mkutano wa Bunge la Afrika Mashariki (EALA), wakati wa kujadili ripoti ya Kamati ya Biashara na Uwekezaji ya EAC ya mwaka 2016.

Hapo inaelezwa kuwa thamani ya biashara miongoni mwa nchi wanachama kwa mwaka huo, ilishuka kutoka dola bilioni 3.2 mwaka 2015 hadi kufikia dola bilioni 2.6.

Moja ya sababu zinazotajwa kuchangia kushuka kwa biashara katika ripoti hiyo ni pamoja na kuendelea kuwapo kwa vikwazo visivyo vya kodi au none tariff barriers (NTBs).

Aidha, kukosekana kwa mifumo inayodhibiti ufanyaji biashara na kingine ni mataifa wanachama kushindwa au kukataa kuridhia mikataba ya biashara baina yao bila sababu yoyote ya msingi.

Jambo hilo si jema kwa afya ya Jumuiya ya Afrika Mashariki inayokusudia kuwa na ushirikiano ili kufikia mtangamano.

Lakini tatizo hilo si kwa EAC pekee huenda ni Afrika nzima.

Masuala yanayohusu ushirikiano yamekuwa magumu kufikiwa kutokana na wanachama kufikiria kibinafsi zaidi.

Wakati mambo yanashindikana kuanzia biashara na maingiliano ya raia wa EAC na hata kwenye Umoja wa Afrika (AU), ni wakati wa kujikumbusha kuwa ili usikike na ushawishi wako kukubalika na wengine ni lazima uwe na nguvu.

Nguvu hizo ni kiburi cha kiuchumi, umahiri wa teknolojia, uwezo wa kijeshi na mamlaka za kisiasa za kushawishi na kuyalazimisha mataifa mengine kukusikia na kukutii.

Ndiyo maana mataifa yenye msuli huo kama Marekani na China ambalo ni taifa la pili kwa uchumi mkubwa duniani yanathamini muungano, umoja na mtangamano.

Si hivyo hata Umoja wa Ulaya (EU) unasimama imara na kulinda muungano wake licha ya kuwapo na sekeseke kama vile Uingereza kujitoa.

Umoja na ushirikiano ndiyo msingi mkubwa wa kuwa imara kiuchumi, kiteknolojia na hata kiushawishi.

Leo hii dunia inazitazama China, Marekani, India na EU kama madola yenye nguvu na ambayo yana ushawishi mkubwa mno (influence).

Amerika inaposimamia jambo leo ni lazima dunia itasikiliza, aidha China inapoinuka kila taifa linasikiliza kufahamu China inasema nini.

Si hivyo tu hata India, Umoja wa Ulaya na pengine mataifa ya Amerika Kusini hasa Mexico.

Afrika isijidanganye kuwa itakuwa inaendeleza ubinafsi wa kila nchi kujifanyia inavyotaka na kukataa mtangamano na ushirikiano.

Kama Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi na Sudan hazitaweza kufanya biashara na kushirikiana zitawezaje kushirikiana na China, India na EU?

Kama inakuwa vigumu kuwa na umoja na ujirani ndani ya Afrika itawezekanaje kuwa na Dola la AU ambalo nalo linatakiwa kusimama kama China au India au EU kwenye kutetea mambo yake iwe kiuchumi au kisiasa?

Inabidi Afrika na pia EAC, kujikumbusha kila wakati kuwa umoja ndiyo silaha pekee ya ushindi.

Kama Marekani ina majimbo 52, Afrika nayo yenye nchi 53 inashindwaje kuwa na mtangamano kama ilivyo Marekani?

Kwanini mataifa ya Afrika yasiungane na kuwa na dola la AU ambalo ndilo litakalokuwa mwanzo wa mafanikio ya kila kitu ikiwa ni pamoja na kuondoa umaskini na uasi wa kisiasa?

Afrika Mashariki inahitaji sana kuungana na kufanya biashara na miradi ya maendeleo pamoja kwa kuunganisha nguvu, kama ilivyo China na India.

Ni wazi kuwa hakuna mafanikio kama Waafrika hawatajiunga na kuamua kufanya mambo kwa ushirika. Baadhi ya wabunge wa EALA wanasema nchi wanachama zimejawa na hofu 'isiyofahamika' ya kuogopa muungano au mtangamano.

Wanaona kuwa kuna woga uliojaa miongoni mwa wanachama wa EAC yenye nchi sita wanachama, kuwa ndio unaochangia kuua jumuiya kwa kuwa unasababisha malengo ya waasisi wa jumuiya kushindwa kufikiwa.

Ni lazima Afrika pamoja na EAC kutekeleza maamuzi wanayojiwekea wenyewe kwa ajili ya manufaa yao na watu wao kwa sababu bila mtangamano hakuna maendeleo. Ni kitu gani kinachosababisha wanachama kuogopana na kushindwa hata kuridhia masuala na mikataba waliyokubaliana wenyewe kwa miongo kadhaa?

Bila kuwa na umoja mambo yataendelea kuwa mabaya kwa Afrika na watu wake watabaki kuwa maskini, wagonjwa, wajinga na walio nyuma kimaendeleo kwa kuwa tu, viongozi wamekataa ushirikiano.

Kwa mfano, kama Tanzania haiwezi kufanya biashara na Uganda, itafanyaje uwekezaji na ushirikiano na mataifa mengine?

Ni lazima kujirekebisha na kuondoa tofauti hizi kwa kuwa China na Afrika na mataifa mengine ya Mashariki ya Mbali kama Indonesia, Malaysia na Korea yalikuwa kwenye kiwango kimoja cha kiuchumi na Afrika miaka ya 1960, lakini hao umoja na ushiriano umewavusha Afrika na EAC zinangoja nini?

Ni wakati wa kutekeleza hayo ambayo viongozi wa Afrika wameyaona na yamethibitisha kuwa umoja ni ushindi na ndiyo mafanikio popote duniani.

**KABWELA** **Na Fadhili Mohammed**



# Mbowe aanika sababu kusuasua uandikishaji

INATOKA UK. 2

George, maarufu kama 'Memorial' Dk. Mghwira alisema: "Manispaa ya Moshi, Mkurugenzi uko hapa, waandikishaji watoke kule waje wawafuate wananchi na waandikishwe wakiwa kwenye eneo lake la kazi.

"Na maeneo mengine, naagiza waandikishaji watoke na kuja kwenye maeneo yenye mwingiliano mkubwa wa watu na kuandikisha. Lakini nawaomba kila mfanyabiashara na hata wanunuzi mjiandikishe, tuko na maofisa ambao nimefuatana nao."

Dk. Mghwira alisisitiza kwamba wanaoandikishwa ni lazima wafahamu kwamba watakwenda kupiga kura katika maeneo yao na si katika soko walilojiandikisha la Memorial.

Akiwa katika eneo hilo, mkuu huyo wa mkoa alitaja maeneo ambayo idadi kubwa hawajajiandikisha kuwa ni Machame, Old Moshi, Kiborloni, Majengo na Msaranga. Mghwira alikwenda pia kuwahamasisha wananchi kujiandikisha katika masoko ya Mbuyuni na Manyema.

Kwa mujibu wa Dk. Mghwira, halmashauri za mkoa huo zilizo chini ya kiwango cha uandikishaji ni Manispaa ya Moshi ikiwa na asilimia 27, Wilaya ya Moshi asilimia 38 na Rombo asilimia 39.

Zingine ni Siha yenye asilimia 41, Same asilimia 45, Hai asilimia 45 na Mwanga ambayo ndio kinara ikiwa imeandikisha kwa asilimia 54.

**DC AZUNGUKA USIKU**

Wilayani Muheza mkoani Tanga, Mkuu wa wilaya hiyo, Mwanasha Tumbo, alitembea usiku na gari lake mitaani kuhamaisha wananachi

kujitokeza kujiandikisha kwa ajili ya uchaguzi huo.

Tumbo alionekana juzi na jana akiwa na gari lake akiwa ameongozana na gari la matangazo.

Mkuu huyo wa wilaya akipita katika vijiwe vyote

vya kahawa, bodaboda na kusimama kisha kuanza kuwahamasisha

wananchi kwenda kujiandikisha.

Alisema uandikishaji kwa ajili ya uchaguzi huo, muda wake umeongezwa na Waziri wa Nchi (Tamisemi), Selemani Jafo, hivyo

wananchi wanatakiwa wajitokeze kujiandikisha ili wapate fursa ya kuwachagua viongozi wanaowapenda.

Jijini Mbeya, watendaji wa Halmashauri ya Jiji, wakiongozwa na Mkurugenzi James Kasusura, waliingia mitaani kuhamasisha wananchi ili wajitokeze kwa wingi kujiandikisha.

**MAMILIONI WAJIANDIKISHA**

Watanzania 15,543,604 sawa na asilimia 68 ya lengo wameshajiandikisha kwenye daftari la wapigakura kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa, huku mkoa wa Pwani ukiongoza kwa kuwa na asilimia 80.

Mkoa huo umeandikisha watu 473,639 ukifuatiwa na Dar es Salaam ulioandikisha watu 2,064,820 sawa na asilimia 77 na Tanga ikiwa ya tatu kwa kuwa na watu 823,194 sawa na asilimia 76.

Mikoa mingine ni Mtwara watu 530,523, Lindi watu 353,649 sawa na asilimia 75 na Iringa watu 381,134 (asilimia 74).

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akielezea tathmini ya uandikishaji ulioanza Oktoba 8 hadi 14.

"Tamisemi imejiwekea malengo ya kuandikisha wapiga kura watapatao milioni 22.916 wenye umri wa miaka 18 na kuendelea kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu. Baada ya hamasa iliyofanywa na wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya, watendaji idadi ya waliojiandikisha imefika watu milioni 15.543 sawa na asilimia 68 ya lengo," alisema Jafo.

Alisema mikoa ambayo ipo chini kiuandikishaji hadi juzi ni Kilimanjaro watu 446,954 sawa na asilimia 48, Kigoma watu 555,856 (asilimia 53) na Arusha watu 551,614 (asilimia 59).

Alisema pia ziko halmashauri sita ambazo zimefanya vizuri zaidi kwa kuandikisha zaidi ya asilimia 95 ambazo ni Mpanda, Mlele (zote Katavi), Kibiti (Pwani), Ngorongoro (Arusha), Songwe na Mbozi (zote Songwe).

Jafo alizitaja pia halmashauri ambazo zimeandikisha chini ya asilimia 50 kuwa ni Manispaa ya Moshi (asilimia 31), Jiji la Arusha (asilimia 32), Msimbo (asilimia 41), Kigoma (asilimia 43), Jiji la Mbeya (46) na Musoma asilimia 49.

**WAKIUKAJI KUKIONA**

Katika hatua nyingine, Waziri Jafo, alivitaka vyombo vya ulinzi na usalama kuwachukulia hatua za kisheria wale wate watakaojiandikisha zaidi ya mara moja.

Alisema kujiandikisha zaidi ya mara moja ni kuhujumu uchaguzi na kwamba adhabu yake ni faini ya Sh. 300,000, kifungo kisichozidi mwaka mmoja au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Jafo alivitaka vyombo vya ulinzi na usalama kufanya uchunguzi hasa kwa wakazi wa Jiji la Dar es Salaam ili kubaini wenye nia ovu ya kuharibu uchaguzi huo.

**Imeandikwa na Godfrey Mushi, KILIMANJARO, Stephen William, MUHEZA, Enock Charles na Mary Geofrey, DAR.**

# Matatani udanganyifu mitihani darasa la saba

INATOKA UK. 2

kwa Mwalimu Peter Sese wa Shule ya Msingi Itale B, Chato na Juma Msengi wa Shule ya Msingi Kanoni (Buchosa) Sengerema na kwa Mwalimu Mkuu Ntwike wa Iramba.

Alisema Septemba 11, katika Shule ya Msingi Sabasaba iliyoko Halmashauri ya Karatu, Mwalimu Mkuu na mlinzi walishirikiana kufanya mtihani na kuwapa majibu watahiniwa.

"Msimamizi Mwalimu Japhet Mollel alikiri kuandaa majibu kwenye vipande vya karatasi kwa kushirikiana na Mwalimu Mkuu Magreth Peter na mgambo Paulo Sixbert," aliongeza.

Mkoani Mtwara katika Halmashauri ya Tandahimba, alisema Mwalimu Mkuu Juma Namgwali wa Shule ya Msingi Chikongola, alishirikiana na msimamizi, Mwalimu Shaban Nalinga, walitoa nje karatasi ya maswali na kuikokotoa na kuwaonesha majibu watahiniwa. Udanganyifu mwingine, kwa mujibu wa Dk. Msonde, ulitokea Ngara ambako walimu Deus Manage, Johakimu Kakuru, Prosper Pius, Erick Balibate na Mwalimu Mkuu Manase Mtinangi walikamatwa kwa kuandaa majibu.

Pia alisema Mwalimu Mkuu, walimu na msimamizi Herzon Eugo walikiri kutoa karatasi za masomo mbalimbali ya mitihani kuwaonyesha watahiniwa. "Tabora, Mwalimu Mkuu, Samwel Dewas wa Shule ya Msingi Kasanga alishirikiana na msimamizi Kashindye Lufunza kufanya somo la Kiingereza na kutoa majibu. Pia Mtwara Mwalimu Mkuu Pius Kazibure wa Shule ya Msingi Kilimanihewa, Nanyumbu na wasimamizi wanane walitoa majibu kwa watahiniwa," alisema.

Aliwataja wasimamizi hao ni Augustino Komba, Ambilikile Mwasile, Apolino Ndomba, Issa Mkanje, Majengo Mihechi, Seleman Ksavoi, Shaziri Mohamed na Yahaya Chihamato.

# Kanda ya Ziwa kinara darasa la saba

INATOKA UK. 2

wamefaulu kwa kupata alama 100 au zaidi ya 250 sawa na asilimia 81.50 na kati yao wasichana ni 395,738 (asilimia 80.87) na wavulana 363,999 ambao ni asilimia 82.20.

Kwa mujibu wa Msonde, watahiniwa waliofaulu walikuwa ni asilimia 77.72 na kufanya kuwe na ongezeko la ufaulu kwa asilimia 3.78.

Hata hivyo, alisema baraza limewafutia matokeo yote watahiniwa 909 kutokana na kufanya udanganyifu na kuzishauri mamlaka husika kuwachukulia hatua waliohusika.

Pia baraza hilo la mitihani limezuia kutoa matokeo ya watahiniwa 81 ambao baadhi yao waliugua, walipata matatizo na kushindwa kuifanya mitihani hiyo yote au baadhi na kutoa fursa kwao kuifanya mwakani.

Dk. Msonde alisema takwimu zinaonyesha ufaulu wa masomo ya Kiswahili, Kiingereza na Sayansi umepanda kati ya kwa asilimia 1.83 na asilimia 6.86 ikilinganishwa na mwaka jana, huku Hisabati ufaulu ukishuka kwa asilimia 1.05.

"Watahiniwa wamefaulu zaidi somo la Kiswahili kwa asilimia 87.25 na somo walilofaulu kwa kiwango cha chini ni Kiingereza kwa asilimia 52.21," alisema.

**KUMI BORA KITAIFA**

Watahiniwa 10 bora kitaifa na shule zao kwenye mabano ni Grace Manga (Graiyaki, Mara), Francis Gwagi (Paradise, Geita), Loi Kitundu (Mbezi, Dar es Salaam) na mshindi wa nne hadi saba ni Victor Godfrey, Aziz Yassin na Goldie Hhayuma wote kutoka Graiyaki.

Wengine ni Daniel Ngassa (Little Treasures, Shinyanga), Hilary Nassor (Peaceland, Mwanza), Mbelele Dalali (Kwema Modern, Shinyanga) na Nyanswi Richard (Graiyaki).

**WASICHANA 10 BORA**

Grace Manga (Graiyaki), Loi Kitundu (Mbezi), Nyanswi Nyamonge (Graiyaki), Neema Mushi (Graiyaki), Maryleocadia Jeremiah (Peaceland), Heavenlight Hhayuma (Twibhoki), Roseleader Steven (Twibhoki), Pilly Zacharia (God's Bridge), Scholastica Shelembi (Little Treasures) na Suzan Fridoline (Little).

**WAVULANA 10 BORA**

Francis Gwagi (Paradise), Victor Godfrey (Graiyaki), Aziz Yassin (Graiyaki), Goldie Hhayuma (Graiyaki), Daniel Ngassa (Little Treasures), Hilary Nassor (Peaceland), Mbelele Dalali (Kwema Modern), Derick Lema (Musabe), Athanas Sekuro (Paradise) na Aron Robert (Mabuga).

**SHULE 10 BORA KITAIFA**

Dk. Msonde alizitaja shule hizo na idadi ya watahiniwa katika mabano kuwa ni Graiyaki (40), Twibhoki (52), Kemebos, Kagera (50, Little Treasures (91), Musabe (52), Tulele, Mwanza (73), Kwema Modern (45), Peaceland (42), Mugini, Mwanza (48) na Rocken Hill, Shinyanga (50).

**MIKOA VINARA KITAIFA**

Mikoa iliyofanya vizuri kitaifa Dar es Salaam yenye watahiniwa 74,940 na waliofaulu ni 69,907 sawa na asilimia 93.28.

Dk. Msonde alitaja mkoa wa pili ni Arusha uliokuwa na watahiniwa 37,645 na kufaulisha 34,509 (asilimia 91.67) na ukifuatiwa na Iringa uliokuwa na watahiniwa 24,998 na waliofaulu ni 22,130 (asilimia 88.53).

"Mkoa wa nne ni Kagera uliokuwa na watahiniwa 46,772 na waliofaulu ni 41,209 sawa na asilimia 88.11. Mkoa wa Katavi umeshika nafasi ya tano ulikuwa na watahiniwa 9,736 wakati waliofaulu ni 8,549 sawa na asilimia 87.81.

"Kilimanjaro imeshika nafasi ya sita iliyokuwa na watahiniwa 34,283 na waliofaulu ni 30,079 sawa na asilimia 87.74 ukifuatiwa na Mbeya uliokuwa na watahiniwa 39,420 na waliofaulu ni 34,306 sawa na asilimia 87.03. Simiyu watahiniwa 28,818 na waliofaulu ni 24,915 sawa na asilimia 86.46," alisema.

Dk. Msonde alisema mkoa wa Njombe umeshika nafasi ya tisa ukiwa na watahiniwa 18,249 na waliofaulu ni 15,768 sawa na asilimia 86.40 na Pwani ukishika nafasi ya 10 kwa kuwa na watahiniwa 29,914 wakati waliofaulu ni 25,467 sawa na asilimia 85.13.

**SHULE UFAULU MFULULIZO**

Dk. Msonde alizitaja shule 10 bora ambazo zimeongeza ufaulu kwa kiasi kikubwa kitaifa kwa miaka mitatu mfululizo iliyoanzia mwaka 2017 na wastani wake kwenye mabano kuwa ni Ngatuni, Ruvuma (72.16), Kinaga, Shinyanga (61.01), Nyahaa, Singida (59.02) na Kisega, Simiyu (58.42).

Zingine ni Mabambasi, Simiyu (58.38), Upolo, Ruvuma (57.91), Semeni, Ruvuma (54.33), Machemba, Ruvuma (54.30), Mwaukoli, Simiyu (53.52) na Gidbasso, Arusha (52.21).

**ZILIZOSHUKA UFAULU**

Dk. Msonde alizitaja shule 10 zilizoshuka ufaulu kwa kipindi hicho cha miaka mitatu na asilimia kwenye mabano kuwa ni Kumba, Morogoro (41.99), Kweshindo, Tanga (33.93), Tandari, Morogoro (33.80), Mbwei, Tanga (30.77), Ndondo, Ruvuma (30.56), Kishinda, Geita (29.06), Bugando, Kagera (28.32), Kwekifinyu, Tanga (28.09), Bubombi, Mara (28.03) na Chihuve, Mtwara (27.33).

**KINARA WAVULANA AFUNGUKA**

Akizungumza na moja ya chombo cha habari, Francis alisema kutokana na ufaulu mfululizo aliopata akiwa elimu ya awali, walimu waliamua kumrusha darasa badala ya kuanza la kwanza aliingia la pili.

"Na sasa matunda yangu ninayaona nimefanya vizuri katika matokeo ya darasa la saba. Ninatarajia kufanya vizuri sekondari," alisema akidokeza kuwa akiwa darasa la pili alishika nafasi ya tatu na mtihani wa taifa wa darasa la nne alipata daraja A masomo yote.

Francis alitaja shule za sekondari ambazo anataka kusoma kuwa ni Ilboru (Arusha), Mzumbe (Morogoro), Mpwapwa (Dodoma) na Pugu, Dar es Salaam kwa sababu zimekuwa zikifanya vizuri.

## HABARI KITAIFA



Wahitimu wa darasa la saba wakifurahi katika mahafali ya tisa ya Shule za Msingi za Atlas, yaliyofanyika mwishoni mwa wiki Madale, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wakulima mahindi kulipwa mil. 315/-

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imetangaza dhamira yake ya kuwalipa wakulima 156 wa mahindi jumla ya shilingi 315,118,510 ikieleza kuwa hatua hiyo inatokana na madai ya kudhulumiwa na mwenyekiti wa Chama cha Ushirika Wilaya ya Kalambo mkoani Rukwa, Linus Kalandamwazye.

Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alitangaza hatua hiyo juzi wakati akizungumza na wanachama wa Muzia Amcos wilayani Kalambo akiwa katika ziara ya kikazi ya siku moja mkoani Rukwa.

Malipo hayo yatawahusu wakulima wa Tarafa ya Mwimbi yenye kata nne ambazo ni Mambwe Kenya, Ulumi, Mkombo na Mwazye kutokana na kupima mahindi yao zaidi ya tani 622.679 kwenye Chama cha Muzia Amcos kilichopewa uwakala na serikali wa kununua mazao kwa wakulima Agosti 8, 2017 kwa makubaliano ya kulipwa ndani ya wiki tatu kutoka tarehe ya kupimwa, lakini hawakulipwa mpaka sasa.

"Kesi ikiwa mahakamani serikali haiwezi kuingilia badala yake wakati tunaendelea na kesi hiyo ninaziagiza taasisi zangu tatu kuchanga fedha kwa ajili ya kuwalipa wakulima hao," alisema Hasunga.

Alisema wanaotakiwa kuchanga fedha hizo kwanza ni Wizara ya Kilimo kwa kushindwa kulishughulikia jambo hilo kwa wakati ili wakulima hao waweze kulipwa fedha zao.

Ameiagiza pia Tume ya Maendeleo ya Ushirika kuchanga fedha hizo kwani wao ndio wasimamizi wa vyama vya ushirika, lakini kwa kipindi chote wameshindwa kushughulikia changamoto hiyo ya wakulima.

Kadhalika, Hasunga aliagiza Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula kuchangia fedha hizo.

Hasunga alisema kuwa serikali haina dhamira ya kuwadunisha na kuwafedhehesha wananchi badala yake imejipambanua kuwanufaisha wakulima katika kilimo.

Alisema kuwa serikali imeamua kuwalipa fedha hizo wakulima ili kuendelea na uzalishaji bora wa mazao ya kilimo, lakini kesi itakapomalizika serikali itazidai fedha hizo. Alimwagiza Mrajisi Msaidizi wa Mkoa wa Rukwa kupanga vizuri madai ya wakulima hao, huku akisisitiza kutoingizwa majina mapya (majina hewa) yasiyohusika na madai ya fedha hizo.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Joachim Wangabo, alimpongeza Waziri Hasunga kwa kukubali kulivalia njuga jambo hilo kwa kuwalipa fedha hizo wakulima kwani kufanya hivyo kutarahisisha wakulima hao kuendelea na uzalishaji wa mazao katika msimu wa kilimo wa mwaka 2019/2020.

Akisoma taarifa ya malalamiko ya kutapeliwa fedha hizo Katibu wa Chama cha MUZIA AMCOS, Geofrey Mbati, aliishukuru Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Rukwa kwa ushirikiano wa karibu katika kipindi chote cha kutafuta mwarobaini wa malipo ya wakulima.

# Ukatili wa kingono kikwazo kwa Tanzania ya viwanda

**Na Yasmine Protace**

MTANDAO wa Jinsia Tanzania (TGNP Mtandao), umesema Tanzania ya viwanda haitaweza kujengwa kama watoto wataendelea kufanyiwa ukatili wa kingono.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Mtendaji wa mtandao huo, Lilian Liundi katika maadhimisho ya kumbukizi ya miaka 20 ya kifo cha Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere.

Liundi ambaye alikuwa mgeni rasmi katika maadhimisho hayo ambapo vijana wa Skauti kutoka shule 50 za Wilaya ya Ilala jijini Dar es Salaam, walionyesha vipaji mbalimbali kupitia tamasha lililoandaliwa la kumuenzi Nyerere, ambapo washindi walipata tuzo.

"Maadhimisho haya yanalenga kumkumbuka Baba wa Taifa kutokana na kuwapenda wanawake na watoto kwa kusimamia haki zao wakati wa uhai wake," alisema.

Alisema TGNP Mtandao inajali haki za watoto na hivyo, ikaamua kuanzisha kampeni ya 1_5_5 namlinda.

Alisema kuanzishwa kwa kampeni hiyo kumezaa matunda ambapo kwa sasa wanafunzi wameweza kujitambua na kutoa taarifa pale wanapofanyiwa ukatili. Fatuma Kalembo, Kamishna wa skauti Wilaya ya Ilala jijini Dar es Salaam, alisema mwaka huu, shule 50 za Wilaya ya Ilala zimeshiriki tamasha.

"Tamasha limekuwa na mwamko na mafanikio mbalimbali ambapo vijana wamejifunza mambo ya ukakamavu, maadili mema na kujitunza katika suala zima la afya.

Akizungumzia changamoto alisema baadhi ya wazazi kuichukulia skauti kama ni mambo ya kisiasa na kuwanyima ruhusa watoto wao kushiriki.

Aliongeza kuwa skauti sio kujifunza masuala ya siasa ni mafunzo ya ukakamavu, maadili mema ikiwamo na kujiamini.

# Miradi ya ulinzi wa mazingira yahimizwa

**Na Mwandishi Wetu**

KITUO cha Kuendeleza Kilimo Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania (Sagcot) kupitia kitengo chake cha 'Green Reference Group' (GRG) wamejipanga kuhakikisha shughuli za kilimo zinazofanywa katika ukanda wake zinazingatia kanuni na sheria za mazingira.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Mtaalamu wa Uhifadhi wa Mazingira wa SAGCOT, John Nakei, alisema lengo ni kufanya kilimo endelevu kisicholeta athari katika mazingira.

"Blueprint ni andiko linaloongoza kufanya shughuli za kilimo na Greenprint ni andiko linaloeleza juu ya kufanya kilimo rafiki na shirikishi,'' alifafanua.

Katika kutekeleza maandiko hayo, kituo kimejikita katika kuangazia mazingira na ushirikishwaji wa jamii katika ukuaji wa shughuli za uwekezaji ili uendane na maendeleo ya watu.

"Tunapenda kuona wabia wetu wakichukua hatua za utunzaji wa mazingira wakati wakitekeleza shughuli zao pasipo kuathiri kizazi cha sasa na kijacho, lakini pia kuwa na kilimo kinachoakisi kwa wananchi,'' alisema Nakei.

Katika kuhakikisha yote hayo yanafanyika, SAGCOT iliunda kamati ya GRG ambayo inawakutanisha wabia kutoka serikalini, sekta binafsi, taasisi za fedha, asasi za kiraia pamoja na wajumbe kutoka vyama vya ushirika.

"Katika kuhakikisha tunakuwa na kilimo chenye tija na endelevu, tumeunda kamati ya GRG ambapo wizara sita zimekuwa sehemu ya kamati hiyo ikiwamo ile ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) na sekta binafsi,'' alisema Nakei.

Nakei aliyataja maeneo muhimu wakati wabia wa kituo hicho wanapoamua kufanya uwekezaji kuwa ni ushirikishwaji wa jamii, utunzaji wa mazingira, mikakati mizuri ya biashara na masuala yote ya msingi ili uwekezaji uwe endelevu.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Sagcot, Geoffrey Kirenga, amekuwa akisisitiza kuwa kilimo endelevu kinategemea mazingira hivyo kazi kubwa ya GRG ni kutoa elimu na mwongozo wa matumizi bora ya ardhi na uzalishaji unaofanywa pasipo kuathiri mazingira.

# Diwani kikaangoni kuoa mwanafunzi

Na **Neema Sawaka,** KAHAMA

MKUU wa Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, Anamringi Macha, ameagiza diwani wa kata ya Kashishi, Magema Samwel, akamatwe na kufunguliwa mashtaka kwa tuhuma za kuoa mwanafunzi.

Diwani Samwel, anatuhumiwa kumwachisha masomo na kumwoa mwanafunzi wa kidato cha pili aliyekuwa anasoma katika Shule ya Sekondari ya Bulige.

Aliagiza diwani huyo wa kata iliyoko katika Halmashauri ya Msalala, kukamatwa maagizo aliyoyatoa, mbele ya Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Saimon Berege na viongozi wa kata na kijiji baada ya kujiridhisha kufika kwenye mji wa diwani na kukuta mwanafunzi huyo akiishi na mama yake mzazi na diwani, huku akifanya kazi za nyumbani hapo.

Mkuu wa Wilaya Macha alisema kuwa diwani huyo ameonyesha vitendo vya aibu kwenye jamii kama kweli amemuoa mwanafunzi, hivyo atafutwe popote alipo na afikishwe kwenye vyombo vya sheria mara moja.

"Mkuu wa shule lazima suala hili ulilifahamu nawe kesho uende, ukaripoti kituo cha polisi utoe maelezo ni muda gani mwanafunzi huyu hafiki shuleni na wazazi wake watafutwe pia wahojiwe kama kweli walimwozesha mwanafunzi ili nao wafunguliwe mashtaka," aliagiza Mkuu wa Wilaya.

Mkurugenzi wa halmashauri hiyo alieleza kusikitishwa na kitendo alichokifanya diwani huyo, akisema kama kweli amemuoa mwanafunzi ni fedheha ila hana majibu ya kutoa kwa kitendo hicho.

Mtendaji wa kata hiyo, Sophia Yusuph, alisema tuhuma hiyo imekuwapo muda mrefu na kuanza kufuatilia ila walipofika jana kwenye mji wa diwani walikuta wamefunga mlango na hakuna mtu yeyote aliyetoka nje mpaka walipoondoka bila kupata taarifa yoyote.

Hata hivyo, mama mzazi wa diwani huyo ambaye aligoma kutaja jina lake, alipohojiwa kuhusu mwanaye kuoa mwanafunzi alikiri ni kweli na kueleza kuwa yeye kaletewa 'mkamwana' mwali, hivyo hawezi kumfukuza ila wazazi wa mwanafunzi huyo ndiyo wenye makosa kukubali mtoto wao kuolewa akiwa na umri mdogo.

Mwanafunzi huyo alipohojiwa na viongozi walioambatana na Mkuu wa Wilaya alikiri kuolewa na diwani huyo na kueleza hivi sasa ameishi naye kwa wiki moja.

Baadhi ya wananchi wanaoishi jirani na diwani huyo, Juliet Malangwa na Alfonce Tumbali walidai kuwa diwani huyo amemwoa binti huyo na kumtolea mahari.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, akisisitiza jambo alipokuwa anazungumza na wananchi wa Kata ya Uyole jijini Mbeya, wakati alipokuwa anawahamasisha kujiandikisha kwa ajili ya kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa. **PICHA NA NEBART MSOKWA.**

# Shule yenye umuhimu kifo cha Nyerere taabani

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

SHULE ya Msingi Bugoyi A, iliyopo Manispaa ya Shinyanga ambayo ina historia ya kipekee inayohusu siku ya kifo cha Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, inaelezwa kuwa iko taabani.

Bugoyi A ina mnara wa Mwalimu Nyerere na siku alipofariki dunia mwaka 1999, Mwenge wa Uhuru ulikuwa shuleni hapo na ulizimwa hapo, inakabiliwa na uchakavu mkubwa wa miundombinu na ukosefu wa vyoo.

Risala ya wanafunzi wa shule hiyo iliyosomwa juzi shuleni hapo na mwanafunzi, Emmanuel Barnaba, kwenye maadhimisho ya kumbukumbu ya miaka 20 ya kifo cha Mwalimu Julius Nyerere, ilieleza.

Barnaba kwa niaba ya wanafunzi wenzake, alisema shule hiyo ina alama kubwa ya mnara wa kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, lakini haiendani na hadhi ya kuwapo kwa kitambulisho hicho, kutokana na kukithiri kwa uchakavu wa madarasa, pamoja na upungufu wa matundu ya choo 55 na kwamba yaliyopo ni 12 pekee.

"Shule yetu hii ya Bugoyi A ina historia kubwa sana katika taifa, ambapo siku anafariki Mwalimu Nyerere mwaka 1999 Mwenge wa Uhuru ulikuwa shuleni hapa na ulizimiwa hapa na kisha kupelekwa kanisani, lakini hatuendani na hadhi ya historia hii kutokana na uchakavu wa madarasa na upungufu wa vyoo," alisema Barnaba.

Mwalimu Mkuu Anna Alute, akizungumza katika tukio hilo, alisema jumla ya wanafunzi ni 1,494 wakike wakiwa 743 wakati wa kiume ni 751. Aidha, matundu ya choo ya wasichana yapo nane, upungufu ni 26, wakati wavulana yapo nane upungufu ni 29, na kusababisha kwa ujumla kukosa matundu ya choo 55.

Naye mgeni rasmi kwenye kumbukizi hizo Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi - CCM Wilaya ya Shinyanga Mjini, Abubakari Mkadamu, aliiagiza ofisi ya mkurugenzi wa wilaya hiyo, kuifanyia maboresho makubwa shule hiyo, ili iendane na hadhi ya historia ya kuwapo mnara wa kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere.

Kwa upande wake Ofisa Elimu Shule za Msingi Manispaa ya Shinyanga, Neema Mkanga, alisema tayari zimetenga fedha kwa ajili ya maboresho ya shule hiyo, ambayo yameanza na ukarabati wa matundu ya choo ya zamani, huku wakijipanga kujenga vyoo vingine vipya.

## Wakumbushwa kufuta ujinga kumuenzi Nyerere

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANAFUNZI wa shule na vyuo mbalimbali wamehimizwa kumuenzi Rais wa kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere, kwa kusoma kwa bidii na kufaulu kwenye masomo pamoja na kutafuta njia za kujitegemea ambayo ni njia ya kumshinda adui ujinga.

Wamekumbushwa kuwa Mwalimu Nyerere, alikuwa akipambana kutokomeza maadui watatu hapa nchini ambao ni umaskini, maradhi pamoja na ujinga na kila adui alikuwa na mikakati ya kumkabili na kwa upande wa ujinga, ni kuongeza bidii ya kujielimisha na wanafunzi wanapaswa wasome kwa bidii ili taifa liweze kuwa na watu wenye uelewa.

Hayo yalibainishwa juzi na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Shinyanga Mjini Abubakari Mkadamu, kwenye maadhimisho ya kumbukizi za miaka 20 ya kifo cha Mwalimu Nyerere, yaliyofanyika kwenye Mnara wa Nyerere katika Shule ya Msingi Bugoyi A.

Huko Bugoyi A siku ya kifo cha Mwalimu Mwenge wa Uhuru ulikuwa shuleni hapo na ulizimwa.

Alisema zawadi peke ambayo wanafunzi watampatia Mwalimu Nyerere ni kusoma kwa bidii ili kumfukuza adui ujinga, na kuachana na tabia ya kuchezea elimu ikiwamo, kuharibu miundombinu ya shule, kwenda na simu shuleni na kuanza kuchati vitu vya kijinga pamoja na kuangalia picha za ngono vitendo ambavyo ni kumkosea Baba wa Taifa.

"Natoa rai kwa wanafunzi nchini kumuenzi Mwalimu Nyerere, Baba Yetu wa Taifa, kwa kujituma na kujikita kwenye masomo na kupata ufaulu mzuri ili kumfukuza adui ujinga, hiyo ndio zawadi pekee ambayo mtampatia huko alipo. Ikiwa adui huyu ni miongozi mwa maadui watatu aliokuwa akiwapinga sana hapa nchini," alisema Mkadamu.

Pia alitoa wito kwa wananchi kumuenzi Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere kwa kudumisha amani na upendo vitu ambavyo aliviachia taifa.

Alionya watu kuacha kufanya viashiria vyovyote vya kutaka kuivunja amani hiyo, bali wananchi wawe wazalendo na kuipenda nchi yao.

Katibu wa Skauti Wilaya ya Shinyanga Mjini ambaye ndio waandaaji wa maadhimisho hayo ya kumbukizi za miaka 20 ya kifo cha Mwalimu Nyerere, Vicent Kanyogoto, alisema Mwalimu anapaswa kuenziwa na Watanzania wote kwa vitendo.

Alisema kama skauti wamekaa siku nne kwenye eneo hilo la Mnara wa Mwalimu Nyerere kwenye Shule ya Bugoyi A Mjini humo, kwa kufanya shughuli mbalimbali kama usafi wa mazingira na kuwapatia vijana elimu ya kuwa wazalendo pamoja na kudumisha amani na upendo.



HABARI ARUSHA

# Waaswa kutumia viboko shuleni kuleta nidhamu

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Arusha Gabriel Daqarro, amewataka walimu jijini Arusha kutosita kuwaadhibu kwa viboko wanafunzi wenye nidhamu mbaya ili kurejesha adabu, heshima na utii shuleni, jambo alilosema ni chachu ya kuongeza ufaulu.

Gaqarro alitoa angalizo hilo, wakati akizungumza na walimu wa ahule mbalimbali za jiji la Arusha katika maadhimisho ya Siku ya Mwalimu Duniani, hivi karibuni.

Alisema suala la utii na nidhamu shuleni halina mjadala , hivyo aliwataka walimu kujua kuwa wanao wajibu wa kutumia viboko pale inapolazimika, lakini bila kumwonea mwanafunzi.

"Ninachowaomba walimu ,mrejeshe nidhamu kwa wanafunzi na msikubali kuzoeana nao.

Kwani kufanya hivyo, itasaidia kurudisha nidhamu shuleni lakini pia msimwonee wanafunzi na kutumia nguvu kupita kiasi wakati mnapotoa adhabu kwani mtaweza kutenda kosa la 'jinai' na kuingia hatiani," alionya Daqarro.

Mkuu huyo wilaya, aliagiza kutohamishwa ovyo kwa walimu bila kupewa fedha za uhamisho huku akiwataka walimu wanaoidai serikali kuwa wavumilivu wakati madai yao ya msingi yanashughulikiwa .

Awali walimu hao kupitia risala yao iliyosomwa na Katibu Mkuu wa Chama cha Walimu Mkoa wa Arusha(CWT) Abraham Kamwela, waliorodhesha changamoto mbalimbali zinazowakabili ikiwemo mazingira magumu wanayokutana nayo kazini.

Pia walilalamikia kuchelewesha kubadilishiwa mishahara kwani tangu walipopewa barua za mabadiliko ya mishahara, bado hakuna mabadiliko yaliyofanyika ikiwamo suala la kupandishwa madaraja.

Aidha, waliiomba Halmashauri ya jiji la Arusha kuwakopesha viwanja ili wajenge nyumba za kuishi kwani baadhi yao wanaishi kwenye mazingira magumu.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Jiji la Arusha Dk. Maulid Madeni, licha ya kuwapongeza walimu hao kwa jitihada zao za kuufanya mkoa wa Arusha kuwa kinara katika ufaulu kitaifa , aliwaomba walimu wazidi kujituma zaidi huku akiwaahidi kuweka mazingira wezeshi na bora ya kazi .

Hata hivyo , Madeni aliitupia lawama kamati ya maandalizi ya maadhimisho hayo kwa kutowatendea haki walimu kwa kufanya mkutano huo usiku huku wakinyeshewa na mvua na kung'atwa na mbu.

Madeni aliwataka walimu hao kumkumbuka mwasisi wa taifa Baba wa Taifa Julius Nyerere, ambaye aliwatoa wananchi kwenye zama za ujinga kwa kuhimiza elimu na kujielimisha.

Katika hatua nyingine Madeni, aliwasisitiza walimu kujiandikisha ili kupiga kura katika uchaguzi mdogo wa serikali za mitaa utakaofanyika mwezi ujao Novemba 24 .



Wahitimu wa mahafali ya 31 ya Chuo cha Utumishi wa Umma mkoani Tanga yaliyofanyika mwishoni mwa wiki, wakimsikiliza Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dk Francis Michael (hayupo pichani). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ahimiza kujiandikisha uchaguzi wa S/Mitaa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti amewataka wananchi wa mkoa huo, kujiandikisha kwa wingi ili waweze kutumia haki yao ya kikatiba ya kuchagua viongozi wa serikali za mitaa na vijiji.

Mnyeti akizungumza jana na wananchi wa kata ya Matui wilayani Kiteto, alisema japokuwa watu wanahamasika kujiandikisha lakini wanatakiwa wajitokeze kwa wingi zaidi ili waweze kutumia haki yao ya msingi.

Alisema ili waweze kupiga kura na kumchagua mwenyekiti wa kijiji, kitongoji, mtaa na wajumbe wa serikali wanapaswa kujiandikisha kwanza kama sharia inavyoelekeza.

Alisema huu ndiyo wakati wa kujiandaa na kuwaondoa madarakani viongozi wabadhirifu wakiwamo waliosababisha migogoro kwa kuuza ardhi ya wananchi bila kufuata taratibu na sheria.

"Mjiandikishe kwa wingi ili muwachague viongozi wa serikali za mitaa ambao watawaongoza kwa muda wa miaka mitano kuanzia sasa," alisema Mnyeti.

Aidha, mbunge wa Babati Mjini (CCM), Pauline Gekul, alisema tayari ameshajiandikisha jana kwenye mtaa wa Ngarenaro ulioko kata ya Bagara.

Gekul alisema amejiandikisha kwenye mtaa huo pamoja na wananchi wengine 260 wa eneo hilo.

"Japokuwa mvua inanyesha lakini tunaendelea kuhamasisha wananchi wa Babati wakajiandikishe kwa wingi sasa hivi tunaelekea mtaa wa Baloa ulio katika kata ya Nangara,"alisema

Hadi juzi wananchi wa mkoa wa Manyara takribani 267,945 waliripotiwa kuwa wameshajiandikisha wakati makisio yalikuwa ni kusajili watu 747,796.

# Aagiza wananchi kulipwa fidia zao

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAKAZI wawili wa kata za Bwawani na Matui, Wilaya Kiteto, walionyang'anywa ardhi yao kwa ajili kujengwa shule za msingi, wamefidiwa maeneo baada ya Mkuu wa Mkoa wa Manyara Alexander Mnyeti kuagiza walipwe haki yao.

Wananchi hao, walifikisha kilio chao kwa Mnyeti kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika kata za Matui na Bwawani, wilayani Kiteto, akiwa kwenye ziara yake ya siku tano ya kukagua miradi ya maendeleo, kusikiliza kero na changamoto za wananchi na kuzipatia ufumbuzi.

Mnyeti alisema kutokana na maeneo ya wananchi kuchukuliwa na taasisi za serikali na kujengwa shule za umma, walistahili kupewa maeneo mengine kama fidia.

"Mkurugenzi nakuagiza utoe maeneo mengine wapewe hawa wananchi waliochukuliwa maeneo yao kwa ajili ya kujenga shule hata kama ni suala la maendeleo lakini wanapaswa kupata haki zao,"alisema

Aliwaambia wananchi kuwa baadhi ya kero ambazo hazina sababu, zinapaswa kutatuliwa kwani wananchi wengine wataichukia serikali bila sababu ya msingi.


Mkazi wa kijiji cha Matui Juma Masare, aliyekuwa anadai ardhi, alilalamika kuporwa eneo lake ekari 12, na serikali ya kijiji ili kujengwa shule ya msingi.

"Baada ya kupora eneo langu serikali ya kijiji ilijenga shule lakini hawakunifidia japokuwa kuna maeneo mengine ," alisema Masare.

Mkazi wa Kijiji cha Wezamtima kata ya Bwawani, Endeni Kilangi, akitoa malalamiko yake kwa Mkuu wa Mkoa alisema alinyang'anywa na serikali ya kijiji hicho ekari 70, ili kujenga shule ya msingi bila kufidiwa.

"Shamba langu, lilichukuliwa na serikali ya kijiji lakini sikufidiwa eneo jingine ilihal kuna maeneo mengine wangeweza kunipa haki yangu," alisema Kiangi.

Alieleza kuwa japokuwa anapenda maendeleo ya jamii lakini angepaswa kufidiwa ardhi kwani kijiji kina seheumu nyingi na kubwa ya ardhi ya kuwapatia.





# Tuhuma kuuzwa mapipa ya lami zaibuliwa upya

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

TUHUMA za kutoweka kwa mapipa ya lami yanayodaiwa kuuzwa kinyemela miaka kadhaa iliyopita na taasisi moja iliyopo Kibosho, Wilaya ya Moshi zimeibuliwa upya.

Aliyeibua tuhuma hizo katika kikao cha Bodi ya Barabara Mkoa wa Kilimanjaro kilichofanyika siku chache zilizopita ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Michael Kilawila.

Alidai kuwa viongozi wa taasisi hiyo waliuza mapipa hayo ya lami yaliyotolewa na serikali kwa ajili ya kutengeneza barabara ya Kibosho miaka kadhaa iliyopita.

"Kinachoshangaza ni kwamba mapipa ya lami, yaliuzwa bila kufuta taratibu za manunuzi na mauzo ya serikali na hata zilizopatikana, hazijulikani zilikwenda wapi ama zimefanya kazi gani, huku wananchi wakiendelea kushangaa," alidai.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti huyo, viongozi wa taasisi hiyo waliuza kila pipa moja kwa Sh. 90,000.

Pia alidai kuwa wananchi walichangia gharama za kusafirisha lami hizo kutoka jijini Dar es Salaam kwa kukatwa pesa zao kwenye mauzo ya kahawa na kufikishwa kwa mapipa ya lami Kibosho.

Akichangia mjadala huo, Diwani wa Kata ya Okaoni, Morice Makoi, alidai hakuna mali ya serikali iliyouzwa na taasisi inayotajwa, bila kufuta taratibu.

"Hakuna lami iliyoibiwa ama kuuzwa na hiyo taasisi, kwanza utawezaje kuuza mali ya Kibosho bila kufuata taratibu, kwani wao walikuwa wapi, kwa sababu hakuna kiongozi aliyehongwa kuficha jambo hilo," alieleza Makoi.

# Mchango wa marehemu Dk. Mengi wakumbukwa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MCHANGO mkubwa wa rasilimali fedha uliowahi kutolewa na aliyekuwa Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, hayati Dk. Regnald Mengi, hasa katika sekta ya elimu, umelifanya Kanisa Katoliki, Jimbo la Moshi kukumbusha upya matendo yake ya huruma.

Jana, Wakili wa Askofu na Msimamizi wa Jimbo Katoliki la Moshi, Padri Deogratius Matiika, alitumia mifano mingi ya matendo ya huruma aliyoyafanya Dk. Mengi wakati wa uhai wake wakati akizungumza na wananchi.

Padri Matiika alikuwa akizungumza na wananchi kutoka mikoa mbalimbali, wakati wa Jubilee ya miaka 50 ya Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Kibosho iliyopo Moshi Vijijini.

Alimtaja hayati Dk. Mengi katika ushiriki wake wa kusaidia sekta ya elimu, akitolea mfano mchango wake wa Sh. bilioni moja aliotoa mwezi Februari, mwaka huu kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa miundombinu ya Shule ya Sekondari Jumuishi ya wenye ulemavu ya Kitaifa ya Mtakatifu Pamakio iliyopo Kijiji cha Kimashuku, Wilaya ya Hai.

"Hakika wapo Watanzania ambao hatutawasahau au kusahaulika katika jamii na vizazi vijavyo kutokana na mchango wake mkubwa katika jamii. Jamii karibu yote inamkumbuka na kumwombea mema huko alipo. Watu wenye ulemavu, wenye mahitaji maalum na hasa wasichana na watu wengine wasio na uwezo wanalia wakikumbuka matendo yake ya huruma," alisema Padri Matiika.

Itakumbukwa kuwa kutokana na matendo yake ya huruma, Februari mwaka huu, Kanisa Katoliki lilimtunuku tuzo maalum ya msamaria mwema ya 'Good Samaritarian Special Needs Awards' kwa kutambua mchango wake katika kusaidia jamii ya watu wenye ulemavu nchini ili kufikia ndoto zao.

Katika jubilee hiyo, Mhashamu Askofu Flavian Kasala wa Jimbo la Geita, aliwasihi Watanzania kuunga mkono juhudi za Rais Dk. John Magufuli za kupiga vita mimba za utotoni kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari.

Mhashamu Askofu Kasala ni Makamu wa Rais wa Baraza la Maaskofu wa Katoliki Tanzania (TEC). Wakati wa mahubiri yake, Askofu Kasala alisema utashi huo wa Rais Magufuli wa kutaka wanafunzi wa kike kutimiza ndoto zao za elimu, kwa kukemea hadharani ukatili huo unaoendelea katika jamii ni ishara tosha kwamba ni kiongozi aliyepewa karama ya kushughulikia matatizo ya watu wake. Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bodi ya Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Kibosho, Aloyce Mushi, alisema ujenzi wa shule hiyo ulitokana na michango ya wananchi ambayo walikatwa kwenye mauzo ya kahawa.

Alisema ni michango hiyo, ndiyo ambayo ilihamasisha wananchi kote nchini kuchangia ujenzi wa shule hiyo.

Katika jubilee hiyo, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Avemaria Semakafu, aliwapongeza wanafunzi waliowahi kusoma shuleni hapo, kwa kujitokeza kukarabati zahanati ya shule hiyo na kuahidi ukarabati wa mabweni na miundombinu mingine.

Hata hivyo, wakati wa chakula, Mwenyekiti wa wanafunzi waliowahi kusoma katika shule hiyo, Monica Dimelo, alianzisha mfuko wa ukarabati wa mabweni na zaidi ya Sh. 500,000 zilikusanywa.



Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, akiongea na wananchi wa Kijiji cha Mwamboku, Kata ya Kashishi katika Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama, muda mfupi baada ya nyumba zao kuezuliwa na upepo mkali kisha kubomolewa na mvua iliyokuwa ikinyesha. **PICHA: NEEMA SAKAWA**

# Diwani Chadema ahamasisha uandikishaji kupiga kura usiku nyumba kwa nyumba

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

ZIKIWA zimebaki saa chache kumalizika kwa muda wa nyongeza wa kujiandikisha uchaguzi wa serikali za mitaa na vijiji, diwani mmoja wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) katika Manispaa ya Moshi, amezua gumzo kutokana na staili yake kupita usiku wa manane kwenye nyumba kuhamasisha wananchi wake kujitokeza.

Diwani huyo ambaye ni Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Katanini, Jonathan Makupa, kwa siku tatu mfululizo amekuwa akipita saa 9:00 usiku mitaani akiwa na kipaza sauti akiwaomba wananchi kujitokeza kwenye uandikishaji.

Katika matangazo yake usiku huo amekuwa akisikika akisema: "Wananchi wangu, mimi ni diwani wenu na mwenyekiti wa kamati ya ulinzi na usalama ya kijiji hadi ngazi ya kata. Nawaombeni sana kesho msiniangushe, twendeni tukajiandikishe, maendeleo yetu yanaanzia katika hili."

Makupa alianza Oktoba 11 hadi 14 kupita katika mitaa ya Magereza, Kibosho Road, Shauri Yako, Kanisani kwa Tegee maarufu Mombasa na mtaa wa Kasablanka.

Jana, alipoulizwa na Nipashe uamuzi wake wa kuhamasisha usiku wa manane wananchi kujitokeza kujiandikisha badala ya kupita muda wa kazi, Makupa alisema wakati huo anaoutumia wananchi wake wanamwelewa kuliko wakati mwingine wowote.

"Unajua mimi ni mwenyekiti wa kamati ya ulinzi na usalama ngazi ya mtaa hadi kata ninayoiongoza, nawajua wananchi wangu wanakuwa wapo vizuri muda gani. Muda huo ni fursa nzuri kwangu na muhimu ya kuongea nao, na pia wakati huo wote wapo majumbani," alisema.

Uchaguzi huo wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji unatarajiwa kufanyika nchini kote, Novemba 24, mwaka huu.

Oktoba 13, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali (Tamisemi), Selemani Jafo, alitangaza kuongeza muda wa siku tatu katika orodha ya uandikishaji wa daftari la wapiga kura.

Hadi kufikia juzi, watu milioni 11 walikuwa wamejiandikisha kwa mujibu wa Waziri Jafo.

Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Dar es Salaam ndiyo inayotajwa kuwa katika hali mbaya ya uandikishaji wapigakura kutokana na wananchi wachache kujitokeza.

# Lishe Bora ni Lazima kwa Ulimwengu Usio na Njaa

Na Fred Kafeero

SIKU ya Chakula Duniani kwa mwaka huu inahimiza juu ya umuhimu wa kuhakikisha lishe bora na endelevu inapatikana kwa wote na kwa gharama nafuu kupitia kauli mbiu 'Lishe Bora kwa Ulimwengu Usio na Njaa'

Takwimu za hivi karibuni zinaonesha kuwa watu zaidi ya milioni 820 wanakabiliwa na njaa na milioni 670 watu wazima na watoto milioni 120 wasichana kwa wavulana (miaka 5 hadi 19) wana unene wa kupindukia, na watu zaidi ya milioni 40 chini ya miaka 5 wamepitiliza uzito.

Huu ni ushahidi kuwa ulimwengu unakabiliwa na changamoto zinazoongezeka zinazohusiana na uhakika wa chakula na lishe jinsi idadi ya watu inavyoongezeka; changamoto nyingine zikiwa katika hali ya mabadiliko ya tabia nchi; afya - hususan juu ya mabadiliko ya ghafla ya milo na tabia za ulaji zinazotokana na utandawazi, kukua kwa miji na vipato.

Walaji, hususan wale wa mijini hawana muda wa kutosha kuandaa vyakula majumbani. Wamejikuta wameingia katika kile kinachoitwa maisha ya kisasa ambayo kwa kiasi kikubwa zinategemea ununuzi wa bidhaa katika maduka makubwa, sehemu za kuandaa vyakula kwa haraka huko barabarani na kwenye migahawa. Hii inatufanya tutegemee milo yenye wanga mwingi, sukari, mafuta, chumvi, vyakula vilivyochakatwa, nyama na aina nyingine ya bidhaa za budhaa zitokanazo na wanyama.

Mchanganyiko wa milo mibovu na aina ya maisha ya kutokuufanyisha mwili kazi za kutosha, sio tu katika nchi zilizoendelea, lakini pia katika nchi za kipato cha chini, ambapo njaa na uzito uliopindukia zinapatikana pamoja. Wataalam wa afya watengaza kwa sauti ya juu kwamba milo mibovu ni sababu kuu ya vifo vitokanavyo na magonjwa yasiyoambukizwa, yakijumuisha mahonjwa ya moyo, kisukari na aina fulani za saratani.

Kama ilivyo katika nchi kadhaa, Tanzania kwa upande mwingine nayo ina tatizo la watu kuwa na lishe duni inayosababishwa na milo ya watu kupungukiwa na viini lishe muhimu ambavyo vinahitajika na mwili kwa ajili ya afya njema au kusababishwa na ugonjwa, malezi na lishe mbovu ya utototni, uchafu wa mazingira na ule wa mtu binafsi, kutofikia huduma za jamii na maji masafi.

Habari njema ni kwamba suluhu ya kutokomeza changamoto hii ya utapiamlo wa aina zote ipo ndanina uawezo wetu ambazo, lakini inahitaji juhudi kubwa zaidi na za pamoja kwa vitendo katika ngazi ya ulimwengu na hata taifa.

Kuweza kufikia Ulimwengu Usio na Njaa ifikapo 2030 ni ajenda pana na inahitaji juhudi za pamoja kufikia hilo. Kutokomeza njaa ni mojawapo ya juhudi hizo, lakini pia kuhakikisha watu wanafaidika na lishe bora ni nyingine.

Hakuna mashaka kuwa Tanzania inaweza kubadilisha hali hii, kwa vile kama nchi imeweza kukidhi mahitaji yake ya chakula kwa



Mwakilishi Mkazi wa FAO nchini Tanzania, Fred Kafeero.

zaidi ya asilimia 120 na kwamba imejaliwa vyakula vingi na vya aina tofauti tofauti vya asili.

Hata hivyo, kuna umuhimu wa kuongeza uwekezaji katika programu za kuhamasisha lishe bora nchi nzima, kuimarisha elimu ya lishe kwa makundi yote, na zaidi ya yote wakulima wanahitaji motisha ili kuongeza na kuchanganya mazao katika uzalishaji wao wa chakula chenye ubora.

Kutokomeza utapiamlo katika aina zake zote ni sehemu muhimu katika majukumu ya FAO na pia ni Lengo la Pili la Maendeleo Endelevu. Kama shirika la utaalamu wa masuala ya chakula na kilimo, FAO inaimarisha uwezo wa nchi kutathmini na kufuatilia hali ya lishe, kusaidia ubadilishanaji wa maarifa na teknolojia, na pia huweka viwango vya ubora.

Kwa juhudi za pamoja kutoka kwa wadau wote (wakulima, Serikali, watafiti, sekta binafsi na walaji) tunaamini lishe bora inaweza kufikiwa na kuihakikisha kuwa Tanzania hakuna njaa ifikapo 2030. Wote basi tujitume kwa ajili ya kuhakikisha lishe bora kwa ajili ya maisha yenye furaha, afya njema na ubora.

Siku ya Chakula Duniani pia ni Siku ya Kuzaliwa kwa FAO.

***Mwandishi wa Makala hii ni Mwakilishi wa Shirika la FAO katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

# Ushirikiano wa FAO na Serikali ya Tanzania kuhakikisha lishe bora



Baadhi vyakula vinavyoangukia katika kundi la lishe bora. **PICHA ZOTE: FAO.**

LISHE bora ina umuhimu mkubwa sana kwenye maisha ya watu. Ulaji wa chakula chenye lishe bora inasaidia kuzuia utapiamlo wa aina zote.

Kwa sasa dunia inakabiliwa na tatizo linaloongezeka la watu wenye utapiamlo unaotokana na njaa au kukosa viini lishe muhimu kwenye vyakula ambavyo ni muhimu kwa ajili ya afya ya mwili. Idadi ya watu wanaougua utapiamlo sugu hususan watoto chini ya miaka 5 ni kubwa sana kwenye nchi zinazoendelea. Mifumo mibovu ya huduma na ulishaji watoto, usafi duni wa binafsi na ule wa mazingira na ushindwa kufikia huduma za afya na maji safi ni miongoni mwa sababu kubwa za tatizo hili.

Kwa upande mwingine, ulaji wa chakula uliopitiliza nao unaongezeka, na athari zake ni unene na uzito uliopitiliza. Hali hii inapekelea kuongezeka kwa matatizo ya shinikizo ladamu, kisukari, magonjwa ya moyo, kiharusi na aina fulani ya saratani.

Ukuaji wa haraka wa miji na mabadiliko ya tabia za kimaisha zinapekelea mabadiliko katika ulaji wa chakula ambapo watu zaidi wanakula vyakula vilivyochakatwa kutoka viwandani ambavyo vina wanga wanga, sukari, mafuta au chumvi nyingi. Hii ikichanganywa na maisha ya kutoushughulisha mwili vya kutosha inachangia kwenye ongezeko la kasi na magonjwa yasiyoambukizwa.

Tanzania pia haijaachwa kwenye huu mkumbo. Idadi za wenye lishe duni na wale zilizopitiliza nayo pia inaongezeka. Karibu theluthi ya watoto wote wanaugua utapiamlo unatokana na njaa au lishe duni. Wakati huo huo, idadi ya watu wanaougua magonjwa yasiyoambukizwa pia nayo inaongezeka tena kwa kazi kubwa.

FAO inashirikiana na Serikali ya Tanzania kukabiliana na changamoto hizi zinzohusiana na masuala ya lishe kupitia miradi na afua kadhaa hapa nchini.

Kuandaliwa kwa Miongozo ya Lishe Bora, kwa mfano, kunalenga kuweka msingi wa chakula na lishe bora kwa umma, afya na sera za kilimo pamoja na program za elimu ya lishe ili kuhamasisha ulaji bora na tabia sahihi za maisha. Zinatoa ushauri kuhusu vyakula, makundi ya vyakula na tabia za ulaji ili kuhakikisha watu wanapata viini lishe vyote muhimu kwa umma ili kuwa na afya njema na kuzuia magonjwa sugu.

> Nia ni kutambua sababu za msingi zinazoathiri uhakika wa chakula na lishe hapa nchini na hivyo kuweza kuweka mikakati ya muda mrefu ya kukabiliana na hali hiyo.



Mwakilishi Mkazi wa FAO nchini Tanzania, Fred Kafeero, akikagua shughuli za kinamama kuhusiana na lishe bora.

Tanzania ilikuwa nchi ya kwanza kuanza mchakato wa miongozo hii mwaka 2017 kwa kupitia ushauri wa kitaalam wa FAO. Mpaka sasa rasimu za miongozo hii zipo tayari ikitilia maanani hali halisi za Tanzania Bara na Zanzibar na ipo katika hatua za mwisho za kupitiwa kabla ya kuridhiwa na kupitishwa rasmi. Kazi kama hiyo inafanyika katika nchi nyingine za Afrika kama vile Rwanda, Swaziland, Zambia na Zimbabwe kwa kupitia ushauri wa kitaalam wa FAO.

FAO pamoja na wadau wengine wa maendeleo inafanya kazi na Serikali ya Tanzania kupitia Mfumo wa Uchambuzi wa Uhakika wa Chakula na Lishe (MUCHALI) kwa Bara na Mfumo wa Taarifa za Tahadhari za Uhakika wa Cha wa Chakula na Lishe wa (Zanzibar FS-NIEWS) kufanya tathmini ya uhakika wa chakula na lishe na sababu kuu za ukosefu wa chakula kwa baadhi ya maeneo hapa nchini.

Nia ni kutambua sababu za msingi zinazoathiri uhakika wa chakula na lishe hapa nchini na hivyo kuweza kuweka mikakati ya muda mrefu ya kukabiliana na hali hiyo.

Pia ni muhimu kutambua kuwa usalama wa chakula na lishe hauwezi kufikiwa bila usalama wa chakula. Pale chakula kinapokuwa sio salama, watoto hawawezi kusoma na watu wazima hawataweza kufanya kazi. Maendeleo yataathirika. Upatikanaji na ufikiwaji wa kiwango cha kutosha cha chakula ambacho ni salama na chenye lishe bora ni muhimu kwa ajili ya kutunza uhai na kulinda afya bora.

Hapa Tanzania timu ya wataalam ya FAO kwenye eneo la usalama wa chakula ipo nchini kuisaidia nchi kuweza kupata misaada ya kukabiliana na tatizo la sumu kuvu. Hii pia inajumuisha kuimarisha uwezo wa kitaifa na ule wa serikali katika kukabiliana na hatari inayosababishwa na sumu kuvu kwa kuhaikisha kuna utunzaji mzuri wa mazao baada ya kuvuna ili kuepusha kuvamiwa na sumu kuvu.

FAO kwa sasa inatoa ushauri wa kitaalam kwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kupitia mradi wa miaka miwili unaoitwa 'Kuboresha Vyakula vya Wauzaji wa Mtaani' kwa ajili ya kuhakikisha usalama na lishe bora katika jiji la Dar es Salaam. Mradi huu unakuza uelewa kwa wauzaji chakula wa mtaani kuhusu viwango vya ubora vya usalama, urasimishaji wa biashara zao na umuhimu wa uhakikisha chakula chao kina uwiano wa makundo yote muhimu kwa ajili ya afya ya umma.

Kama sehemu ya Mradi wa Mradi wa pamoja wa Umoja wa Mataifa kwa kushirikiana na SIDA, FAO inatoa msaada wa kitaalam kwa ajili ya kupitia mfumo wa utunzaji na mimea hapa nchini kwa kuimarisha uwezo wa Serikali kutoa huduma za ukaguzi na mazuio ili kuepusha hatari inayoweza kuenezwa na visumbufu na magonjwa katika minyororo ya kilimo na chakula.

Kupitia Mfuko wa Fleming wa Wizara ya Afya ya Uingereza, FAO imekuwa ikifanya kazi na Serikali ya Tanzania kukuza uelewa na mifumo sahihi ya kupambana na vijuasumu au antibayotiki katika sekta za kilimo na chakula ikijumuisha afya ya wanyama, uzalishaji nafaka, uvuvi na ufugaji samaji kuhakikisha usalama wa chakula. Unatekelezwa chini ya mfumo wa afya moja na umeboresha usalama wa chakula kwa kiasi kikubwa katika afya ya wanyama nay a mazingira.

Msaada wa FAO wa kitaalam kwa Wizara ya Kilimo kwa ajili ya kuwezesha kilimo ambacho ambacho kinatilia maanani masuala ya lishe unadhihirika katika ngazi ya serikali za mitaa, ambapo kwa mfano kwa kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo hapa Tanzania (TARI) usambazaji wa mapando ya viazi lishe vyenye utajiri wa Vitamin A unaendelea kule Dodoma ili kuboresha afya za watu. Vivyo hivyo, misaada ya kifedha na utaalam vimetolewa kule katika Kituo cha Utafiti wa Kilimo Maruku Bukoba, ambapo mazao mbali mbali yenye utajiri wa viini lishe yalihamasishwa miongoni mwa wakulima, kama vile maharage lishe ambayo yamesambaza mkoa mzima wa Kagera kwa sasa ili kuwahakikishia watu lishe bora. Hii ilijumuisha na shughuli za uhamasishaji wa lishe bora na kampeni kwenye mkoa mzima.

Kila mtu ana haki ya kupata chakula salama, chenye lishe bora na cha kutosha. Tunaposherehekea Sikuya Chakula Duniani mwaka huu, hii iwe fursa ya uhakikisha kuwa tunakula vyakula salama na vyenye lishe bora kuanzia ngazi ya uzalishaji mpaka kwenye sahani. Kila mmoja katika mnyororo wa chakula anawajibika kuhakikisha kuwa kunakuwepo lishe bora. Ni muda wa vitendo sasa!

***This is more f plant protection than nutrition***

# Kliniki nchini Tanzania yawasaidia mama mzazi na watoto wake kupata mlo kamili na kuimarisha kipato chao



Mtoto wa Happy, Yalumbwe, mwenye miezi 14 akifanyiwa uchunguzi na muuguzi wakati alipohudhuria kliniki. **PICHA: WFP/ALICE MARO**

**Na Alice Maro**

KLINIKI nchini Tanzania yawasaidia mama mzazi na watoto wake kupata mlo kamili - na kuimarisha kipato chao

Mwanzoni mwa mwaka 2018, Happy Kennethy Mbalay na mumewe walikuwa wakitarajia kupata mtoto wao wa tatu.

Mume alikuwa akitafuta kazi na hatimaye aliipata–lakini ilikuwa mbali, takribani kilomita 1,000. Kwa hiyo, ilimpasa kuhama. Hii ilimaanisha kwamba Happy, aliyekuwa mjamzito, licha ya changamoto mbalimbali za kimwili na kihisia za ujauzito, alibaki peke yake kukabiliana na changamoto za kulea watoto wao wawili wenye umri wa miaka saba na minne.

Wawili hawa waliishi katika nyumba ndogo ya vyumba viwili katika eneo la vilimavilima la Buigiri mkoani Dodoma, nchini Tanzania. Ilimuwia vigumu sana Happy kuendesha maisha kwa fedha kidogo alizotumiwa na mumewe. Kwa hiyo, aliamua kutafuta njia nyingine ya kuingiza kipato.

Licha ya kuwa na ujauzito wa wiki 20, mama huyu mwenye miaka 31, alianza kupita nyumba hadi nyumba akiuza nguo kwa wanakijiji wenzake. Halikuwa jambo jepesi. Huku akiwabembeleza wanakijiji kununua nguo zake zenye rangi na mapambo ya kupendeza, Happy alipata wanunuzi wachache tu. Ilimuwia vigumu kuwapatia watoto wake mlo bora.

Kwa bahati nzuri, takribani majuma manne yaliyopita , Happy alikuwa amejiandikisha kwenye mradi wa Boresha Lishe. Kupitia mradi huu aliweza kuhudhuria kliniki katika zahanati ya Buigiri, ambayo ni ya serikali na ilikuwa ikisaidiwa na mradi huo (ambao ulifadhiliwa na Umoja wa Ulaya na Japan kwa pamoja).

> Happy alifaulu kurejesha mkopo wake na alibakiwa na fedha za kutosha kununua nyama, maziwa, siagi, sukari, matunda na vyakula vya aina nyingine ambavyo hakuweza kuvimudu hapo kabla.



Kila mwezi, Happy alipokea msaada wa unga maalumu wa lishe ulioongezewa virutubisho pamoja na vitamini na madini muhimu. Alielimishwa pia kuhusu lishe na kupata ushauri kuhusu namna bora ya kuwalisha watoto wachanga. Kliniki pia ilifuatilia maendleo yake ya lishe.

Kupitia vipimo vya kila mwezi, Happy alipata msaada wa kilishe aliouhitaji na hatimaye alijifungua mtoto wa kiume mwenye afya njema. Mtoto huyu alikuwa na uzito wa kilo 3.7. (Alimpa mtoto huyu jina la Yalumbwe Emmanuel Mussa, jina la kwanza ambalo ni la lugha ya Kigogo lilimaanisha "Apewe Sifa".)

Baada ya kujifungua mtoto wake, Happy alirudi kwenye utaratibu wa kufanyiwa vipimo na kuendelea kupokea msaada wa unga wa lishe hadi mtoto wake alipotimiza miezi sita. Hivi sasa, Yalumbwe ametimiza miezi 14 na anapokea mgao wa chakula cha lishe maalumu.

**MAFUNZO YA MAPISHI**

Kupitia uangalizi wa Save the Children, ambalo ni shirika linalofanya kazi na WFP katika utelekezaji, watumishi wawili wa afya, ambao ni kiungo kati ya kituo cha afya na jamii, hupewa jukumu la kufuatilia mara kwa mara maendeleo ya wanufaika wote wa mradi, wakiwemo Happy na Yalumbwe.

Wakati wa ujauzito wake, Happy alipata msaada zaidi kutoka kwa watumishi wa ustawi wa jamii na kumpa mafunzo ya usafi wa mazingira (WASH–matumizi bora ya maji, usafi binafsi na wa mazingira); mafunzo ya kupika vyakula vya lishe na pia mafunzo kuhusu VICOBA–kupata huduma za kuweka akiba na kukopa kupitia vikundi vya akiba na kukopeshana kijijini.

Kupitia utaratibu wa VICOBA, Happy alipata jibu la matatizo yake ya kupata fedha ili kuimarisha biashara yake. Baada ya kuchukua mkopo wa Shilingi za Kitanzania 50,000 aliwekeza katika kuuza nguo bora zaidi. Kwa sababu hii aliongeza wateja na kujipatia kipato zaidi.

Happy alifaulu kurejesha mkopo wake na alibakiwa na fedha za kutosha kununua nyama, maziwa, siagi, sukari, matunda na vyakula vya aina nyingine ambavyo hakuweza kuvimudu hapo kabla.

Kuimarisha ubora wa mlo na kuwa na vyakula mchanganyiko

Mchanganyiko wa milo ni miongoni mwa mbinu muhimu za kuhakikisha mama wazazi na watoto wao wanapata lishe bora na ya kutosha. Ni kwa sababu hii kwamba mradi wa Boresha Lishe hutoa elimu ya mbinu za kilimo bora.

Happy alijifunza namna ya kuanzisha bustani za mbogamboga nyumbani ambapo alilima mbogamboga za aina tofautitofauti kwa ajili yake na watoto wake. Analima jamii ya mikunde na matembele. Happy pia alijifunza kutumia kifaa kinachotumia nishati ya jua ili kukaushia na kuhifadhia mbogamboga za ziada kwa matumizi ya baadaye–hasa muhimu wakati wa kuadimika kwa mbogamboga.

Kabla ya kupata mafunzo, Happy alikuwa na kawaida ya kudharau matunda ambayo hupatikana muda mwingi katika maeneo yao, pasipo kujua kuwa yana virutushibo vingi. Haya ni pamoja na ubuyu, zambarau na ukwaju–ambayo yote yanapatikana kwenye masoko ya jirani. Tangu ajiunge na mradi wa Boresha Lishe, Happy amejifunza njia bora za kupata milo na kujenga uelewa mkubwa zaidi kuhusu chakula.

"Sasa kwa vile nimepata elimu kuhusu manufaa ya kula mlo kamili, ninahakikisha kwamba familia yangu inapata milo tofautitofauti," anasema.

Happy anaongeza kusema kwamba anafurahia kula milo bora na kujitunza na kuiangalia familia yake. Pia amekuwa mhamasishaji asiye rasmi wa mradi wa Boresha Lishe hapo nyumbani kwake na anawapa marafiki na majirani zake elimu kuhusu lishe bora.

# Kesho mwisho, wapigakura changamkieni kujiandikisha



Wananchi wakiwa katika foleni ya kujiandikisha kwa ajili ya kupiga kura. **PICHA: MTANDAO**

**Na Sabato Kasika**

RATIBA ya uandikishaji wa orodha ya wapigakura katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2019, imefanyiwa marekebisho ili kuwapa fursa Watanzania wengi zaidi kujiandikisha.

Uandikishaji huo ulianza Oktoba 8 na ulitarajiwa kumalizika Oktoba 14 mwaka huu, lakini ratiba hiyo imesogezwa hadi Oktoba 17 huku sababu kuu za kuongeza muda wa kujiandikisha zikiwa mbili.

Hiyo ni kwa mujibu wa tangazo kutoka Ofisi ya Rais Tawala la Mikoa na Serikali za Mitaa, kwamba limetolewa chini ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2019 (Matangazo ya Serikali Na 371, 372, 373 na 374 ya Waziri mwenye dhamana, Seleman Jafo, anasema tangu uandikishaji wa wapigakura ulipoanza Oktoba 8, umeendelea kupata mafanikio makubwa, kwa vile kufikia Oktoba 12, zaidi ya wananchi milioni 11 walikuwa tayari wamejiandikisha katika daftari la orodha ya mpigakura wa Serikali za Mitaa.

Anasema, pamoja na mafanikio hayo kumekuwapo na changamoto kuu mbili wakati uandikishaji ukiendelea, hasa mvua nyingi iliyonyesha na kusababisha watu wengi kushindwa kujiandikisha kwa wakati.

> Maeneo mengine baadhi ya kaya zimejikuta zikizingirwa na maji, hususani Mkoa wa Morogoro na ukanda wa Mkoa wa Pwani.

"Maeneo mengine baadhi ya kaya zimejikuta zikizingirwa na maji, hususani Mkoa wa Morogoro na ukanda wa Mkoa wa Pwani," anasema Jafo.

Sababu nyingine ya kuongeza muda inaelezwa kuwa ni baadhi ya watu kuchanganya mambo na kushindwa kutambua kuwa uandikishaji huo hauhusiani na Daftari la Kudumu la Wapigakura.

"Wamekuwa wakichanganya kwamba kwa kuwa wameshaandikisha katika daftari la kudumu na kupewa kitambulisho cha mpigakura, wamekuwa na dhana isiyo sahihi kwamba vitawawezesha kupiga kura,"anasema.

Jafo anabainisha kuwa dhana hiyo imesababisha baadhi ya wananchi kuchelewa kujiandikisha katika zoezi la uandikishaji kwa ajili ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba 24 mwaka huu.

"Kutokana na changamoto kuu hizo, na pia kutokana na misingi ya utoaji haki na kwa kuzingatia masharti ya Kanuni za Uchaguzi za Mitaa kama zilivyoainishwa hapo juu, natoa mwongozo kuwa zoezi la uandikishaji linaongezwa siku tatu zaidi za uandikishaji hadi Oktoba 17, 2019 badala ya tarehe 14 Oktoba, iliyotangazwa awali," anasema.

## KUTOJIANDIKISHA

Yapo mambo ya msingi ambayo mtu asipojiandikisha atayakosa katika uchaguzi huu unaokuja, ikiwamo kutokuwa na haki ya kumchagua mgombea mwenye sifa nzuri ambaye anahitajika katika mtaa.

Vilevile mwananchi atakosa fursa ya kumkataa kiongozi anayesababisha kero mbalimbali, kama uzembe, kutokuwajibika, mbadhilifu, mporaji wa mali za wananchi au za wanyonge.

Katika hilo, asiyejiandikisha atakosa fursa ya kumchagua Mhamasishaji wa maendeleo katika mtaa wake, atakosa fursa ya kumkataa kiongozi anayeuza maeneo ya umma yakiwamo ya wazi.

Wananchi pia wakumbuke kuwa kwa mtindo huo watakosa fursa ya kumchagua mkuu wa ulinzi na usalama wa mtaa, mtu atakayewaondolea kero zinazotishia amani na utulivu katika mtaa wao.

Watambue kuwa watakosa fursa ya kumchagua mhamasishaji mkuu wa maendeleo katika mtaa wao kama huduma za afya, elimu, miundombinu mbalimbali kama vile barabara, taka na mitaro.

Katika mazingira, wanaweza kukosa fursa ya kumchagua kiongozi mwajibikaji na mwadilifu anayejua kuwa huduma za ofisi za Serikali za Mitaa ni bure, ikiwamo kugonga mihuri ili kupitisha nyaraka mbalimbali zinazohitaji ridhaa ya ngazi ya chini ya uongozi wa serikali.

Asiyejiandikisha atakosa fursa ya kuzuia michango holela na tozo za mtaa zisizokuwa na baraka za wananchi, kama tozo kubwa za taka, michango isiyo ya lazima, kiwango kikubwa cha ada za ulinzi shirikishi.

Pia kuna kukosa kumchagua kiongozi anayewaunganisha wananchi kwa kufanya mikutano ya kisheria ile ya kila miezi miwili, kuwaleta wananchi pamoja na kukosa kiongozi mwadilifu.

Kiongozi atakayewasomea mapato na matumizi ya fedha za mtaa na zile zinatoka halmashauri kuja kwenye mtaa na fedha zinazokusanywa na kamati za mtaa. Hivyo kutojiandikisha ni kupoteza haki yako ya msingi ya kuchagua kiongozi unayemtaka.

## RATIBA HII NI FURSA

Hatua ya serikali kuongeza muda ni fursa pekee kwa wale, ambao bado walikuwa wanasuasua au kuamini kwamba vitambulisho walivyonavyo vinahusika kwenye uchaguzi huu wa Novemba.

Kuongezwa kwa muda wa kujiandikisha kumeambatana na elimu, ambayo kimsingi inapaswa kuzingatiwa na Watanzania wote wenye sifa za kuajindikisha kwa ajili ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Jambo la muhimu ni kila mmoja kuizingatia na kuacha kuchanganya mambo ili aweze kushiriki kikamilifu kwa ajili ya kuwapata viongozi wanaofaa kuongoza mitaa kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Elimu ya mpigakura imekuwa ikitolewa maeneo mbalimbali nchini kwa lengo la kumwezesha kila Mtanzania kushiriki katika uchaguzi, hivyo ni muhimu kuitumia elimu hiyo vizuri.

Ingawa suala la kushiriki katika uchaguzi ni la hiyari na kidemokrasia, lakini bado wananchi wanatakiwa kutambua kwamba kutoshiriki kunaweza kusababisha wakapatikana viongozi wasiofaa.

Hii inaweza kuwa imeifanya serikali kuona haja ya kuongeza muda wa kujiandikisha ili wale ambao hawajapata nafasi hiyo waweze kujitokeza katika muda huo ambao umeongezwa.

Wakurugenzi walishaelekezwa kutekeleza demokrasia vizuri kwenye uchaguzi huo, na tayari serikali ilishatoa uwezeshaji kwa kila eneo, na haitarajii kusikia hujuma, hivyo wananchi hawana budi kuunga mkono juhudi hizo.

Uchaguzi huo unatarajia kutumia zaidi ya Sh. bilioni 82, Wananchi wazitendee haki fedha hizo kwa kujiandikisha kwa wingi na kisha kushiriki katika uchaguzi ili kuwapata viongozi bora na si bora viongozi.

# Vijana 10,000 Afrika washiriki kongamano lao Kigali Rwanda



Baadhi ya vijana waliokutana kwenye Kongamano la siku tatu jijini Kigali nchini Rwanda. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

JUMLA ya Vijana 10,000 kutoka nchi zote za Afrika na baadhi ya wawakilishi wa mashirika ya vijana ulimwenguni wamekutana jijini Kigali nchini Rwanda, kujadiliana mkakati wa kubadili mtazamo potofu kuhusu jinsi bara la Afrika linavyotazamwa.

Hili ni kongamano la siku tatu ambapo viongozi wa serikali na wakuu wa serikali wanachanganua sababu za kulifanya bara la Afrika liendelee kuonekana dhaifu mbele ya macho ya walimwengu.

Karibu nchi zote zimetuma vijana wawakilishi kwenye kongamano hili. Mazungumzo yanayoendelea katika kongamano hilo ni kuhusu nafasi ya vijana katika kutatua changamoto zinazolikabili bara hilo.

Moja ya changamoto zilizotangazwa na vijana hao ni ukosefu wa utawala bora barani Afrika, kitu ambacho wanasema kimelifanya bara hilo kushindwa kupiga hatua ya haraka kimaendeleo katika sekta mbalimbali.

Ni kongamano ambalo kwa siku yake ya kwanza liliongozwa na Rais Paul Kagame akiwa na viongozi wengine wakiwemo mawaziri wa vijana kutoka Afrika ambapo vijana walipata nafasi ya kuuliza maswali na kuonyesha changamoto zinazolikabili bara hilo.

> Hatua ya kuanzia inaweza kuwa nyumbani, yaani kama nyumbani kwako ni Mali, Cape Verde, Cameroon na kadhalika, yaani pale ulipotoka wakati unakuja hapa.



Rais Paul Kagame wa Rwanda. **PICHA: MTANDAO**

**USHAURI WA RAIS KAGAME**

Rais Kagame amewaambia vijana hao kwamba changamoto hizo zipo barani Afrika lakini itakuwa vigumu kuziondoa ikiwa hakutakuwepo na muungano wao.

"Hatua ya kuanzia inaweza kuwa nyumbani, yaani kama nyumbani kwako ni Mali, Cape Verde, Cameroon na kadharika, yaani pale ulipotoka wakati unakuja hapa," anasema na kuongeza:

"Baada ya hapo unakwenda kwa majirani na kwa kufanya hivyo maana yake unazidi kuungana na mwisho zile changamoto ambazo zilikuwa ni za nchi moja sasa zinakuwa za bara zima na hivyo kuzikabili inakuwa rahisi kwa sababu sasa sote tumekwishaungana na kuzikabili kwa pamoja," anasema Rais Kagame.

Imetangazwa kwamba zaidi ya asilimia 60 ya wakazi wa Afrika ni vijana ambao kimsingi ndio wanakabiliwa na changamoto za ukosefu wa ajira ambapo mwisho wa siku wanarubuniwa na kujiingiza kwenye vitendo ambavyo ni hatari kwa usalama wa bara lao.

Kongamano hili la siku tatu linajaribu kuzitazama changamoto na nafasi ya vijana na kuzikabili. **BBC**

TUJIKUMBUSHE

# SHAKIL AFRIDI

## • Ni Daktari aliyeisaidia CIA kumpata Bin Laden

DAKTARI wa Pakistan ambaye aliisaidia Marekani kumpata kiongozi wa kundi la al-Qaeda, Osama Bin Laden amekata rufaa dhidi ya hukumu yake jela.

Ni mara ya kwanza ambapo kesi ya Shakil Afridi inasikilizwa katika Mahakama ya wazi.

Jaji aliahirisha kesi hiyo hadi Oktoba 22, kufuatia ombi la waendesha mashtaka.

Kinachodaiwa kufanywa na Dk. Afridi kilikuwa aibu kubwa kwa Pakistan, lakini yeye mwenyewe anadai ya kwamba alinyimwa haki yake wakati wa kusilizwa kwa kesi hiyo ambapo alihukumiwa kifungo cha miaka 33 jela.

Hakushtakiwa rasmi kwa jukumu lake katika operesheni hiyo ya mwaka 2011, ya kumsaka na kumuua mtu aliyekuwa akitafutwa sana duniani.

Kufungwa kwake jela kulisababisha hisia kali, hatua iliyosababisha Marekani kufutilia mbali msaada wake kwa Pakistan wa takriban dola milioni 33, ikiwa ni dola milioni moja kila mwaka kwa hukumu yake katika Mahakama ya Peshawar.

Rais wa Marekani Donald Trump aliahidi katika uchaguzi wa 2016, kwamba atamwachilia huru Afridi baada ya dakika mbili iwapo atachaguliwa, lakini hilo halijafanyika.

Huku daktari huyo akionekana kuwa shujaa Marekani, nchini Pakistan anaonekana kama msaliti ambaye alilileta aibu taifa hilo.

Makomando wa jeshi la wanamaji la Marekani walisafiri kwa helikopta kutoka Afghanistan mpaka Pakistan na kumuua aliyepanga njama za mashambulizi ya Septemba 11 na kuondoka na mwili wake bila kuzuiwa.

Na hatua hiyo ilizua maswali mengi ya iwapo jeshi la Pakistan lilikuwa linajua iwapo Bin Laden alikuwa nchini humo.

Pakistan imesalia kuwa mshirika asiyeaminika katika vita vya Marekani dhidi ya wapiganaji wa Kiislamu.

### DK. SHAKIL AFRIDI NI NANI?

Dk. Afridi alikuwa daktari mkuu katika Hospitali ya Wilaya ya Khyber. Akiwa mkuu wa huduma za afya, alikuwa amesimamia baadhi ya mipango kadhaa ya chanjo zinazofadhiliwa na Marekani.

Kama mfanyakazi wa serikali, alianzisha mpango wa chanjo ya Homa ya Ini (Hepatitis B), ikiwemo katika mji wa Abbottabad ili kubaini iwapo waliokuwa wakiishi katika eneo hilo ni ndugu za bin Laden.

Inadhaniwa kwamba mfanyakazi mmoja wa Dk. Afridi alitembelea nyumba ya akina Osama bin Laden na kuchukua vipimo vya damu, lakini haijulikani iwapo hilo lilisaidia Marekani kumpata Osama.

Dk. Afridi alikamatwa Mei 23, 2011 siku chache tu baada ya Bin Laden kuuawa. Alidaiwa kuwa na miaka 40 wakati huo.

Ni mambo machache yanayojulikana kuhusu maisha yake, mbali na kwamba alitoka katika familia maskini na kufuzu katika chuo cha matibabu cha Khyber 1990.



Theodore Hall. **PICHA: MTANDAO**



Osama Bin Laden. **PICHA: MTANDAO**

> Huku daktari huyo akionekana kuwa shujaa Marekani, nchini Pakistan anaonekana kama msaliti ambaye alilileta aibu taifa hilo.

Familia yake imekuwa ikiishi katika maficho tangu kukamatwa kwake, ikihofia shambulio la kijeshi.

Mkewe ni msomi kutoka Abbotabad ambaye alikuwa mwalimu mkuu wa Shule ya serikali kabla ya kwenda mafichoni.

Wawili hao wana watoto watatu, wavulana wawili na msichana mmoja, watoto wawili wakiwa watu wazima kufikia sasa.

Januari 2012 , maofisa wa Marekani walikiri hadharani kwamba Dk. Afridi alikuwa akikifanyia kazi kikosi cha Ujasusi cha Marekani. Lakini haijulikani jukumu lake lilikuwa ni lipi katika CIA.

Hakusema lolote kuhusu jukumu lake wakati kesi yake ilipokuwa ikisikilizwa na tume ya Abbottabad kuhusu mauaji hayo.

Dk. Afridi hakujua ni nani aliyekuwa akilengwa katika operesheni hiyo wakati alipoajiriwa na CIA kulingana na uchunguzi wa Pakistan.

### ALIHUKUMIWA NA NANI?

Ijapokuwa awali alikuwa ameshtakiwa kwa kutekeleza uhaini, Dk. Afridi alifungwa Mei 2012, baada ya kupatikana na makosa ya kufadhili kundi la Lashkar-e-Islam, kundi la wapiganaji lililopigwa marufuku.

Alihukumiwa kifungo cha miaka 33 jela kwa madai ya kushirikiana na kundi hilo na Mahakama moja ya kikabila, ijapokuwa hukumu hiyo ilipunguzwa na kufikia miaka 23, baada ya kukata rufaa.

Daktari huyo pia alishutumiwa kwa kutoa msaada wa dharura kwa wapiganaji hao na kuyaruhusu makundi kama hayo katika hospitali ya serikali alikokuwa akisimamia.

Familia yake imekana mashtaka hayo na mawakili wake wanasema kwamba fedha alizotoa ni kikombozi cha dola 6,375 ili kumwachilia, baada ya kutekwa 2008.

Kutoka katika chumba chake cha jela mwaka 2012, alidaiwa kuliambia shirika la habari la Fox News kwamba alikuwa ametekwa na kuteswa na majasusi wa Pakistan. Mwaka mmoja baadaye alifanikiwa kupeleka barua aliyoandika kwa mkono kwa wakili wake akisema kwamba amenyimwa haki

### KWA NINI HAKUSHTAKIWA KWA KUISAIDIA MAREKANI?

Hilo haliko wazi, lakini suala hilo la Bin Laden lilikuwa pigo kubwa kwa Pakistan.

Ijapokuwa maofisa walikasirishwa na kile walichokiona kama ukiukaji wa haki ya uhuru wa taifa hilo, huduma ya ujasusi ililazimika kukiri hadharani haikujua kwamba mwanzilishi huyo wa kundi la al - Qaeda alikuwa akiishi kwa siri katika eneo hilo katika nyumba ya ghorofa tatu ambayo ilikuwa imezibwa na kuta ndefu kwa miaka kadhaa.

Kwa nini kesi hiyo inasikilizwa mahakamani wakati huu?

Kufikia sasa, mchakato mzima wa kesi yake umeanzishwa chini ya usimamizi wa sheria za uhalifu za Uingereza, ambazo zilitawala maeneo ya kikabila karibu na mpaka na Afghanistan hadi mwaka uliopita.

Mahakama za kikabila zilisimamiwa na maofisa wa utawala, zikisaidiwa na baraza la wazee wa kikabila na hawakuwa wakifuata sheria inavyohitajika.

Hiyo ilionekana kuwa njia rahisi ya kukabiliana na Afridi, ikiwa si kwa suala la kufanyika hadharani.

Lakini kuunganishwa kwa maeneo ya kikabila na mkoa wa Khyber Pakhtunkhwa mwaka uliopita, kunamaanisha kwamba kesi hizo zimerudishwa katika mahakama za kawaida. Katika siku ya kusikilizwa kwa kesi yake, hukumu yake inaweza kupunguzwa ama kuongezwa, kwa kuwa waendesha mashtaka watahoji.

Tangu alipohamishwa mwaka uliopita kutoka jela ya Peshwar hadi Punjab, kumekuwa na madai kwamba huenda akaachiwa, ikiwezekana kupitia kubadilishana wafungwa na Aafia Siddiqui, mtu aliyedaiwa kuwa mshirika wa al - Qaeda ambaye kwa sasa yuko jela Marekani. **BBC**




Jengo la Kiwanda cha Nguo cha Urafiki, moja ya matunda ya uongozi wa Mwalimu Julius Nyerere. **PICHA: MTANDAO**

# Ubinafsishaji na mtazamo wa Mwalimu Julius Nyerere

**Na Mwandishi Wetu**

MIAKA 20 ya kifo cha Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, taifa linamkumbuka na kusherehekea maisha yake ya kujitoa kuitumikia Tanzania ili kuiondoa kwenye umaskini na kuifikisha kwenye hatua ya kujitegemea na maisha bora kwa kila mwananchi.

Kikubwa alichojitahidi kwenye kuimarisha uchumi ni kujenga viwanda.

Alianzisha viwanda kwenye sekta zote kuanzia kilimo, mifugo, usafiri, vyakula na kwenye maeneo mengine mbalimbali.

Mwalimu anakumbukwa kwa kujenga viwanda vya baiskeli kama Nabico kilichokuwa kikiunda baiskeli, kilikuwapo kiwanda cha kuzalisha maturubai, vibiriti, magunia na kadhalika.

Morogoro wanamkumbuka kwa karakana kubwa ya kuchonga vipuri vya chuma kwa ajili ya mitambo mbalimbali huko Mang'ula.

Moshi kuna kiwanda kikubwa cha Machine Tools, wakati wakulima wa nafaka watamuenzi kwa uzalishaji mkubwa wa shiyiri na ngano uliokuwa ukifanywa na Shirika la Taifa la Chakula na Kilimo la NAFCO huko Arusha.

Mwalimu Nyerere hakutaka Tanzania ihangaike kwa kusaka mafuta. Kwa kushirikiana na wawekezaji kutoka Italia, taifa lilijenga mtambo wa kusafisha mafuta wa TIPER ulioko Kigamboni Dar es Salaam, ambao kazi zake zilivuka mipaka ikisafisha mafuta na kuyapeleka Zambia kupitia bomba la Tazama.

Kiwanda cha nyama cha Tanganyika Packers, kilichokuwa kikubwa Afrika Mashariki na Kati ni mambo makubwa yaliyofanywa na Mwalimu ambayo sasa yanashuhudiwa kama maajabu ya kitaifa.

Lakini, hatua zilizochukuliwa kuanzia mapema miaka ya 1990 zilipelekea kuvibinafsisha viwanda hivyo.

## MIONGO BILA MWALIMU

Mwalimu alikuwa na maono makubwa na mengi aliyatimiza kwa kuweka msingi wa kila alichokuwa amekikusudia.

Kwa kiasi kikubwa alifanikiwa kuiacha Tanzania ikiwa nchi ya viwanda mpaka kifo chake pamoja na kwamba taifa lilikuwa limejitumbukiza kwenye sera za ubinafsishaji wakati huo.

Uuzaji wa mashirika na kampuni za umma ulivihamisha viwanda na mashirika kutoka kwenye sekta ya umma kwenda kwa watu binafsi, wakiwamo wageni.

> Baadhi ya viwanda viliahidiwa kuwa vingeboreshwa na kuzalisha zaidi, kinachoonekana ni kubakia kama vilivyokuwa au hali yake kuwa duni zaidi kuliko hata kabla ya kubinafsishwa.

Licha ya Mwalimu kuanzisha viwanda kuanzia vya kusokota nyuzi, kusindika asali, kuunda baiskeli hadi vya kutengeneza zana za kilimo, alishuhudia vifo vya taasisi hizo.

Hata hivyo mpaka umauti unamkuta Oktoba 14, 1999 huko London Uingereza, Mwalimu, hakukubaliana na ubinafsishaji.

Ubinafsishaji ambao uligubikwa na majina mengi, wapo waliouita 'ugenishaji' ulionekana kuwa ungekuwa na tija kwa sababu ya ahadi lukuki zilizotolewa kila mara kwenye soko la madalali waliokuwa wakiuza viwanda hivyo.

Ungesikia utazalisha ajira zaidi, utaleta teknolojia ya kisasa, utaongeza kodi badala ya kupewa ruzuku na kuzalisha bidhaa za kutosheleza soko la ndani na ziada itauzwa nje. Utaboresha pale serikali ilipokwamia.

## KIINI MACHO

Ukweli ni kwamba miaka 20 baada ya Mwalimu, ubinafsishaji umechangia sehemu ndogo kuamsha na kuendeleza viwanda alivyojenga Baba wa Taifa.

Baadhi ya wawekezaji hawakutimiza malengo yaliyokusudiwa hata walipouzia viwanda hivyo. Kwa ujumla wamevichezea.

Mathalani, kiwanda cha matairi cha General Tyre, hakijainuka tangu kilipobinafsishwa hadi sasa ambapo Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) limeahidi kuwekeza na kukipa sura mpya.

Watanzania wameendelea kushuhudia matairi ya kila aina yenye ubora na hata yaliyo duni yakitoka nje ya mipaka huku kiwanda chao kikiendelea kulishwa kwa mpira licha ya kwamba kipo mikononi mwa taasisi ya serikali.

Si hivyo, tu hata kiwanda kikubwa cha nyama kilichojengwa kwa gharama kubwa cha Tanganyika Packers kilichoko Kawe Dar es Salaam, kadhalika nacho hakijatimiza azma ya kubinafsishwa.

Tanganyika Packers kiwanda cha kisasa kilichokuwa na mitambo ya kisasa na mashine za hali ya juu za kukata nyama kimebakia magofu na kuta zilizobanduka na kubomoka na hakuna aliyelieleza taifa kuwa mashine hizo ziko wapi.

Ni jambo jema kuwa eneo la kiwanda hicho linatumika kwa ajili ya maombi, sala na kumtukuza Mungu. Ni uwanja wa makanisa japo ardhi hiyo imemilikishwa na Shirika la Nyumba la Taifa kwa ajili ya kuendelezwa.

Wakati Tanzania ni ya tatu kwa uzalishaji wa nyama Afrika, haina kiwanda kikubwa cha kusindika nyama licha ya kwamba serikali imeendelea kualika wawekezaji kujenga viwanda vya kusindika nyama na mazao ya mifugo.

Mkoani Kilimanjaro, mitambo ya kutengeneza vipuri na mashine za viwandani ambacho ndicho kiwanda cha Moshi Machine Tools nacho kimeendelea kuzorota bila mafanikio. Viwanda vikubwa vya nguo vya Mwatex, Sunguratex na Urafiki vimebakia kuyumbishwa na wawekezaji waliovinunua ambao hawajawasaidia Watanzania kubadili maisha yao.

Katika viwanda hivyo vya nguo mathalani kiwanda cha Mutex, kinaelezwa kuwa kilikuwa na mitambo ya kisasa na mashine zenye teknolojia ya hali ya juu, baadhi zikitokea Ufaransa nazo hazifahamika ziliko na pengine lini kitaanza kuzalisha vitenge bora.

Ni wazi kuwa kwa ujanja, viwanda vingi vilivyobinafsishwa vimebadilishwa matumizi badala ya kuendelezwa.

Kwa mfano kuna vingine jijini Dar es Salaam vinatumika kuweka vipuri ili kuzalisha bidhaa nyingine. Viwanda hivyo alivyojenga Mwalimu baada ya kuuzwa vimegeuzwa maghala ya kuweka bidhaa za mataifa ambayo wafanyabiashara au kampuni zake zilinunua viwanda au kampuni hizo zilizoanzishwa kwa kazi kubwa na Baba wa Taifa.

Baadhi ya viwanda viliahidiwa kuwa vingeboreshwa na kuzalisha zaidi, kinachoonekana ni kubakia kama vilivyokuwa au hali yake kuwa duni zaidi kuliko hata kabla ya kubinafsishwa.

Baadhi ya viwanda hivyo (majina tunayo) vilikuwa na maghala ya kuweka bidhaa mbalimbali, vimeyakodisha kwa ajili ya kampuni nyingine kuhifadhi bidhaa zake. Tena wawekezaji hao wanalipwa kodi.

Kilichoonekana baada ya ubinafsishaji ni hujuma maana mitambo iling'olewa, mashine kuondolewa na kubaki viwanda hewa.

## JITIHADA MPYA

Serikali ya Awamu ya Tano imejipambanua kwa kupigia chapuo kuimarisha viwanda na ujenzi wa uchumi wa kujitegemea ili kumuenzi Baba wa Taifa ambaye ndiye mwanzilishi wake.

Ujenzi wa viwanda ni suala linalosukumwa kwa kasi kubwa na serikali ya awamu ya tano.

Licha ya kwamba Mwalimu alikuwa na njozi ya kuijenga Tanzania ya viwanda na alianzisha mtandao mkubwa wa viwanda, hata kama hakukamilisha lengo hilo alifanya kazi kubwa.

Licha ya changamoto nyingi, kazi ya Mwalimu ya kuanzisha viwanda inapata tena msukumo mpya kwa msingi kuwa yaliyopita si ndwele watu wagange yajayo.

Ujenzi wa viwanda umeanza kwa kasi zaidi na mkoa wa Pwani sasa ndio wa viwanda badala ya Morogoro kama ilivyokuwa enzi za Mwalimu.

Taifa limeshuhudia ujenzi wa viwanda vya kutengeneza marumaru, mabati na viuadudu huko Kibaha mkoni Pwani.

Mashirika ya umma yamechukuliwa tena na serikali na yamefufuka.

Lipo Shirika la Reli (TRC) na la ndege ATCL yanafanya kazi za kuaminika. Taasisi za umma, kama Mifuko ya Taifa ya Akiba ya Wafanyakazi –NSSF na PPF zimehamasishwa kuanzisha viwanda, mathalani mradi wa sukari wa Mkulazi mkoani Morogoro.

Taifa limeanzisha minada ya kuuza dhahabu na tanzanite badala ya kuiuza nje moja kwa moja.

Si hivyo tu shirika la NDC linashirikiana na wabia mbalimbali kuanzisha miradi kama uwekezaji wa kuzalisha magadi soda mkoani Arusha na kuwekeza kwenye umeme wa makaa ya mawe.

Leo taifa linapokumbuka kifo na maisha yaliyotukuka aliyoishi Mwalimu, ni vyema kuthamini na kulinda kwa nguvu zote mali za Watanzania.

# Mikwamo kisiasa ya Netanyahu yamchanganya mkuu wa majeshi



Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu. **PICHA: MTANDAO**

**Na Ani Jozeni**

MKUU wa majeshi ya Israel, Luteni-Jenerali Aviv Kochavi anajitahidi kutokuhitajika kuongea chochote mbele ya vyombo vya habari au wakuu wenzake serikalini, kutokana na hitilafu ya kutafsiriwa atasema nini kuhusu Waziri Mkuu Benjamin Netanyahu.

Wachunguzi wa habari wanasema kuwa suala hilo linampa tabu mkuu wa majeshi kuliko kupanga mbinu za kukabiliana kijeshi na Iran, kazi ambayo anaifanya kila iitwapo leo.

Ila kumkwepa amiri jeshi mkuu mwenye matatizo ambaye kamanda wa jeshi asingependa kuonekana naye au kusema lolote juu yake imekuwa mtihani wa aina yake kwa kamanda.

Baadhi ya wachunguzi wanasema kuwa hali hiyo inaleta matatizo katika kupata taarifa sahihi kuhusu hali ya usalama wa taifa, kwani mkuu wa majeshi ndiye anayeweza kusema kwa uhakika hali ilivyo, na atasita kufanya hivyo kulingana na jinsi atakavyotafsiriwa kuhusiana na hali ya waziri mkuu.

Akisema kuwa hali ni nzuri inaweza kueleweka kuwa ni kumsaidia Netanyahu, na akisema kuwa hali ni mbaya inaweza ieleweke kuwa anataka kuwasaidia wakuu wa zamani wa majeshi ya Israel walioko katika chama pinzani cha 'Buluu na Nyeupe,' chama cha kizalendo kinachotaja rangi za bendera ya Israel. Hataki mojawapo.

Taarifa zinasema kuwa Luteni jenerali Kochavi ambaye ndiyo kwanza amemaliza mwaka mmoja katika nafasi hiyo anajitahidi kuhakikisha kuwa jeshi la Israel, haliingii katika mikwaruzano inayoikumba nchi hiyo kisiasa hivi sasa.

> "Netanyahu alikabana koo na aliyekuwa mkuu wa majeshi, Jenerali Benny Gantz, ambaye hadi sasa amesita kushiriki serikali ya pamoja na Netanyahu.

Kuna migawanyiko katika chama cha Likud kinachoongoza nchi hiyo na kushindwa kupata serikali mpya hata baada ya uchaguzi mkuu kurudiwa, kwanza ukifanyika mwezi Machi na ukarudiwa mwezi uliopita, kwa matokeo yale yale.

Netanyahu alikabana koo na aliyekuwa mkuu wa majeshi, Jenerali Benny Gantz, ambaye hadi sasa amesita kushiriki serikali ya pamoja na Netanyahu.

Kukosekana kwa serikali kamili, Netanyahu akiwa kaimu waziri mkuu, ni tatizo jeshini.

Tatizo ni kuwa hali ya usalama wa Israel inaonekana kuingia mazingira magumu zaidi kutokana na maadui zake pande zote wakiwa na nguvu zaidi kuliko awali.

Kwa mfano Hamas sasa wanafaulu kurusha maroketi kwa wiki mara moja au mbili ndani ya Israel, ingawa siyo kila siku inaleta majeruhi.

Kwa upande mwingine kundi la Hezbollah nchini Lebanon limejizatiti zaidi na lina nguvu kuliko Hamas, hata kulifanya jeshi la Israel kuwa na wakati mgumu kugundua mahandaki wanayochimba chini ya eneo la mpaka kupenya ndani ya Israel bila kugundulika.

Wakifualu kukamilisha handaki na kuingiza kundi la wapiganaji wa kujitolea mhanga inaweza kuwa balaa kwa Israel na kuvuruga uongozi wa nchi, jeshi.

Mabadiliko katika maeneo mengine pia yanaleta wasiwasi kwa wakuu wa majeshi ya Israel, ikiwa ni pamoja na kuimarika kwa nguvu za Iran huko Iraq na maeneo ya Ghuba, na hata kufikiwa kwa ushirikiano wa karibu zaidi kati ya Iran, Uturuki na Russia, ingawa lengo lao kubwa ni hali ya Syria.

Hali ya kimkakati inaonekana kuwa ni ngumu lakini inahitaji tafsiri ya kisiasa ya utawala ulioko madarakani, lakini Netanyahu ana matatizo siyo katika uchaguzi mkuu tu ila hata kisheria, kwani uwezekano wa kufikishwa mahakamani unaongezeka, hasa akishindwa kuunda serikali mpya. Ni eneo la utelezi mkali.

Kuunda serikali yenye viti zaidi ya 60 bungeni imekuwa tatizo kwani kiongozi mmoja wa mrengo wa kulia (upande wa Netanyahu), Avigdor Lieberman, amekataa kuunga mkono serikali inayoongozwa na Netanyahu, na kwa vile hawezi kuunda serikali na Jenerali Gantz, anataka Netanyahu na Gantz waunde serikali, wakati Gantz hataki kukaa katika serikali moja na Netanyahu.

Vyama vya kisiasa vya raia wa Kiarabu vilimuunga mkono Gantz, lakini bila kupata chama angalau kimoja cha mrengo wa kulia, Gantz hawezi kuunda serikali yenye mrengo wa kushoto na msaada wa mrengo wa kulia. Ni mkwamo ambao wachambuzi wa habari hawajui utaisha vipi, na Rais Reuven Rivlin amechoshwa na kurudiwa uchaguzi.

Netanyahu ana kesi mbili ambazo zinamsumbua, moja ikiwa inahusiana na rushwa katika shauri linaloitwa la Bezeq-Walla, na nyingine ni zawadi zenye harufu ya rushwa, yaani zisizo halali, kesi zinazotajwa kwa namba za kiusalama kama kesi namba 400 na kesi namba 1000.

Licha ya kuwa kesi hizi zimemdhoofisha kiasi fulani Netanyahu, bado karibu nusu ya wapiga kura wana imani naye au na vyama ambavyo vinamuunga mkono, na kwa jumla ameonekana ana uwezo mkubwa zaidi wa kufikia muafaka wa kuunda serikali.

Tatizo kwa upande wake ni baadhi ya wanasiasa kutotaka kushirikiana naye moja kwa moja kutokana na kashfa hizo, wasijivurugie.

Wakuu wa ulinzi na usalama walikuwa na mkutano wa kujadili hali ya usalama nchini humo, ambako hapakuwa na jambo kubwa lililotangazwa, kwani kaimu waziri mkuu hawezi kusukuma ajenda muhimu.

Jeshi linaendelea kufuatilia mikakati iliyokubaliwa awali, ambayo ni pamoja na kuwa huru kushambulia vituo vyovyote vya kijeshi vya Iran katika nchi zinazopakana na Israel, na vituo kama hivyo vimepigwa nchini Syria mara kwa mara, na hata Iraq, kuacha Lebanon.

Baadhi ya wanasiasa wa Likud walikuwa wanajaribu kupandisha utambi kuhusu hali ya kiusalama lakini jeshi la Israel limekuwa likijitenga na matamshi hayo, kuwa ni propaganda.

Hisia za Luteni-Jenerali Kochavi kuhusu hali ya usalama wa nchi hiyo zilionekana pia katika salamu alizomtumia mkuu mpya wa majeshi ya Marekani, Jenerali Mark Milley aliyezungumza naye kwa simu Jumatano iliyopita.

Taarifa zilisema makamanda hao wawili wanafahamiana kwa undani kutokana na kushirikiana katika nafasi zao zilizotangulia na kwa hiyo wana uelewa ambao unafanana katika maeneo tofauti ya suala pana la usalama Mashariki ya Kati.

Ilileta hisia kwa baadhi ya wachunguzi wa habari kuwa uelewano huo ni ishara kuwa wakati utawala wa Trump ulishindwa kutoa jibu medani ya mafuta ya Saudia ilipopigwa, Israel ni suala jingine.

Taarifa iliyotolewa na ofisi ya Jenerali Milley ilisema kuwa wakuu hao waliongelea kwa haraka masuala yanayowahusu pamoja, na kukubaliana kukutana wakati ujao, ambako Jenerali Milley aliyakinisha dhamira ya Marekani kuendelea na uhusiano wa karibu na Israel. Taarifa ilisema kuwa Israel na Marekani zina mahusiano ya dhati katika ngazi ya jeshi na jeshi, uhusiano ambao ni muhimu katika kuhakikisha amani na usalama eneo la Mashariki ya Kati.

Ni kama kusema kuwa mapungufu ya Marekani kuhusu Iran pale inaposhambulia meli katika Ghuba ya Uajemi, kupiga ndege isiyo na rubani ya Marekani au hata kupiga medani ya mafuta Saudia isidhaniwe kuwa ndiyo hali halisi ya Marekani.

Ni kujua kuwa iko mipaka; vitendo hivyo havijaifikia bado, lakini endapo hatari kwa Israel itafikia kiwango cha kuleta wasiwasi, Marekani itakuwa tofauti.





# Waingia mitaani kuhamasisha uandikishaji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATENDAJI wa serikali jijini Mbeya wameingia mitaani huhamasisha wananchi kujiandikisha baada ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, kuongeza siku tatu za wananchi kujiandikisha ili kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, James Kasusura, juzi aliingia mitaani na alikuwa anatembelea 'vijiwe' vya waendesha pikipiki, maarufu kama 'bodaboda' na wapigadebe wa stendi kuu akiwahamasisha vijana kwenda kujiandikisha.

Alilitaka kundi la waendesha bodaboda kufuata sheria ili kuwafunga midomo watu wenye fikira kuwa kundi hilo ni kundi la wahuni na badala yake kazi hiyo ionekane kama kazi zingine.

Kasusura aliwataka vijana kwenda kujiandikisha ili wawe na sifa za kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba 24, mwaka huu na kuchagua viongozi ambao watawasaidia kuleta maendeleo.

Alisema watu wanaotakiwa kujiandikisha kushiriki uchaguzi huo ni wale wenye umri wa miaka 18 na kuendelea, wakazi wa mitaa husika bila kujali itikadi za vyama vyao.

"Msiishie kulalamikia maendeleo kuwa hayaji na badala yake hakikisheni mnajiandikisha ili kuwa na uhalali wa kuwachagua viongozi watakaowaletea maendeleo kwenye maeneo yenu," alisema Kasusura.

Aliwataka kuwapuuza watu wote wanaowapotosha kuwa ili ushiriki uchaguzi huo ni lazima uwe na kitambulisho cha mpigakura kitu ambacho alisema ni uongo.

Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Madereva Bodaboda wa Stendi Kuu, Augustino Mwamanda, alisema kwa sasa asilimia kubwa ya wanachama wao wamejiandikisha na sasa wanaendelea kuhamasisha waliobaki.

Alisema watahakikisha mpaka siku ya mwisho wanachama wote wanajiandikisha na wanashiriki kuchagua viongozi wa mitaa yao na kwamba wanafahamu kuwa hiyo ni haki yao ya kikatiba.

Mwamanda alisema kwa sasa wanachama wa chama hicho pia wanaelekezana mambo mbalimbali ikiwemo kuzingatia sheria katika utendaji kazi ili kuepuka migogoro na serikali.

"Sisi tangu mwanzo tulikuwa tunahamasishana ndiyo maana wengi tumejiandikisha, lakini hatutaishia hapa kwani tutaendelea kuhamasishana kwenda kupiga kura," alisema Mwamanda.

Baadhi ya mawakala wanaowakilisha vyama vya siasa walisema baada ya serikali kuongeza siku za kuandikisha, wananchi wameendelea kujitokeza na kwamba kasi hiyo ikiendelea kuna uwezekano mkoa wa Mbeya ukaendelea kuwa miongoni mwa mikoa inayofanya vizuri.

Mmoja wa mawakala hao, Grace Lamson, kutoka Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika eneo la Forest alisema uandikishaji huo unaenda vizuri katika eneo hilo.



Mbunge wa Jimbo la Isimani ambaye ni Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, akisubiri kujiandikisha katika daftari la wapigakura la uchaguzi wa viongozi wa Serikali za Vijiji na Mitaa katika kituo cha Msimbo kilichopo Tarafa ya Idodi mkoani Iringa jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wapongeza ufadhili mabaraza ya biashara

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WADAU wa biashara mkoani Mbeya, wamelishukuru Shirika la Maendeleo la Uholanzi (SNV) kwa kuanzisha utaratibu wa kushirikiana na serikali kuboresha utendaji kazi wa mabaraza ya biashara mkoani hapa.

Kwa mujibu wa wadau hao, utaratibu huo utasaidia kutatua mapema changamoto zinazowakabili.

Kauli hiyo waliitoa juzi wakati wa mkutano wa wadau wa mabaraza ya biashara kutoka katika wilaya zote za Mkoa wa Mbeya wakiwamo watendaji wa serikali, sekta binafsi na maofisa wa SNV wanaotekeleza mradi wa uboreshaji wa mfumo wa masoko ya maziwa na alizeti.

Ofisa Biashara wa Mkoa wa Mbeya, Stanley Kibakaya, alisema mabaraza ya biashara yamekuwa yakikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo ukata hali ambayo huyafanya wakati mwingine yasifanye majadiliano kwa mujibu wa sheria.

Alisema baadhi ya wajumbe wanaochaguliwa kwenye mabaraza hayo, hawana uwezo wa kutosha kuwezesha ufanisi wa kujadili hoja na badala yake huwa wanaishia kulalamikia serikali kutotekeleza baadhi ya mambo.

Kibakaya alisema baada ya kubaini changamoto hizo, waliiandikia SNV barua kuomba kusaidia kuboresha mabaraza hayo na hatimaye kuridhia.

"Mheshimiwa Rais alipokutana na wafanyabiashara Ikulu jijini Dar es salaam, baadhi yao walitoa malalamiko ambayo yalitakiwa yatolewe kwenye mabaraza na kupatiwa ufumbuzi huko huko. Walifikisha malalamiko yao huko kwa sababu mabaraza wakati mwingine hayafanyiki," alisema Kibakaya. Naye Ofisa Mtendaji wa Chemba ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Kilimo (TCCIA) Mkoa wa Mbeya, Emile Malinza, alisema changamoto kubwa inayoyakabili mabaraza hayo katika ngazi ya mkoa na wilaya ni fedha za uendeshaji kwa madai kuwa serikali huwa haina bajeti kwa ajili ya shughuli hizo.

Alisema wamewahi kukubaliana kufanya zamu kugharimia mabaraza hayo kati ya sekta ya umma na sekta binafsi lakini walikwama kutokana na mamlaka za serikali za mitaa kutokuwa na mtiririko mzuri wa fedha.

Malinza alisema kama mabaraza hayafanyiki, changamoto zinazokwamisha sekta ya biashara hazitatuliwi kwa wakati, hivyo sekta hiyo kushindwa kukua kwa kasi inayostahili.

"Kukua kwa sekta ya biashara kunategemea sana majadiliano ya mabaraza ya biashara. Mabaraza yasipofanyika changamoto za wafanyabiashara hazitatuliwi kwa wakati mwafaka," alisema Malinza.

Mshauri wa Masuala ya Sera katika Mradi wa Maziwa na Alizeti (TAM), Renatus Mbamilo, alisema shirika hilo liliamua kuanza kushirikiana na serikali kuboresha mabaraza hayo baada ya kupokea barua kutoka katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ikiwaomba kufanya hivyo.

Alisema shirika hilo linatekeleza mradi huo chini ya ufadhili wa Shirika la Msaada la Watu wa Uingereza (UK AID) ambalo fedha zake zinasimamiwa na Shirika la KPMG- Tanzania.

# Wananchi hatarini kukosa mawasiliano

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ZAIDI ya wananchi 3,000 wa Kata ya Ikukwa wilayani Mbeya, wako hatarini kukosa mawasiliano ya barabara baada ya daraja linalounganisha kata hiyo na Wilaya za Songwe, Chunya na Mbeya kupata nyufa kubwa zinazoashiria kuwa linaweza kuvunjika wakati wowote.

Kutokana na hali hiyo, baadhi ya madereva wanalazimika kulikwepa na kupita pembeni katika kipindi hiki ambacho mvua hazijaanza kunyesha, lakini endapo mvua zitanyesha hakutakuwapo na njia mbadala isipokuwa kwenye daraja hilo.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Ikukwa, Jostan Mwavileka, alisema daraja hilo likivunjika hali ya maisha kwa wananchi wa eneo hilo itakuwa ngumu kwa vile barabara hiyo ndiyo pekee inayoingia na kutoka kwenye kata hiyo.

Aliiomba serikali kuwajengea daraja hilo kabla ya msimu wa mvua kuanza akidai kuwa mbali na kuathiri maisha ya wananchi pia wagonjwa na wajawazito nao hawatasafiri kufuata huduma za afya mjini.

"Tunaiomba serikali iuone umuhimu wa daraja hili kwa maisha ya wananchi wanaoishi huku, itujengee kabla ya mvua hazijaanza maana endapo ikinyesha na likasombwa na maji sisi tutakuwa na wakati mgumu sana," alisema Mwavileka.

Baadhi ya wananchi hasa kinamama walisema kuwa mbali na daraja hilo kutishia kukatika mawasiliano, pia barabara hiyo inahitaji matengenezo ili kupitika kirahisi.

Yalipa Mwasipa, mkazi wa Kata ya Ikukwa alisema barabara hiyo ina mashimo makubwa ambayo yanasababisha wagonjwa na wajawazito wanaopewa rufani kwenye zahanati yao ili wakatibiwe kwenye hospitali kubwa mjini Mbeya wasafiri kwa taabu.

Mbunge wa Mbeya Vijijini, Oran Njeza, alisema barabara hiyo ni muhimu kwa maisha ya wananchi wa eneo hilo na kiuchumi kwa vile inaunganisha wilaya za Songwe, Mbeya na Chunya.

Alisema analichukua suala hilo na kulifanyia kazi ambapo aliahidi kuwasiliana na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura) ili wachukue hatua za dharura za kujenga daraja hilo.





# Vituo vya zimamoto kujengwa halmashauri

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Zimamoto na Uokoaji nchini limeanza ujenzi wa vituo vya zimamoto kwenye halmashauri za mikoa mbalimbali nchini ili kuimarisha utendaji kazi zake katika sekta hiyo.

Hayo yalibainishwa na Kamishna wa Fedha na Utawala wa jeshi hilo, Baraka Semwanza, wakati akizungumzia kuhusiana na maboresho ya vituo na magari mitambo ya kuzimia moto yanayofanywa na jeshi hilo.

Alisema ujenzi huo unatarajia kuanza wakati wowote kuanzia sasa katika maeneo ya Chato, Mbinga na Kilolo mkoani Iringa, huku eneo la Manyoni mkoani Singida, Namtumbo na Ilemela mkoani Mwanza.

Kamishna Semwanza alisema moja ya vitu ambavyo jeshi hilo linatoa kipaumbele ni ujenzi wa vituo hivyo ambao wanaamini vikikamilika kila mahali itakuwa imewarahisishia kwa kiasi kikubwa kufanya kazi zake kiufasaha pale majanga ya moto yanapotokea.

"Tunafanya maboresho ya vituo pamoja magari mitambo ya kuzimia moto tunahitaji kuona sekta hii inaimarika na kufanya kazi kiufanisi katika jamii inayotuzunguka," alisema Kamishna Semwanza.

Alisema lengo ni kuona kila halmashauri inajitegemea katika utendaji kazi za jeshi hilo ili kusiwe na visingizio vyovyote pale panatokea majanga ya moto katika sehemu mbalimbali.

Mbali na hilo alisema jeshi hilo litaendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya kujikinga na majanga ya moto pale yanapotokea katika maeneo mbalimbali hapa nchini ikiwamo matumizi sahihi ya vizima moto.

Kamishna huyo pia alisema jeshi hilo linawaasa wananchi kuzingatia misingi ya maelekezo ya elimu inayotolewa na jeshi hilo katika taasisi, shuleni, vituo vya mabasi na sehemu mbalimbali.

Alisema lengo la kufanya hivyo ni kutaka wananchi kupata uwelewa juu ya kujikinga na majanga ya moto pale yanapotokea ikiwamo kujua matumizi ya kifaa cha kuzimia moto.



Diwani wa Kata ya Kilimani jijini Dodoma, Neema Chiwanga (kushoto), akijiandikisha jana kwenye daftari la wapigakura wa uchaguzi wa serikali za mitaa kituo cha Nyerere, kulia ni mwandikishaji wa kituo hicho, Tishio Kipingi. **PICHA NA IBRAHIM JOSEPH**

# Watoto mazingira magumu waomba msaada

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

SERIKALI na wadau mbalimbali wameombwa kuwasaidia kuwajengea majengo watoto 68 wanaoishi mazingira magumu ambao wanaolelewa katika kituo cha yatima cha Shirika la Malezi endelevu (SHIME) kilichopo Dodoma Makulu. Wameomba msaada huo kutokana na nyumba waliyokuwa wakiishi kutakiwa kuondoka.

Ombi hilo lilitolewa jana na watoto wa kituo hicho wakati wakizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma wakati wakieleza changamoto walizonanzo.

Akizungumza kwa niaba ya wenzake Andrea George, alisema wanalazimika kuomba kwa serikali na wafadhili kutokana na mmiliki wa nyumba hiyo waliyokuwa wakiitumia awali kuwapa miezi mitatu kuwa wameondoka.

"Ndugu zetu wanahabari kwa kupitia kwenye vyombo vyenu vya habari tunaiomba serikaki yetu sikivu wakiwamo watu binafsi na mashirika yasiyo ya kiserikali kutusaidia fedha, ili tuweze kupata eneo litakalotuwezesha kujenga kituo chetu ili tuendelee kupewa huduma mbalimbali ikiwamo ya elimu," alisema. Aidha, aliwaomba wadau waliokuwa wanajitokeza kuwapa misaada wakiwamo wabunge waendelee kuwasaidia ili waendele kupatiwa malezi bora yanayotolewa kituoni hapo. Naye Mary Willson, mlezi wa kituo hicho akizungumza kwa niaba ya wazazi, alisema kuna hatari ya kuwapoteza watoto hao ikiwa juhudi za haraka hazitachukuliwa kwa ajili ya kujenga kituo hicho. Alisema idadi ya watoto wanaolelewa ni wengi na kituo kimekuwa kikiwahudumia kwa misaada mbalimbali kama ya kiafya, kielimu, mavazi na chakula.

Mkurugenzi wa kituo hicho, Zawadi Mgeni, alisema jengo hilo walilokuwa wakilitumia awali walisaidiwa na mmiliki huyo kama sehemu ya kuwahifadhi.

Alisema kituo hicho kilianzishwa mwaka 2012 na walikabidhiwa ili waweze kuwahudumia watoto hao ambao wanaotoka karibu kata tatu ikiwamo ya Makole, Tambukareli na Dodoma Makulu.

Ni kweli tunatakiwa kuondoka ili kumpisha mmiliki mwenyewe kwa ajili ya kuishi, hivyo tunaiomba serikali, taasisi, mashirika na wadau wanaotusaidia kutuwezesha kifedha ili tuweze kupata eneo ambalo tutakalojenga kituo na kiasi kinachohitajika ni Sh. milioni 200," alisema.

## Rushwa mitaa yaibua Takukuru

**Na Renatha Msungu,**

DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani Dodoma, imesema imejipanga kuhakikisha inatokomeza rushwa serikali za mitaa kutokana na eneo hilo kuongoza kwa vitendo hivyo.

Akizungumza na Nipashe jana Mkuu wa Takukuru mkoani hapa, Sosthenes Kibwengo, alisema katika taarifa ya robo ya mwaka huu wa fedha Julai hadi Septemba 2019, inaonyesha vitendo vya rushwa kwenye kata, mitaa na vijijini asilimia 39.4.

Alieleza kutokana na hali hiyo, Takukuru imejipanga kutoa elimu ya kutosha hasa wakati huu wa uchaguzi wa serikali za mitaa, ili kutokomeza rushwa maeneo hayo.

Alisema wanaendelea kutoa elimu kwa wananchi kupitia klabu hizo ambazo zimeanzishwa katika wilaya na kata tofauti ili kuhakikisha wananchi wa vijijini na mijini wanaelewa nini maana ya rushwa.

"Tunahitaji kuona asilimia hiyo inatoweka kabisa ndio maana hatusiti kuendelea kutoa elimu kwa wananchi dhidi ya mapambano ya rushwa," alisema Kibwengo.

Alisema klabu hizo zimekuwa msaada mkubwa kwa wananchi kwa sababu zinasaidia kutoa elimu hiyo kwa wakazi katika mitaa na vijiji mbalimbali kutokana, na kwamba wengi wao walikuwa hawana uwelewa mkubwa wa madhara ya utoaji na upokeaji rushwa.

Kibwengo alisema klabu hizo zimekuwa msaada mkubwa kwa wakazi wa maeneo tofauti hapa jijini kwa kuwa zimekuwa zikitoa elimu hiyo kupitia jumbe mbalimbali katika mikusanyiko ikiwamo mikutano na makongamano.

"Takukuru tunaendelea kutoa elimu kwa wananchi lengo ni kuona kila mmoja anaelewa nini madhara ya rushwa kwa jamii," alisema Kibwengo.

Pamoja na hayo, alisema kutokana na serikali kuwekeza fedha nyingi katika miradi wanayotekeleza, wananchi wanapaswa kuchagua viongozi wenye weledi ambao watakuwa chachu kubwa ya kufanya maendeleo ya kata, mitaa na vijiji kupitia miradi ya serikali.

Alisema miradi ya maendeleo inayotekelezwa na serikali ni mali yao, hivyo ni vema wajipambanue na kuchagua viongozi waadilifu wasiopenda rushwa.





## Zawa yaahidi mita wateja wa nyumbani

**Na Abdallah,** ZANZIBAR

MAMLAKA ya Maji Zanzibar (Zawa), imeahidi kuwa ifikapo mwaka 2020 inatarajia asilimia kubwa ya wateja wa Zanzibar na Pemba hasa wa nyumbani, itakuwa imewafungia mita za maji.

Ofisa Uhusiano wa Zawa, Zahoro Suleiman, alisema hayo wakati akizungumza na Nipashe jana mjini Zanzibar.

Alisema kwa mwaka huo wanatarajia kufikia asilimia 70 ya kufunga mita hizo za maji hasa nyumbani kwa wateja wa maeneo ya mijini ambayo kwa asilimia kubwa wanatumia maji kutoka mamlaka hiyo, ikilinganishwa na maeneo mengine ambayo wananchi wamechimba visima.

Alisema kwa hivi sasa tayari wamekamilisha kufunga mita hizo kwa asilimia 20 katika maeneo mengi ya Mkoa wa Mjini Magharibi, Wilaya ya Kaskazini A pamoja na Wilaya ya Kusini kwa wateja wa nyumbani.

"Matarajio yetu ni kuona kuwa angalau asilimia 70 mwakani tunawafungia mita hizo kwa watumiaji wa nyumbani ikilinganishwa na hivi sasa. Mita hizi zinasaidia kuwaleta karibu watumiaji wa maji ili kuchangia huduma hii kwa wakati," alisema.

Aidha, alisema kwa hivi sasa tayari wamefanikiwa kwa asilimia 90 kufunga mita hizo katika maeneo ya biashara kama vile mahoteli makubwa, migahawa mikubwa pamoja na baadhi ya viwanda na wateja wakubwa.

Hata hivyo, alisema kazi hiyo inafanyika kwa mafanikio makubwa kutokana na ushirikiano wanaoupata kutoka kwa masheha na wananchi wa maeneo husika, pindi wanapokwenda kufunga mita hizo.

# Ushirikina chanzo ongezeko la ukoma

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia mpango wa kutokomeza ukoma, imeonya kuwa tatizo la ukoma linachangiwa na watu kuhusisha ugonjwa huo na ushirikiana.

Aidha, imesema inatoa mafunzo na uhamasishaji kwa wananchi wa vijijini ili kuwaongezea ufahamu na tahadhari dhidi ya maradhi hayo.

Akizungumza na Nipashe, Mkuu wa Taaluma wa Kitengo cha Kifua Kikuu, Ukimwi, Ukoma pamoja na homa ya ini, Dk. Hasnuu Fakih Hassan, alisema kupitia mpango huo wahudumu wa afya wanatembea katika maeneo mbalimbali ya vijijini Unguja na Pemba ili kuwabaini wagonjwa hao na kupatiwa matibabu.

Alisema kesi za maradhi ya ukoma hasa katika kisiwa cha Pemba ni nyingi, ila changamoto iliyopo ni baadhi ya wananchi kuhusisha ugonjwa huo na ushirikiana.

Alisema jambo hilo husababisha hata wanapogundulika na wataalamu hao wa afya wanaotembelea vijijini wengi wao wanakuwa tayari wameshaumia na ugonjwa huo umeenea kwa kiasi kikubwa.

"Watu wanaoumwa ukoma wapo Pemba na hata Unguja lakini bado jamii wanauhusisha na mambo ya kishirikiana. Kwa hiyo wagonjwa wengi hukimbilia kwa waganga badala ya kuja hospitali kupata tiba. Serikali inatoa fedha kwa ajili ya ugonjwa huo sisi tunawataka waje hospitalini ili watibiwe," alisema Hassan.

Aidha, alisema ugonjwa huo wa ukoma unapelekea ulemavu wa kudumu kutokana na kushambulia na kumaliza kiungo kimoja kimoja cha mwili hivyo wananchi wayachukulie maradhi hayo kama ugonjwa hatari na watafute elimu na ufahamu wanayopewa na wataalamu wa afya.

Alisema kuwa katika miezi ya Aprili na Juni wagonjwa 10 wa ukoma waligunduliwa na wahudumu wa afya. Waliwagundua katika maeneo ya Kaskazini na Kusini Pemba huku wagonjwa hao wakiwa wanaendelea kupatiwa matibabu bure hospitalini.

Hata hivyo aliwataka wananchi kuacha kuingiza imani potu kuhusu ugonjwa wa ukoma na badala yake wafuate maelekezo kutoka kwa wataalamu wa afya kwani ugonjwa huo unaambukiza pale inapofikia hatua ya mwisho.

Aidha, pia wanawaelimisha wananchi kuhusu maradhi hayo na jinsi ya kuyatibu na kujihadhari.

Alisema kutokana na kutokuwa na fedha za kukabiliana na changamoto za magonjwa hayo, serikali imekuwa ikitoa fedha kila baada ya muda fulani ili kuwatibu wagojwa hao wa ukoma kama ilivyo wagonjwa wengine.



Wafanyabiashara katika Soko la Buguruni Dar es Salaam wakishusha machungwa kwenye gari kwa ajili ya kuwauzia wateja jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wazazi wapewa tiba wabakaji watoto wao

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WIZARA ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, imewataka wazazi na walezi kuwa karibu na watoto wao, ili kujua nyendo zao kwa lengo la kuwakinga na kuwaepusha na vitendo vya udhalilishaji.

Mohammed Jabir, Ofisa wa Wizara hiyo, aliyasema hayo huko Chuini Wilaya ya Magharibi A, katika mkutano ulioandaliwa na sheha wa shehia hiyo kwa lengo la kuwapatia elimu wananchi kuhusu namna ya kupambana na vitendo vya udhalilishaji na ukatili kwa wanawake na watoto.

Alisema wazazi wanapaswa kuwa karibu na watoto wao katika mazingira yoyote kuanzia shuleni (skulini) na mitaani kujua maeneo anayocheza na hata katika madrasa kwani vitendo vya ubakaji na udhalilishaji hutokea katika mazingira tofauti.

Alisema kuwa katika kukabiliana na vitendo hivyo si busara wazazi kuwaachia polisi au maofisa wanawake pekee bali jitihada za makusudi zinahitaji katika kuhakikisha vitendo hivi vinapunguzwa au kutokomezwa nchini.

Alisema wapo baadhi ya wazazi wako mbali na watoto wao, bila kujua kuwa jukumu la ulezi ni wao na si kuwaachia wafanyakazi wa ndani peke e.

Alisema jambo hilo ni hatari katika maisha haya ya sasa yaliyojaa vitendo vya udhalilishaji ikiwamo vya ubakaji na hata ulawiti kwa watoto wa kike na wakiume.

Ofisa wanawake na watoto wilaya ya Magharibi A, Sabra Mgeni, aliwataka walimu wa vyuo vya madrasa kuwa na kamati maalum katika wilaya hiyo kuratibu na kujua wageni na wenyeji watakaoingia kuanzisha madrasa katika maeneo yao.

Alisema kuwa wapo baadhi ya walimu wa madrasa ambao hawana imani ya dini wala hawana utu ambao, wanajihusisha na kufanya ukatili na ulawiti kwa watoto wadogo.

Alisema jambo hilo halikubaliki na linapaswa kukemewa kwa nguvu zote na kwa sasa kwa kiasi kikubwa hasa kwa kuwa taifa lina mpango mkakati wa kutokomeza tatizo hilo.

Alisema ni vyema kuanzia sasa ofisi ya Mufti wa Zanzibar, ikawatambua walimu wote wa madrasa waliopo kila wilaya ili iwe njia moja wapo ya kumaliza au kupunguza tatizo la ulawiti na ubakaji wa watoto katika baadhi ya vyuo vya madrasa hapa nchini.

# CAAT kuwavutia Wachina kuwekeza

Na Enok Charles

JUMUIYA ya Watanzania waliosoma nchini China (CAAT), imeazimia kuwa kiunganishi kati ya Tanzania na China, kushawishi wawekezaji kutoka China kuja nchini na kukuza biashara kati nchi mbili hizo.

Lengo ni kuendeleza azma ya Serikali ya kufikia uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025.

Akizungumza wakati wa kufunga mkutano mkutano wa mwaka wa CAAT, Mwenyekiti wa CAAT, Liggyle Vumilia, alisema kazi kubwa ya CAAT, wanachama wake na watu walipata kuishi China ni kuunganisha Watanzania na fursa za uwekezaji zilizoko China ili kukuza biashara kati ya nchi mbili hizo.

Mkutano huo umewawezesha wataalamu wa Tanzania waliosoma China kujadili fursa za biashara na uwekezaji kati ya nchi mbili hizo. "Fursa za biashara kati ya Tanzania na China ni nyingi, hivyo ni jukumu letu kutumia elimu na maarifa tuliyopata katika kuainisha fursa na kuzifanyia kazi ili kujijenga kiuchumi, na kupunguza tatizo ajira," alieleza Vumilia.

Aliongeza kuwa maendeleo ya Tanzania yataletwa na Watanzania kwa kushirikiana, kutambua fursa, kuzifanyia kazi ili kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla, hasa kwa wataalum walisoma nje kuleta uzoefu wao Tanzania.

"Nafasi tuliyonayo kama wasomi ni kuchochea maendeleo ya nchi kwa kuleta uzoefu,maarifa na teknolojia kutoka katika mataifa ya nje ili visaidie kujenga uchumi wa viwanda na kuifanya nchi kupiga hatua kimaendeleo," alisema Vumilia

Balozi wa China nchini, Wang Ke, aliipongeza jumuiya hiyo kwa kuendeleza ushirikiano uloasisiwa na Mwalimu Julius K. Nyerere pamoja na Mao ze Dong na kuisihi jumuiuya iendelee kutumia fursa zilizopo ili kuzinufaisha nchi mbili hizo.

Balozi mstaafu wa Tanzania nchini China, Luteni Jenerali msataafu Abdulrahman Shimbo, alisema:

"Jumuiya hii itawaleta pamoja wanahitimu wote waliosoma China na kujadili changamoto na fursa zilizopo na kuleta mawazo mapya yatakayosaidia kuongeza biashara na uwekezaji kati ya China na Tanzania."




Meneja Huduma Bora wa NBC, Jane Dogani, akikabidhi zawadi kwa baadhi ya watoto wa wateja wa benki hiyo katika hafla ambayo NBC iliwaandalia watoto hao ikiwa ni sehemu ya matukio ya benki hiyo kuadhimisha mwezi wa huduma kwa wateja. Hafla hiyo ilifanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wito wazazi kuwafungulia watoto wao akaunti ya elimu

Na Mwandishi Wetu

Wazazi nchini wameshauriwa kufungua akaunti maalim ya watoto ili kuwapa uhakika wa elimu wawapo hai au wasipokuwapo.

Ushauri huo umetolewa na Benki ya NBC), ikiwataka kufungua akainti ya Chanua pamoja na bima ya elimu ya Educare za benki hiyo.

Wito huo ulitolewa jijini Dar es Salaam na Kaimu Mkurugenzi wa Wateja Binafsi wa benki hiyo, Benjamin Nkaka, katika hafla waliyoiandaa kwa ajili ya watoto wa wateja wao ikiwa ni sehemu ya matukio ya kuadhimisha Mwezi wa huduma kwa wateja wa NBC.

Alisema akaunti ya watoto ya Chanua ya NBC pamoja na bima ya elimu ya educare vitamuwezesha mzazi kuanza kuwekeza kidogodogo kwa ajili ya mtoto wake hivyo kuondoa hofu ya watoto kupata elimu bora pindi mzazi anapoondoka duniani.

"Akaunti ya Chanua na bima ya Educare za NBC ni suluhisho la uhakika kwa elimu ya watoto, wakati mzazi awapo duniani,asipokuwepo au atakapotapa ulemavu wa kudumu, nawashauri wazazi kuwafungulia watoto wenu akaunti hii na kuanza kuwekeza pamoja na bima ya educare zote kutoka NBC," alisema.

# Ziara ya Rais Magufuli Katavi yawaibua UVCCM

**Na Gurian Adolf,** KATAVI

JUMUIYA ya Vijana wa CCM (UVCCM) mkoa wa Katavi, imemshukuru Rais John Magufuli kwa kufanya ziara ambayo imewezesha mkoa huo kupata miradi mipya ya maendeleo.

Baadhi ya mambo hayo ni ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami zenye urefu wa kilometa 120 ambazo ni za Kibaoni-Sitalike na Vikonge-Uvinza pamoja na kiwanda cha kuchambua pamba.

Pongezi hizo zilitolewa jana na Mwenyekiti wa UVCCM wa mkoa huo, Theonas Kinyonto, alipokuwa akizungumza na wandishi wa habari juu ya mafanikio ya ziara ya Rais katika mkoa huo aliyoifanya hivi karibuni. Alisema ziara hiyo imekuwa na mafanikio kwa wakazi wa mkoa huo kwani wameweza kukupatiwa miradi mipya ambayo haikuwapo awali. Kinyonto alisema katika ziara hiyo Rais Magufuli aliiagiza Wizara ya ujenzi uchukuzi na mawasiliano kuanza mara moja mchakato wa ujezi wa barabara kwa kiwango cha lami yenye urefu wa kilometa 71 kutoka Kibaoni hadi Sitalike kwenda Mpanda mjini. Aliitaja barabara nyingine ni ya kutoka Vikonge Wilaya Tanganyika kuelekea Uvinza ambayo itangenezwa kwa kiwango cha lami kwa kilometa 50 awali barabara hiyo ilikuwa imetengenezwa kwa kilometa 35 kutoka Mpanda mjini hadi Vikonge.

Alisema mradi mwingine mpya ni wa ujenzi wa kiwanda cha kuchambua pamba ambapo alitoa kiasi cha shilingi bilioni 1.6 kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda hicho.

Pia aliiagiza Wizara ya Mifugo na Uvuvi kujenga kiwanda cha samaki katika eneo la mji wa Karema katika mwambao wa ziwa Tanganyika na kuzindua kwa mara ya kwanza safari za ndege za Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) ambazo zimeanza safari za kutoka Dar es Salaam, Tabora hadi Mpanda mkoani Katavi.

**HABARI KIMATAIFA**

# Mzee wa miaka 94 aoa wanawake 19

**KAMPALA,** Uganda

ULE msemo ukistaajabu ya Musa utayaona ya firauni umedhihirika huko Uganda baada ya Mzee Nulu Ssemakula (94) kutoka kijiji cha Ruyonza kuongeza idadi ya wanawake na kufikia 19.

Hatua ya mzee huyo ambayo imewaacha wananchi midomo wazi imekuwa ya kipekee katika kijiji hicho ambacho jamii yake imekuwa na ndoa ya mke zaidi ya mmoja, naye alikua akizingatia sana masuala ya familia na dini.

Ssemakula ni muislamu wa kwanza kutoka kijiji cha Ruyonza kwenda kuhiji Maka mwaka 1977, Gazeti la Daily Monitor la Uganda limeeleza.

Ssemakula anajivunia kuwa na wake 19 ambao wamemzalia watoto zaidi ya 100, mdogo kabisa akiwa na umri wa miezi kumi na mke mdogo kabisa akiwa na miaka 24, ambaye kwa sasa ni mjamzito. Hivi sasa anaishi na watoto wake wadogo 66.

**Ssemakula amejenga msikiti na shule, Shule ya msingi Kiyombero, mashine ya kubangua kahawa na mashine ya kupoza maziwa katika kijiji ili aweze kuhudumia familia yake.**

Wakati baadhi ya watoto wake wana wajukuu, Ssemakula anasema bado ana matumaini ya kuwa na watoto zaidi na hata wake wengi zaidi.

Ssemakula alioa mke wa kwanza mwaka 1952, ambaye baada ya muda mfupi tu akaoa wengine watano. Bado wanaishi pamoja. Daily Monitor limeeleza.

"Kwa bahati mbaya niliwapoteza wake zangu wanne ambao walinihitaji zaidi ya uwezo niliokuwa nao, nikawaacha waende. Lakini waliniacha na watoto. Bado nitaoa tena ikiwa nitaishi miaka mingi zaidi na hata kuwa na watoto wengi zaidi.Ninafurahishwa sana na watoto na wake, ndio utajiri wangu wa kweli," alisema Ssemakula.

Ssemakula amejenga msikiti na shule, Shule ya msingi Kiyombero, mashine ya kubangua kahawa na mashine ya kupoza maziwa katika kijiji ili aweze kuhudumia familia yake.

Akiwa amezungukwa na makazi ya watoto na wajukuu zake, nyumba yake ni kubwa zaidi ikiwa imeezekwa kwa mabati.

Ssemakula huongea huku akiwa na nguvu mithili ya kijana, mcheshi sana kwa wageni, watoto wake na wake zake hucheka sana wanapokuwa wanasikiliza vichekesho vyake ingawa huvisikia mara kwa mara.

"Unapokuwa na wake wengi na watoto wengi, ni kama kuendesha nchi, unapaswa kuomba hekima," alisema Ssemakula.

Alisema changamoto kubwa ambayo ameshawahi kukutana nayo si kuwa na familia kubwa, bali kupoteza mifugo yake katika vita vya waasi mwaka 1979.

Pamoja na kuwa na familia kubwa amemudu kuwasomesha watoto wake, familia yake ina wahandisi, madaktari, wauguzi, maofisa afya, waalimu na wanasheria, wengine wamepitia vyuo vya ufundi huku wengine wakiwa wafanyabiashara. **BBC**



Maofisa wa Tume ya Uchaguzi na vifaa vya uchaguzi wakisafirishwa katika maeneo mbalimbali nchini Msumbiji kwa kujiandaa na Uchaguzi Mkuu. **PICHA: REUTERS**

## Zuma kufikishwa kortini

**JOHANESSBURG,** Afrika Kusini

RAIS wa zamani wa Afrika Kusini, Jacob Zuma, anayeendelea kukabiliwa na kashfa mbalimbali zilizosababisha kung'atuliwa madarakani mwaka 2018, anatarajiwa kupandishwa mahakamani kwa mara ya kwanza.

Zuma anatarajiwa kufikishwa katika Mahakama Kuu ya Pietermaritzburg kuhusiana na rushwa.

Kesi yake inahusiana na rushwa katika kesi ya zamani, miaka 20 iliyopita ya mkataba wa silaha, kesi ambayo inaihusisha kampuni ya Ufaransa Thales.

Zuma, aliyekaa madarakani kuanzia mwaka 2009 hadi mwaka 2018, anashitakiwa kwa kosa la ufisadi, utakatishaji wa fedha na kupitisha mlango wa nyuma pesa kuhusu mkataba mkubwa wa silaha wa Randi bilioni 51 (sawa na Euro bilioni tatu kwa bei ya sasa) mkataba uliotolewa mwaka 1999.

Wakati wa mashitaka dhidi yake, alikuwa waziri katika ngazi ya mkoa na baadaye makamu wa rais.

Anatuhumiwa kuwa alipokea Randi milioni nne (sawa na Euro 249,000 kwa bei ya sasa) kama hongo kutoka kampuni ya Ufaransa ya Thales.

Jacob Zuma na kampuni hiyo inayotengeneza vifaa vya kielektroniki na ulinzi, ambayo pia inakabiliwa na mashitaka hayo, wameendelea kukana mashitaka dhidi yao. **RFI**

# Msumbiji wapiga kura kumchagua rais mpya

**MAPUTO,** Msumbiji

WANANCHI wa Msumbiji jana walipiga kura kumchagua rais na wawakilishi wao watakaowaongoza kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Rais Felipe Nyusi ambaye kwa sasa yupo madarakani anatarajiwa kushinda awamu ya pili ya uongozi.

Mustakabali wa kisiasa wa Msumbiji utajulikana baada ya wapiga kura takriban milioni 13 kupiga kura kuwachagua wawakilishi wao kuanzia Rais, Wabunge na Wawakilishi wa mikoa.

Uchaguzi huo unaonekana kama mtihani kati ya chama tawala nchini humo na upande wa upinzani baada ya kutia saini mkataba wa amani mnamo Agosti kufuatia machafuko ya miaka 15 yalioizonga nchi hiyo na kusababisha vifo vya takriban watu milioni moja.

Rais Nyusi anatarajiwa kupata changamoto kutoka kwa kiongozi wa upinzani Ossufo Momade wa chama cha Renamo, Chama cha Momade kinaonekana kupata umaarufu mkubwa katika siku za hivi karibuni na anatumaini kuwa umaarufu huo huenda ukamsaidia. Mgombea mwengine wa urais ni Meya wa Mji wa Beira, Daviz Simango wa chama cha upinzani cha MDM.

Rais Nyusi ametaka raia wa nchi hiyo kuwa watulivu na kuwatolea wito wa kudumisha amani, ikiwa ni wiki moja tu baada ya idara ya polisi kuthibitisha kuwa baadhi ya polisi wanashukiwa kuhusika na mauaji ya muangalizi maarufu wa uchaguzi Anastacio Matavel.

"Nawatakia kila la kheri raia wa Msumbiji, natumai uchaguzi huu utakwenda vizuri. Na mgombea bora ashinde, mgombea mwenye mawazo bora, ilani bora na mpango bora kwa watu wa Msumbiji. Asanteni", alisema Rais Nyusi.

Mauaji ya Matavel yamelaaniwa vikali na waangalizi wa kimataifa wa uchaguzi na pia yamepandisha joto la kisiasa nchini humo.

Hali hiyo ya hati hati huenda ikawatia hofu baadhi ya wapiga kura ambao huenda wakakosa kujitokeza kutekeleza wajibu muhimu wa kushiriki uchaguzi.

Tume ya uchaguzi nchini humo imevifunga takriban vituo 10 vya kupigia kura katika wilaya ya Kaskazini ya Cabo Delgado kutokana na ukosefu wa usalama. **DW**

# WB kuipatia Tanzania Dola mil. 500 za elimu

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, amefanya mazungumzo na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Dunia anayewakilisha nchi za Afrika, Anne Namara Kabagambe, Mjini Washington DC, Marekani.

Mazungumzo hayo yalilenga katika kubadilishana uzoefu juu ya utekelezaji wa Sera mbalimbali za fedha na namna uchumi wa Dunia unavyoendeshwa.

Katika mazungumzo hayo, baadhi ya miradi ya ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), ujenzi wa bwawa kubwa la kuzalisha umeme la mto Rufiji, mradi wa elimu, na miradi ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), ilijadiliwa.

Dk. Mpango alieleza dhamira ya Serikali ya kuinua kiwango cha elimu, kwa kutafuta fedha zaidi na mikopo ya masharti nafuu ambayo itaelekezwa kwenye elimu.

"Katika Mradi wa Elimu unaotarajiwa kuwasilishwa Benki ya Dunia Novemba, 2019, tunatarajia kupata dola za Marekani milioni 500, na nimemuomba Kabagambe azidi kusisitiza ili Taifa liweze kupata fedha hizi kwa wakati, na tunaamini kwamba fedha hizo zitaidhinishwa na Benki ya Dunia kama tunavyotarajia." alisisitiza Dk. Mpango.

Alisema pamoja na miradi ya elimu, sekta ya nishati ya umeme pia ni muhimu katika kuinua uchumi wa nchi kwa sababu ukipatikana umeme wa kutosha utasaidia kwa vitendo agenda ya uchumi wa viwanda kwa kuongeza thamani ya mazao na kuboresha huduma mbalimbali za kijamii nchini.

Aliiomba Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) zisaidie kwenye miradi mikubwa inayotekelezwa na Serikali hasa katika sekta ya umeme na miundombinu. Aidha Dkt. Mpango alieleza kuwa hivi karibuni Benki ya Dunia iliipatia Tanzania mkopo wenye masharti nafuu wa dola za Marekani milioni 450 kwa ajili ya utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii- TASAF, awamu ya tatu.

"Hivyo kupitia miradi miwili ya Elimu na TASAF, Tanzania inatarajia kupata dola za Marekani milioni 950". Aliongeza Dk. Mpango

Kwa upande wake, Kabagambe alielezea kufurahishwa na utekelezaji wa miradi inayofanyika Tanzania kwani alipata fursa ya kuona miradi mbalimbali ikiwemo SGR na miradi inayotekelezwa na TASAF, na kuelezea kuwa ni miradi ya mfano na kwa nafasi yake ataendelea kuitangaza miradi hiyo ili Tanzania iweze kupata fedha zaidi ya kutekeleza miradi hiyo.

Dk. Mpango anaongoza ujumbe wa Tanzania kwenye Mikutano ya Mwaka ya Benki ya Dunia na IMF ambapo alisema mikutano hiyo ni muhimu kwa kuwa nchi itapata fursa ya kuweza kujadiliana na Taasisi hizi za IMF na WB kuhusu miradi wanayofadhili.




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akisalimiana na Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi, Biashara Ndogo na za Kati wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi, baada ya sherehe za kilele cha Mbio za Mwenge na kumbukizi ya miaka 20 ya kifo cha Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, Mjini Lindi. NMB ilikuwa mmoja ya wadhamini wa mbio za Mwenge. **NA MPIGAPICHA WETU**

## 'Dakika saba' aachiwa huru, alipa mil. 100/-

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Uhujumu Uchumi na Rushwa maarufu kama ya Mafisadi, imemwachia huru Mohammed Yusufali baada kuhukumiwa kulipa fidia ya Sh. milioni 100.

Yusufali alitiwa hatiani kwa makosa ya kukwepa kodi na kuisababishia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) hasara.

Mbali na Yusufali, washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Alloycious Gonzaga na Isaack Kasanga, ambao bado hawajamwandikia barua Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP) ya kukiri makosa hayo.

Hukumu hiyo iliyomwachia huru Yusufali ilisomwa jana na Jaji Lilian Mashaka, baada ya mshtakiwa huyo kutii agizo la Rais John Magufuli la kumwandikia barua DPP ya kuomba msamaha na kukiri makosa yake.

Baada ya mahakama kumtia hatiani, Wakili wa Serikali Mkuu, Pendo Makondo, alidai kuwa, mshtakiwa ni mkosaji kwa mara ya pili kwa kuwa alishatiwa hatiani na mahakama hiyo katika kesi namba 6/2019 kwa makosa ya kuisababishia hasara TRA mapema wiki iliyopita.

Makondo alidai pamoja na adhabu itakayotolewa na mahakama, pia itoe amri ya mshtakiwa kulipa fidia ya Sh. milioni 100.

Kabla ya kutolewa adhabu hiyo mfanyabiashara huyo maarufu kama Dakika Saba wa Magufuli aliomba mahakama isimpe adhabu kali kwa kuwa amezingatia agizo la rais na aliingia makubaliano na DPP kwa hiyari yake.

Mapema mahakamani hapo baada ya kufanyika makubaliano hayo, mshtakiwa huyo aliondolewa mashtaka ya kula njama, kughushi, kufanya biashara bila leseni na utakatishaji fedha na kusomewa mashtaka mawili yakukwepa kulipa kodi nakuisababishia hasara Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Wakili wa Serikali Mkuu, Hashim Ngole, alimsomea maelezo ya awali kwamba pamoja na mambo mengine alidai mshtakiwa akiwa na wenzake ambao ni Gonzaga na Kasanga ni washtakiwa katika kesi hiyo walishirikiana kutenda makosa hayo.

Ilidaiwa mwaka 2010 Yusufali na wenzake hao waliunda mpango wa kufanya biashara isiyo halali ya kukopesha fedha kwa umma na Machi 4, mwaka 2011 walianzisha kampuni iliyoitwa Superial Finacing Solution (SFS) na kuisajili Brella wao wakiwa kama wanahisa na wakurugenzi.

Machi 11, 2011 kampuni hiyo ilipata leseni ya biashara Manispaa ya Kinondoni, iliyowapa mamlaka ya kufanya biashara ya kutoa ushauri wa kifedha kwa manispaa hiyo pekee, ukopeshaji fedha kwa lengo la kupata faida haikuwa miongoni mwa mamlaka waliyopewa.

Ilidaiwa kuwa, mshtakiwa huyo na wenzake walipata Namba ya Usajili ya Mlipakodi (TIN) kutoka TRA Ilala, na kuanza biashara ya ukopeshaji fedha kwa riba Kinondoni tofauti na walikopewa TIN.

## Viwanda kushindana uzalishaji bora bidhaa

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZALISHAJI kutoka viwanda 61 wanatarajiwa kuchuana kuwania tuzo za mzalishaji bora wa bidhaa nchini, kwenye tuzo za Rais za wazalishaji bora viwandani (PMAYA).

Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania (CTI), Perege Gumbo, alisema tuzo hizo zinatarajiwa kufanyika kesho jijini Dar es Salaam, lengo likiwa ni kutambua jukumu na mchango wa sekta ya viwanda katika ujenzi wa uchumi, kuvutia wawekezaji na kuongeza ubora katika shughuli za uzalishaji.

"Mshindi wa jumla atapatikana kwa kuangalia vigezo vingi, mojawapo ni mizani katika utawala kwa kuangalia idadi ya wanawake na wanaume ambapo wanawake wanapaswa kuwa asilimia 30," alisema Gumbo na kuongeza:

"Pia tutaangalia kigezo cha mazingira, kiwanda husika lazima kiwe na mfumo uliobora wa kutolea taka, pia kiwanda au kampuni inapaswa kuwa na uhusiano mzuri na wafanyakazi wake kwa kuwaendeleza kimasomo. Pia tutaangalia ubora wa bidhaa zinazozalishwa, pamoja na uhusiano wa sekta zingine za kiuchumi," alisema.

Alisema tuzo hizo zimegawanywa katika makundi mbalimbali kama makundi ya viwandani ambao ndani yake kuna wazalishaji wa viwandani, waundaji bidhaa na wachakataji bidhaa.

"Pia kuna kundi la viwanda vikubwa ambapo tutaangalia mauzo ya kila mwaka ambayo yanapaswa kuwa zaidi ya Sh. bilioni 100, mtaji kwenye uwekezaji kwenye mitambo uwe zaidi ya Sh. bilioni mbili, na idadi ya wafanyakazi walioajiriwa wawe zaidi ya 100," alisema Gumbo.

Alisema kwa viwanda vya kati, mauzo ya mwaka yawe kuanzia Sh. milioni 500 hadi Sh. bilioni 1.99, mtaji wa uwekezaji katika mitambo uwe kuanzia Sh. bilioni moja hadi Sh. bilioni 99.9, idadi ya wafanyakazi iwe kuanzia 50 hadi 99.

Viwanda vidogo, vigezo ni mauzo yao kwa mwaka yaanzie Sh. milioni 10 hadi 499, mtaji wa uwekezaji usizidi Sh. bilioni moja na idadi ya wafanyakazi ianzie watano hadi 49.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa CTI, Leodegar Tenga, alisema idadi ya washiriki kwa mwaka huu imeongeza kutoka 48 mwaka jana hadi 61 mwaka huu.

Tenga alisema mgeni rasmi wa tuzo hizo ni Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, na kwamba tuzo hizo inalenga kutambua jukumu na mchango wa sekta ya viwanda katika uchumi, kutangaza umuhimu wa sekta ya viwanda na kukuza biashara nchini.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### VIWANJA / MASHAMBA

**SHAMBA LINAUZW**A, Hekari 25@Tshs 800,000/= ziko Miono Kijiji cha Mkange Wilaya ya Chalinze (kuelekea Sadani Game Reserve) mwendo dakika 40 toka barabara kuu iendayo Tanga. Wasiliana na 0713 604049 / 0784 604049.


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


### VYETI VIMEPOTEA



**JACKLINE B. LUGWISHA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1093-0012** kilichotolewa na ALDERSGATE SEKONDARI November, 2013. Cheti cha Ualimu chenye **index E0594-0017** kilichotolewa na SEMS TEACHERS COLLEGE May, 2016. Cheti cha Kuzaliwa namba **B.No 0391514.** Pamoja na Transcript ya cheti cha Ualimu. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/URA/RB/350102/2019.**

115461802

### CHETI KIMEPOTEA



**VICTORIA MWIGUNE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0181-0026** kilichotolewa na KISARAWE LUTHERAN JUNIOR SEMINARY mwaka 2009. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/KIJ/RB/383179/2019.**

115459002


### KUPOTEA KWA CHETI



FEBRONIA DEOGRATIUS KASONOKO anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.0989/0011 kilichotolewa na KIBARA SEKONDARI mwaka 2019.
Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi:
DAR/KIJ/RB/381324/2019.

115460902

### KUPOTEA KWA CHETI



JULIANA FULLA anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.0613/0062 kilichotolewa na NYAMPLUKANO SEKONDARI mwaka 1998.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi:
DAR/KIL/RB/44486/2019.


115460802

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**TUNZO BASHARI MSUYA**
anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili
**T 981 DNR ISUZU ELF.**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Control No:
**9910810302292.**

115461902

### KUPOTEA KWA CHETI



PASKALI MASUNZU anatangaza kupotea kwa cheti cha ualimu chenye namba 8756 kilichotolewa na Morogoro Teachers College mwaka 2012,

Yeyote atakaeiona atoe Taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
PWA/MAP/RB/165179/2019.

115457302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No; 204/2019**

**Ombi la PIUS MASUNGA MASANJA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ATHANAS PIUS MASUNGA MASANJA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 22/10/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 09/10/2019.



115462202

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**


**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;203/2019**

**Ombi la DEOGRATIUS MASELE ZILIZOBONELA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu MASELE ZILIZOBONELA YOHANA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 07/11/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 08/10/2019.



115462102


IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF DODOMA
AT DODOMA
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO….. OF 2019
In the matter of the Estate of the late PATRICK HARUNI ELISHA Of Ihumwa within Dodoma City
AND
IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY MSACHE PATRICK HARUNI

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filled on or before the 22ND Day of October, 2019.

Dated at Dodoma this 15TH day of October, 2019.



115462002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**


**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)**

**Katika mahakama ya mwanzo MWANG'OMBE**

**Usimamizi wa mirathi 52/2019**

**Ombi la MARIA NICHOLAS LEPTOS kuteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi ya Marehemu ASHA TANDE**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 25/10/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.
Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 12/9/2019.



1154461702

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ABUBAKARI YUSUF ABUU**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili
**T 137 AND.** Aina Yake FUSO. Yenye chassis namba **FK417K541956** na Engine number **6D16630313.** Yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo cha polisi, Taarifa ya Polisi:
**MOR/MOR/RB/380059/2019.**

115462402

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA
USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II
(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)
Katika mahakama ya mwanzo DODOMA MJINI
Usimamizi wa mirathi 74/2019

Ombi la SIMON ESMAIL NDOLOSI kuteuliwa

Msimamizi wa mirathi Marehemu ISMAILI ATHUMANI KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA.

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 8/11/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

Tarehe 15/10/2019



215461502

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
RUFAA/MADAI NO.31/2019
Katika Mahakama ya Wilaya DODOMA
Shauri la Rufaa jinai No.31/2019
Katika mahakama ya mwanzo ya DODOMA URBAN
SERAPIUS KIWAYA…………………MRUFANI
Dhidi ya
RAMADHAN ABDI…………………MRUFANIWA

KWA: RAMADHANI ABDI
Kwa kuwa Rufaa iliyotajwa hapo juu itasikilizwa katika Mahakama iliyotajwa hapo juu siku ya Jumatano tarehe 6/10/2019.unatakiwa uhudhurie katika Mahakama hiyo Mrufani/Mrufaniwa/Shahidi pamoja na vielelezo vyovyote kama vipo.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na mhuri wa Mahakama hii leo tarehe 15/10/2019.



115461602


**Uza,**

**Chenye Thamani Kubwa**

**Kwa Kutangaza Nasi**

**Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0767 223311**



**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




# CAVANI ATAKA KUJIUNGA JUVENTUS

**PARIS,** Ufaransa

HUKU mkataba wa Edinson Cavani ukitarajiwa kumalizika, nyota huyo sasa anataka kuondoka kwenye mji huo mkuu wa Ufaransa, kwa mujibu wa Calciomercato.

Mkongwe huyo wa Paris Saint-Germain awali alikuwa akihusishwa na mpango wa kuhamia katika klabu ya David Beckham inayoshiriki Ligi Kuu ya Marekani (MLS), Inter Miami.

Hata hiyo, sasa Cavani ameripotiwa kwamba anataka kurudi kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A, katika klabu ya Juventus.

Cavani awali alisema kwamba, anataka kumalizia soka lake katika klabu hiyo ya PSG, lakini sasa inaonekana ameamua kubadili maamuzi.

Cavani - ambaye amekuwa mfungaji wa wakati wote wa PSG tangu alipowasili hapo akitokea Napoli mwaka 2013, mkataba wake wa sasa unamalizika mwishoni mwa msimu.

Nyota huyo raia wa Uruguay mwenye umri wa miaka 32, tayari wawakilishi wake wameanza mazungumzo na Juventus ili aweze kurudi kule Italia.

# Kane asifu wenzake kuvumilia ubaguzi

**SOFIA,** Bulgaria

NAHODHA wa England, Harry Kane amesema anajisikia fahari juu ya wachezaji wenzake baada ya nchi yake kukumbwa na ubaguzi wa rangi wakati wa mchezo wa kufuzu michuano ya Euro 2020 dhidi ya Bulgaria.

Mchezo huo uliopigwa Jumatatu jijini Sofia ulikumbwa na ubaguzi wa rangi kwa wachezaji weusi wa England wakati wakiwafumua Bulgaria mabao 6-0.

Mchezo huo ulisimamishwa mara mbili kabla ya mapumziko wakati England wakipata ushindi huo mnono kwenye Uwanja wa Taifa wa Vasil Levski National, huku mashabiki wengi wa Bulgaria wakiondolewa uwanjani kwa zomea yao ya ubaguzi wa rangi.

Wachezaji wa England waliwataarifu maofisa wa mchezo huo wa tabia ya ubaguzi ya mashabiki na wakaamua kuendelea na mchezo huo wa Kundi A.

Baada ya mchezo, Kane ambaye alifunga bao la sita baada ya bao la ufunguzi la Marcus Rashford na Ross Barkley na Raheem Sterling ambao kila mmoja alifunga mawili, aliwaambia waandishi wa habari: "Kwa uhakika najisikia fahari kubwa kutoka kwa wachezaji wenzangu na marafiki wote waliohusika kwenye mchezo wa taifa letu usiku huu (juzi). Haukuwa usiku rahisi kwa kila mmoja.





# Griezmann 'alia' sare

**PARIS,** Ufaransa

ANTOINE Griezmann amesema Ufaransa inajisikia "uchungu" baada ya kucheza kwa kiwango cha juu zaidi, lakini wakaishia kutoka sare na Uturuki juzi Jumatatu kwenye mchezo wa kufuzu Euro 2020.

Ufaransa ilishindwa kupata nafasi ya kufuzu kwa michuano hiyo mwakani baada ya sare hiyo ya kufungana bao 1-1 na Uturuki mjini Paris.

Olivier Giroud aliyetokea benchi alionekana kama vile ameipa Ufaransa tiketi ya kufuzu Euro 2020 kwa bao la kichwa la dakika ya 78.

Hata hivyo, sherehe ya mabingwa hao wa dunia imelazimika kusubiri kwani bao la Kaan Ayhan la kusawazisha limeifanya sasa Ufaransa isubiri hadi mchezo mwingine.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya mchezo huo wa Kundi H, Griezmann aliwaambia waandishi wa habari: "Tuna huzuni, na sio kawaida kwa sababu tulicheza vizuri kwa kiwango bora, lakini hatukupata ushindi.

"Tulifunguka kwa kucheza kwa kushambulia kwa kasi, lakini tulishindwa kupata mabao mengi, hivyo tuna kazi nyingine ya kufanya kwenye mchezo unaofuata.

"Tunatakiwa kujifunza kutokana na makosa tuliyofanya na naamini tutakuwa kwenye nafasi nzuri tu katika mchezo ujao."

## HABARI MICHEZO




# SANCHEZ NJE YA DIMBA MIEZI MI3

**MILAN,** Italia

KOCHA wa Chile, Reinaldo Rueda amebainisha kwamba, winga wa Inter Milan, Alexis Sanchez anaweza kukaa nje kwa kipindi cha miezi mitatu na anatakiwa kufanyiwa upasuaji wa kifundo cha mguu baada ya kuumia akiichezea timu ya taifa.

Sanchez aliumia wakati akiichezea Chile dhidi ya Colombia ambapo mchezo huo ulimalizika kwa sare ya bila kufungana.

Akizungumza kupitia Football Italia, Rueda alithibitisha kwamba, Sanchez atalazimika kufanyiwa upasuaji, lakini utamfanya akae nje kwa muda mrefu.

Alisema: "Atafanyiwa upasuaji. Inter, klabu yake itaamua. Tunaweza kumpoteza kwa miezi miwili au mitatu.

"Ni aibu kwa sababu ameanza tena kuichezea Inter na kufunga mabao mawili, pia akicheza kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Alikuwa na furaha na hamasa kubwa kucheza tena. Sasa tunatakiwa kusubiri kwa maamuzi mengine zaidi."

Bila kujali ni kiasi gani ameumia, lakini hizi ni taarifa mbaya zaidi kwa Sanchez, ambaye amekuwa akicheza kwa mkopo akitokea Manchester United huku sasa akijaribu kurudisha ubora wake wa kucheza.

Baada ya kuwa na wakati mgumu wa kupata nafasi kwenye kikosi cha Inter, Sanchez alifunga bao kwenye mchezo wake wa kwanza kuichezea timu hiyo wakati ikiibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Sampdoria.

# Neymar akumbwa na majanga tena



**PARIS,** Ufaransa

NEYMAR atakuwa nje ya uwanja kwa muda wa wiki nne baada ya kuumia misuli ya paja wakati Brazil ikitoka sare ya kufungana bao 1-1 na Senegal Alhamisi iliyopita, kwa mujibu wa timu ya madaktari ya Paris Saint-Germain.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, alifikisha mechi 100 kuichezea Brazil maarufu kama Selecao kwenye mchezo huo uliopigwa nchini Singapore.

Alilazimika kutolewa nje ya uwanja katikati ya mchezo huo baada ya kupata majeraha. Neymar alikubwa na matatizo ya majeraha wakati wa msimu wa 2018/19, akikosa mechi 27 kuichezea PSG na zile za kimataifa.

Jumatatu, PSG ilithibitisha kwamba, nyota huyo atalazimika tena kuwa nje ys uwanja kwa muda mrefu baada ya kufanyiwa vipimo vya MRI, na ikatangazwa kwenye tovuti yao kwamba, mchezaji huyo atalazimika kukaa nje ya dimba kwa wiki nne tu.



# *Garcia kocha mpya Lyon akiwapiku Wenger, Blanc*

**LYON,** Ufaransa

LYON imemtangaza Rudi Garcia kuwa kocha wake mpya, akiwashinda Laurent Blanc na Arsene Wenger, huku Jose Mourinho yeye akikataa kukutana na viongozi wa klabu hiyo, kwa mujibu wa ESPN.

Garcia mwenye umri wa miaka 55, alionekana kuwa ndiye mtu sahihi kwa klabu hiyo baaada ya mchakato wa kutafuta kocha wao mpya.

Kocha wa zamani wa Arsenal, Wenger pia alikuwa akihusishwa na mpango wa kuchukua mikoba ya Sylvinho, ambaye alifukuzwa wiki iliyopita baada ya miezi miwili kazini, lakini hakuitwa kukutana na Mwenyekiti wa Lyon, Jean-Michel Aulas na Mkurugenzi wa soka, Juninho.

Blanc alikaribia kuwa kocha mpya wa klabu hiyo, baada ya kufanya mazungumzo mara mbili na klabu hiyo.

Kocha huyo wa zamani wa Paris Saint Germain alikuwa anapewa nafasi kubwa zaidi ya kuwa kocha wa klabu hiyo, lakini akapigwa chini.

Lyon ilitaka kuwa na kocha mwenye uwezo wa kuisaidia klabu hiyo kufanya vizuri kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa.

Mourinho, ambaye alikuwa hana kazi tangu alipoondoka Manchester United Desemba mwaka jana, alipewa ofa ya kukutana na uongozi wa klabu hiyo, lakini akaitolea nje.

Garcia aliisaidia Marseille kufika fainali ya Kombe la Europa Mei mwaka 2018, lakini walifungwa mabao 3-0 kutoka kwa Atletico Madrid mjini Lyon.

Mfaransa huyo pia alishafanya kazi katika klabu za Lille, Saint-Etienne na AS Roma.

# DON… ZA SOKA
## MA… YA ULAYA




# RONALDO NDANI YA SITA WALIOTUPIA MABAO 700

## Rekodi inakuja moja kwa moja - sikwenda kuzitafuta, zinanitafuta! Bila kuwa...

**KIEV,** Ukraine

MSHAMBULIAJI wa Ureno na Juventus, Cristiano Ronaldo amesisitiza kwamba hajali sana kuhusu kuvunja rekodi kwani hayo ni maisha anayoyaishi na kutokea ni kawaida kwake, kauli hiyo aliitoa baada ya kufunga bao lake la 700 katika wasifu wake kisoka kwenye klabu na timu ya taifa.

**Ronaldo aliisawazishia Ureno kwa penalti wakati wakiwa nyuma kwa bao moja katika kipindi cha pili kwenye mechi ya kuwania kufuzu Euro 2020 dhidi ya Ukraine ambayo waliangukia pua kwa mabao 2-1 juzi, Jumatatu jijini Kiev, Ukraine.**

Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 34, hakufanya makosa katika maguu hayo 12 ya mtu mzima baada ya Taras Stepanenko kuunawa mpira ndani ya boksi, lakini bao hilo halikutosha kuifanya Ureno kuepuka kupoteza mchezo kwa mara ya kwanza tangu Kombe la Dunia 2018.

Kipigo hicho kwa Ureno katika Uwanja wa Olympic kulifanya tukio hilo la Ronaldo kuwa tamu chungu, ambaye sasa ni sehemu ya wachezaji walioweza kufikia idadi hiyo ya mabao 700.

Josef Bican (raia wa Czech-Austria), ambaye aliichezea klabu ya Rapid Vienna, Slavia Prague kati ya mwaka 1931-1955 hadi sasa yeye ndiye kinara akiwa na mabao 805, akifuatiwa na Mbrazil Romario ambaye katika kipindi cha mwaka 1985-2007 alifunga mabao 772, klabu alizozichezea zikiwa ni Vasco da Gama, PSV na Barcelona.

Nafasi ya tatu inashikwa na Mbrazil Pele ambaye hadi anatundika daluga alikuwa na mabao 767, akiichezea Santos na New York Cosmos kuanzia mwaka 1957-1977.

Anayemfuata ni Ferenc Puskas raia wa Hungary, aliyetundika daluga na mabao 746 huku klabu alizozichezea zikiwa ni Budapest Honved na Real Madrid kati ya mwaka 1943-1966.

Nafasi ya tano inashikiliwa na Mjerumani Gerd Muller mwenye mabao 735 ambapo mbali na timu ya taifa aliichezea klabu ya Bayern Munich pekee kati ya mwaka 1962-1981.

Na mchezaji wa sita ni wa kizazi hiki cha 'doticom', Mreno Ronaldo ambaye juzi alifikia rekodi hiyo ya mabao 700, ambapo mbali na timu yake ya taifa mabao mengine ameyafunga akiwa na klabu ya Sporting CP, Manchester United, Real Madrid na Juventus, kuanzia mwaka 2002.

"Si kwamba ni yeyote tu anaweza kufikia idadi hii," aliwaambia wanahabari. "Shukrani kwa wachezaji wenzangu, wenzangu na makocha ambao wamenisaidia kuwa mchezaji kama nilivyo.

"Nimekatishwa tamaa kwa kutoshinda, bali fahari kwa timu."

Akimulika kuhusu mafanikio yake binafsi, Ronaldo aliongeza: "Ni rekodi kiasi gani nilizonazo? Sijui. Ninapaswa kufurahia wakati huu na kuwashukuru wale ambao walinisaidia kufikia alama hii ya kuvutia.

"Mara ya mwisho kucheza katika uwanja huu nilishinda Ligi ya Mabingwa Ulaya, wakati mzuri hiyo imepita. Leo tumecheza vizuri lakini hatukushinda. "Rekodi inakuja moja kwa moja - sikwenda kuzitafuta; rekodi zinanitafuta! Bila kuwa na umakini hufanyika kawaida."

## ZISIKUPITE

### ALLEGRI KUTUA NA EVRA UTD

KOCHA wa zamani wa Juventus, Massimiliano Allegri angemtaka beki wa zamani wa Manchester United, Patrice Evra - ambaye alimnoa akiwa Turin - kujiunga naye katika benchi la ufundi hapo Old Trafford kama atateuliwa kuinoa klabu hiyo. ***(Daily Mail)***

### NEYMAR NJE MWEZI MMOJA

PARIS St-Germain imethibitisha kuwa mshambuliaji Mbrazil Neymar, 27, atakuwa nje ya kikosi kwa wiki nne akiuguza misuli ya paja. (***Mirror)***

### AWATAKA EMERSON, KANTE

KOCHA wa zamani wa Chelsea, Maurizio Sarri amemtaka beki wa Italia Emerson Palmieri, 25, na kiungo wa Ufaransa N'Golo Kante, 28, kuondoka Stamford Bridge na kujiunga na Juventus. ***(Daily Express)***

### RABIOT CHAMBO YA ERIKSEN

MAURIZIO Sarri anataka kumnasa kiungo wa Tottenham, Christian Eriksen, na Juventus inaweza kumtoa ofa Adrien Rabiot, 24, kwa Spurs kwa kubadilishana na Mholanzi huyo. ***(Le 10 Sport via Mirror)***

### MILAN YAMMULIKA ELNENY

AC Milan inapanga kumfuata kiungo wa asiyehitajika Arsenal, Mmisri Mohamed Elneny, 27, katika dirisha la usajili la Januari, ambaye kwa sasa anacheza kwa mkopo Besiktas. (***Gazzetta - in Italian)***

### KUMSHANGAA POCHETTINO

KOCHA wa zamani wa Tottenham, Harry Redknapp amesema Mauricio Pochettino atakuwa "mpuuzi" kuachia ngazi ili kujiunga na Manchester United, ambaye anaamini "itamchukua miaka" kujjenga. ***(Mirror)***

### EMERY, ARSENAL IPO HIVI

KOCHA wa Arsenal, Unai Emery hana kipengele kinachomruhusu kuuvunja mkataba wake kwa kuununua mwishoni mwa msimu katika mkataba alliosaini mwaka 2018. (***The Athletic, via Express)***

### MANDZUKIC ANUKIA UNITED

MANCHESTER United inatumai Juventus itakubali kupokea pauni milioni tisa ili kumwachia straika wao, Mcroatia Mario Mandzukic, 33. (***Goal.com)***

### CHELSEA NAYO KWA ALLEN

CHELSEA ni moja kati ya klabu za Ligi Kuu England zenye moto wa kumfukuzia kiungo kinda Charlie Allen, 15, ambaye amechomoza katika kikosi cha kwanza cha Linfield ya Kaskani mwa Ireland. ***(Daily Express)***

### LINDELOF KAIPOTEZEA BARCA

VICTOR Lindelof, 25, amedai hakuwazia kabisa kuhusu suala la usajili ambao ulikuwa ukimhusisha na kutua Barcelona majira yote ya joto na Msweden huyo akionyesha "uaminifu" kwa Manchester United. ***(Goal.com)***

### GLAZER KUUZA HISA UNITED

MMILIKI mwenza wa Manchester United, Kevin Glazer, mmoja kati ya wamiliki sita wa Glazer wanaoiendesha klabu hiyo, anajiandaa kuuza asilimia zake 13. ***(The Sun)***

## HABARI MICHEZO

# AZAM WAZIDI KUKOMALIA MAKALI YA NYAVU LIGI KUU

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya kupata mabao saba katika mechi mbili za kirafiki walizocheza, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Iddi Cheche, amesema bado wanahitaji kuona safu ya ushambuliaji inafanya vema zaidi katika kila mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara watakayocheza.

Azam FC iliifunga Green Warriors mabao 5-0 na baadaye juzi ikawafunga African Lyon 2-0, katika mechi hizo mbili za kirafiki walizocheza za kujiandaa kuwakabili mabingwa watetezi wa ligi hiyo, Simba ifikapo Oktoba 23, mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Cheche, alisema wanahitaji kuona safu yao ya ushambuliaji inatumia nafasi zote wanazozitengeneza ili kuwa salama katika kila mechi wanayocheza.

**Cheche alisema Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu inaushindani zaidi ya msimu uliomalizika, kwa sababu idadi ya timu zinazotarajiwa kushuka daraja ni nyingi, hivyo kila klabu inataka kukimbia janga hilo.**

"Bado tunataka kuona timu inafunga zaidi, unapopata nafasi, unatakiwa uitumie vizuri, haya ni baadhi ya makosa ambayo tunatakiwa kuyafanyia kazi, huko mbele mambo yasije kuwa magumu, tunataka kufunga mabao zaidi ili kujihakikishia pointi tatu," alisema Cheche.

Aliongeza kuwa amefurahi kuona wachezaji waliokuwa majeruhi wamepona, na wamerejea katika kikosi hicho kinachowania ubingwa wa Bara kwa mara ya pili. "Tunaweza kucheza mechi nyingine ya kirafiki au la, tutaangalia hili na kufanya uamuzi, tunajua Simba ni moja ya timu ngumu, lazima tuwe imara kabla ya kukwakabili," Cheche alisema.

Simba iliyocheza mechi nne na kujikusanyia pointi 12 inaongoza katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara wakati Azam FC iliyoshuka dimbani mara tatu inafuatia ikiwa na pointi tisa huku Yanga yenye pointi nne iko katika nafasi ya 13, lakini imecheza mechi tatu.




Mratibu wa Shirika la OCCRI, Rehema Sanga (kulia), akiwa amemkabidhi Kombe Nahodha wa timu ya Expendable, Eric Costantine, kufuatia kuibuka washindi katika mchezo wa fainali wa michuano ya Kombe la Mbuzi dhidi ya Kivule FC uliochezwa katika Uwanja wa Shule ya Msingi Kivule jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mwakinyo, Mfilipino kuvaana U/Uhuru

**Na Faustine Feliciane**

BONDIA Mtanzania Hassan Mwakinyo, anatarajia kupanda ulingoni Novemba 29, mwaka huu jijini Dar es Salaam kupambana na bondia raia wa Ufilipino, Any Tinampay.

Pambano hilo la kimataifa la uzito wa Super Walter (Kilo 69) litakuwa la raundi 10 huku likitanguliwa na mapambano ya utangulizi kutoka kwa mabondia wa ndani na nje ya nchi.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mwakinyo, alisema amekubali kucheza pambano hilo la kimataifa kutokana na utayari wake wa kupata changamoto mpya.

"Niwashukuru wadhamini wangu Sportpesa na promota wangu kwa kuniletea pambano hili, nimejipanga vizuri na naendelea kujipanga kwa sababu sitaki niwaangushe Watanzania ambao wamekuwa wakinisapoti siku hizi," alisema Mwakinyo.

Alisema anaamini pambano litakuwa gumu na lenye changamoto kutokana na ukweli kuwa bondia Tinampay ni bondia mkubwa na anashika nafasi ya pili kwa ubora nchini baada ya Manny Pacqiao.

Kwa upande wake, promota wa pambano hilo Jay Msangi, alisema maandalizi yote yamekamilika na pambano hilo lina baraka zote kutoka serikalini kupitia kwa Baraza la Michezo nchini (BMT).

"Pambano litafanyika Uwanja wa Uhuru siku hiyo ya Ijumaa Novemba 29, hili tunalichukulia kama tukio la kitaifa kwa sababu Mwakinyo anaiwakilisha Tanzania," alisema Msangi.

Alisema kuwa kabla ya pambano hilo litakaloanza majira ya saa tatu usiku, kutakuwa na mapambano matano ya utangulizi na kutoa wito kwa kampuni kujitokeza kudhamini.

"Tunatarajia pambano hili litarushwa moja kwa moja kwenye televisheni na vipo vituo vya televisheni vya nje ya nchi kama Kenya na Ufilipino wameomba kurusha moja kwa moja nchini kwao kupitia kituo kitakachoonyesha hapa nyumbani," alisema.

Pambano hili la Mwakinyo linafanyika ikiwa ni miezi saba kupita tangu alipocheza pambano la mwisho ambalo aliibuka na ushindi.

## Tigo kutoa Renault Kwid kwa mshindi

**Na Mwandishi Wetu**

Kampuni ya simu ya Tigo imetangaza promosheni ijulikanayo kama Tigo Fiesta 2019 Chemsha Bongo kwa wakazi wa jijini Dodoma ambapo mshindi atajinyakulia gari aina ya Renault Kwid yenye thamani ya Sh. milioni 23.

Akizungumza wakati wa mkutano na waandishi wa habari uliofanyika Dodoma jana, Meneja wa Tigo Kanda ya Kaskazini, Lilian Mwalongo alisema promosheni hiyo inaenda sambamba na msimu wa 'Tigo Fiesta 2019-Saizi Yako' ambao ulizinduliwa jijini Mwanza na utamalizika jijini Dar es Salaam.

Alisema wateja wa Tigo wanaoshiriki katika promosheni hiyo kwa mara ya kwanza wana nafasi ya kushinda hadi Sh. milioni moja kila wiki huku mshindi wa jumla ataweza kujinyakulia gari mpya aina ya Renault Kwid yenye thamani ya Sh. milioni 23.

"Washindi wa promosheni hii watatangazwa kila wiki na ili kushiriki kwenye promosheni hii, wateja wanatakiwa kujisajili kwa kutuma neno MUZIKI kwenda 15571 au kwakutembelea tovuti www.tigomusic.co.tz nakuchagua neno 'Trivia'.

## Saba zathibitisha Chalenji wanawake

**Na Somoe Ng'itu**

BARAZA la Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa), limesema jumla ya timu saba zimethibitisha kushiriki mashindano ya Kombe la Chalenji kwa Wanawake ambayo yanatarajiwa kufanyika kuanzia Novemba 16 hadi 28, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili juzi, Katibu Mkuu wa Cecafa, Nicholas Musonye, alizitaja nchi zilizothibitisha kushiriki mashindano hayo kuwa ni pamoja na Uganda, Rwanda, Ethiopia, Eritrea, Kenya, Burundi na wenyeji Kilimanjaro Queens ya Tanzania Bara.

Musonye alisema maandalizi ya mashindano hayo yako katika hatua za mwisho na anaamini nchi nyingine wanachama zitathibitisha kushiriki michuano hiyo inayofanyika kwa mara ya tatu kwenye ukanda huu.

Musonye amezitaka nchi zote kufanya maandalizi mazuri ili kuendeleza ushindani uliozoeleka katika mashindano hayo.

"Mpaka leo (juzi) ni nchi saba ndizo zimethibitisha kushiriki mashindano haya, ila naamini nchi nyingine pia zitathibitisha na kufanya idadi ya timu kuongezeka, pia ninawakumbusha wote kuandaa timu zao, tunataka kuona ushindani kama mwaka jana kule Kigali, bingwa alijulikana siku ya mwisho ya mashindano," alisema Musonye.

Kilimanjaro Queens ndio mabingwa mara mbili mfululizo wa mashindano hayo ambayo yalianza kufanyika mwaka 2016 na mwaka huu yanachezwa kwa mara ya tatu.

# Michezo

Jumatano Oktoba 16, 2019

Nipashe




Ronaldo ndani ya sita waliotupia mabao 700

UKURASA 30

SOMA HIYO...




Kiboko ya Mashujaa, Kiungo wa Simba, Sharaf Eldin Shiboub, akipiga saluti kushangilia baada ya kuifungia timu yake bao pekee dakika ya 56 wakati wakishinda 1-0 dhidi ya wenyeji wao, Mashujaa FC kwenye mchezo wa kirafiki uliopigwa Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma juzi. **NA MPIGAPICHA WETU**

# SIMBA, YANGA HAKUNA KULALA

## ●●● Aussems kuwatolea uvivu Warundi leo huku kikosi cha Zahera chini ya Mwandila kikiwa...

**Na Somoe Ng'itu**

KATIKA kujiimarisha kuelekea mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya mapumziko kupisha Kalenda ya Fifa, zinazotarajiwa kuendelea hivi karibuni, Simba inatarajia kuikaribisha Aigle Noir kutoka Burundi kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika huku Yanga wakishuka kwenye Uwanja wa Uhuru kujipima na Pan Africans inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza.

**Mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba wenyewe wanajiimarisha ili kuivaa Azam FC hapo Oktoba 23, mwaka huu, wakati Yanga itakuwa ugenini jijini Mwanza kuvaana na Mbao FC kwenye Uwanja wa CCM Kirumba, Oktoba 22, mwaka huu.**

Kocha Mkuu wa Simba, Patrick Aussems, amesema watashuka uwanjani katika mchezo huo kwa ari ya juu ili kuwapa furaha mashabiki wao, licha ya kuwapo kwa changamoto ya uwanja.

Aussems alisema kiufundi, mechi hiyo ya leo pia itaendelea kuwaimarisha wachezaji wake na anaamini zimenyanyua viwango vyao na kuwa tayari kupambana kuivaa Azam FC.

"Uwanja si rafiki, huwezi kucheza wala kuonyesha kiwango chako halisi, lakini nina furaha kuona mashabiki wamejitokeza kwa wingi kuja kuiona timu yao, nina matumaini tutawapa burudani wanayoitarajia," alisema kocha huyo raia wa Ubelgiji.

Noel Mwandila, Kocha Msaidizi wa Yanga, alisema mchezo wa leo dhidi ya Pan Africans si tu utawaimarisha kuelekea kuivaa Mbao FC bali pia ni mwendelezo wa kukiimarisha kikosi chao ambacho Oktoba 27, mwaka huu kitawakaribisha Pyramids kutoka Misri katika mchezo wa hatua ya mtoano wa mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Mwandila alisema kila mchezo wanaocheza ni muhimu kwao, hivyo wanawataka mashabiki na wanachama wa Yanga kuendelea kuungana katika kipindi hiki wanachopambana kuhakikisha wanatinga hatua ya makundi ya michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika inayowakabili.

Aliongeza kuwa wachezaji waliokuwa majeruhi wamepona, na wote wanatarajiwa kuwapo kwenye kikosi kitakachoondoka jijini Dar es Salaam Jumapili kuelekea Mwanza.

Baada ya mchezo dhidi ya Mbao FC, Yanga ambao ndio wawakilishi pekee wa Tanzania waliobakia katika mashindano ya kimataifa yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (Caf), wataendelea na maandalizi ya kuwakaribisha Pyramids.

# Stars kamili yatua Sudan

**Na Mwandishi Wetu**

KIKOSI cha timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars) kimewasili salama jijini Khartoum tayari kuwakabili wenyeji wao, Sudan katika mchezo wa marudiano wa kuwania tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), itakayochezwa kesho utwa Ijumaa kwenye Uwanja wa El Merreikh Omdurman.

Taifa Stars imetua Khartoum ikitokea Kigali, Rwanda ambako ilicheza mechi ya kirafiki dhidi ya wenyeji wao Amavubi na mchezo huo ulimalizika kwa suluhu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo, alisema wameamua kwenda Khartoum mapema ili kutoa nafasi kwa wachezaji kuendelea na mazoezi ya kuwavaa wenyeji wao.

Ndimbo alisema wanashukuru baada ya mechi dhidi ya Amavubi, hakuna mchezaji aliyeumia, hivyo nyota wote wanaocheza katika Ligi Kuu Tanzania Bara, waliondoka kuelekea Khartoum na wale wanaocheza nje ya nchi, walirejea Dar es Salaam na baadaye kuanza safari ya kurudi katika klabu zao.

"Timu imeshafika Sudan tangu alfajiri (jana), tunataka tufanye maandalizi kwa utulivu na umakini, tunajua mechi iliyoko mbele yetu ina changamoto, tunataka kusonga mbele katika mashindano hayo," alisema Ndimbo.

Kuhusu mchezo dhidi ya Rwanda, Kocha Msaidizi wa Taifa Stars, Juma Mgunda, alisema jana kuwa mchezo huo umesaidia kuwapa mwanga kuelekea mechi yao ya Ijumaa.

"Mechi ya kirafiki huwa inalenga vitu vingi kiufundi, ndio maana hutoa nafasi kubwa kwa wachezaji wengi kuonekana, kuna vitu mbalimbali tunaviangalia ili kuboresha na kuangalia mapungufu," alisema Mgunda.

Stars itashuka dimbani keshokutwa ikiwa na kumbukumbu ya kufungwa bao 1-0, katika mchezo wa kwanza waliocheza Uwanja wa Taifa hapa nchini.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >